TURKU UNIVERSITY DEPARTMENT OF GEOGRAPHY PUBLICATIONS B

Nr 15

MAENDELEO YA MAKAZI VIJIJINI BAADA YA UJAMAA, MAGHARIBI MWA WILAYA YA BAGAMOYO, TANZANIA

Cosmas H. Sokoni
(Mhariri)

TURKU 2010

YALIYOMO

Utangilizi **4**
Cosmas H. Sokoni

Mabadiliko ya makazi vijijini Tangu Enzi ya Ujamaa magharibi mwa Wilaya ya Bagamoyo **11**
Taimi Sitari

Ongezeko la watu na athari zake katika misitu magharibi mwa Bagamoyo, Tanzania **25**
Emmanuel Mhache

Uhakika wa Umiliki wa Ardhi, Mpango wa Matumizi Ardhi wa Kijiji na Raslimali ya Misitu magharibi mwa Wilaya ya Bagamoyo **37**
Jussi Ylhäisi

Maendeleo ya mfumo wa chakula vijijini baada ya enzi ya Ujamaa. Uchunguzi kifani kutoka Lugoba, Tanzania **55**
Toni Haapanen

Uhusiano wa miji na vijiji na mchango wake katika maendeleo vijijini **74**
Cosmas H. Sokoni

SHUKRANI

Tunawashukuru wote waliotuwezesha kufanya utafiti huu: The Academy of Finland waliotoa fedha za utafiti; uongozi wa Chuo Kikuu cha Turku na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kutupa nafasi ya kufanya utafiti; uongozi wa serikali mkoa wa Pwani; Wilaya ya Bagamoyo, tarafa, kata na vijiji vilivyofanyiwa utafiti kwa kutuwezesha na kutupa ushirikiano wakati wa utafiti. Tuawashukuru pia wananchi walioshirikishwa katika tafiti hizi kwa nafasi mbali mbali kwa mchango wao wa mawazo. Hata hivyo, mawazo yaliyoko humu ni ya kila mtafiti mwenyewe ambaye amebeba jukumu juu yake.

UTANGULIZI

Cosmas H. Sokoni, Idara ya Jiografia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Mabadiliko ya Muundo wa Makazi Vijijini

Tanzania ilifanya mabadiliko makubwa katika muundo na mfumo wa makazi vijijini katika miaka ya sabini (1970s) kupitia operesheni vijiji. Inakadiriwa kuwa kati ya watu milioni saba nadi tisa walihamishwa kutoka makazi madogo madogo na yaliyotawanyika kwenda vijiji vya ujamaa vilivyokuwa vikubwa na vyenye nyumba zilizojengwa karibu karibu na kwa mpangilio wa gridi. Katika mkoa wa Pwani tukio hili liliitwa Operesheni Pwani, 1974-5. Mabadiliko haya ya muundo wa makazi ya vijijini yalitarajiwa kuongeza uzalishaji wa kilimo kwa kurahisisha kilimo cha pamoja cha mashamba makubwa, kwa kutumia zana za kisasa, na hivyo kuongeza uhakika wa upatikanaji wa chakula. Pia operesheni ililenga kufikisha huduma za kijamii karibu zaidi kwa wananchi ambazo ni za muhimu katika kuongeza tija katika kilimo (Silberfein, 1989). Hata hivyo, mapinduzi ya kilimo yaliyotarajiwa katika eneo la magharibi mwa Wilaya ya Bagamoyo, hayakupatikana. Mashamba makubwa ya pamoja hayakuweza kudumu na mbinu za kisasa za kilimo hazikuweza kuendelezwa. Ingawa malengo ya kuongeza uzalishaji wa kilimo hayakuweza kupatikana kama ilivyotarajiwa, mabadiliko katika makazi yamekuwa ya kudumu. Makazi ya vijiji yamekuwa ya kudumu na kilimo cha kuhama hama kimebadilika kuwa cha mashamba ya kudumu.

Tafiti nyingi zilifanyika ili kutathmini matokeo ya uanzishaji wa vijiji vya ujamaa. Tafiti nyingi ziliangalia athari za mfumo mpya wa vijiji katika uzalishaji wa kilimo na katika mazingira (Boesen et al, 1977; Kikula, 1997; Lawi, 2007). Tafiti hizi zilitilia mkazo juu ya mapungufu ya mfumo mpya wa vijiji: kwa mfano uharibifu wa mazingira maeneo ya karibu na vijiji ; kupungua kwa tija katika uzalishaji wa mazao kutokana na kuongezeka kwa umbali kati ya makazi na mashamba (McCall, 1985). Uzuri wa ujamaa unaotokana na kubadilika kwa mfumo wa makazi haukupewa uzito mkubwa. Utafiti wa Sitari (1983) juu ya mabadiliko ya mfumo wa makazi ya vijiji magharibi mwa

wilaya ya Bagamoyo kati ya 1950s na 1979 unazingatia manufaa ya mfumo wa vijiji ulioanzishwa katika kutoa fursa mbalimbali za wananchi kujipatia riziki zao. Utafiti huo ulikuwa ni sehemu ya mradi mkubwa wa utafiti juu ya wajibu wa utamaduni katika kuunda upya maisha ya vijijini Tanzania (The Role of Culture in the Restructuring of Rural Tanzania) uliofadhiliwa na Academy of Finland na kutekelezwa na Taasisis ya Taalamu za Maendeleo, Chuo Kikuu cha Helsinki.

Tokea wakati huu, kumetokea mabadiliko makubwa kiuchumi na kisiasa nchini Tanzania. Kuanzishwa kwa uchumi unaofuata soko huria katika miaka ya themanini kumemaliza enzi ya ujamaa nchini. Mifumo mipya ya kupata na kutumia raslimali imeanzishwa vijijini. Kutokana na kipindi kirefu kilichopita hadi sasa na mabadiliko mbali mbali yaliyotokea, kuna haja tena ya kutathmini athari ya mfumo wa makazi ya vijijini ulioanzishwa wakati wa ujamaa kwenye maendeleo vijijini. Makala zilizopo katika ripoti hii, zinatokana na utafiti juu ya Maendeleo ya Makazi vijijini, Umiliki wa Ardhi na Uhakika wa Chakula toka enzi ya ujamaa Mashariki mwa Tanzania (Rural Settlement Development, Land Ownership and Food Security since Ujamaa Era in Eastern Tanzania). Utafiti huu kwa kiasi fulani unafuatilia utafiti wa awali (Sitari, 1983) na umefadhiliwa na the Academy of Finland. Kikundi cha watafiti kimejumuisha Idara ya Jiografia ya Chuo Kikuu cha Turku, Finland na Idara ya Jiografia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Utafiti unajumuisha pia watafiti wazoefu watatu na wanachuo wawili walioko katika mafunzo ya digrii ya uzamifu (Doctor of Philosophy). Utafiti huu umezingatia mabadiliko ya muundo wa makazi vijijini; utumiaji wa raslimali za misitu; mabadiliko katika matumizi ya ardhi; mfumo wa chakula na uhakika wa kupata chakula na uhusiano kati ya miji na vijiji.

Lengo la utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

1. Kuchunguza utekelezaji wa malengo ya siasa ya ujamaa na kwa kiasi gani athari zake bado ziko vijijini.
2. Kuchunguza kwa kiasi gani jamii za vijijini na wakulima binafsi wamejibu shinikizo katika matumizi ya ardhi na mazingira linatokana na mabadiliko ya sera za taifa.
3. Kutafiti juu ya mabadiliko ya maendeleo ya uchumi na mfumo wa chakula katika vijiji vya utafiti kwa kuzingatia hali ya uhakika wa upatikanaji wa chakula na sababu zinazochangia hali hiyo.

4. Kuchunguza hali ya utekelezaji wa sheria mpya za ardhi na raslimali za misitu katika vijiji vya utafiti.
5. Kuchunguza muingiliano kati ya vijiji na miji na mchango wake katika maendeleo ya vijijini.

Kila mmoja wa watafiti katika timu hii alijihusisha katika lengo mojawapo. Hata hivyo kunauwezekana mkubwa kuwa mada hizi zinaingiliana. Watafiti walikuwa huru kuweka wazi zaidi mada zao na kuchagua maeneo (vijiji) vya kufanyia utafiti.

Eneo la utafiti

Kwa vile utafiti huu ulilenga kufuatilia matokeo ya utafiti wa awali wa Sitari (1983), ilibidi ufanyike maeneo yale yale ya magharibi mwa Wilaya ya Bagamoyo. Utafiti ulifanyika katika maeneo ya vijijini yaliyoko pembezoni mwa barabara kuu itokayo Chalinze kwenda Segera (Tanga). Vijiji vingi vilichaguliwa kando kando mwa barabara, lakini baadhi ya vijiji kama Kiwangwa na Miono viko mbali na barabara kuu. Eneo hili liko pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam lenye ongezeko la idadi ya watu na shughuli za uchumi unaokua kasi. Miundo mbinu mizuri ya barabara inarahisisha mawasiliano katika eneo hili la utafiti na jiji la Dar es Salaam na miji mingine midogo ya Bagamoyo, Chalinze, na Kibaha. Kata zilizofanyiwa utafiti ni Kiwangwa; Mbwewe; Msata; Lugoba na Miono (Mchoro 1). Eneo la utafiti limepata mabadiliko makubwa ya miundo mbinu ya barabara na maji hivi karibuni.



Mchoro 1: Maeneo yaliyofanyiwa utafiti

Mbinu za utafiti zilizotumika

Watafiti wametumia mbinu mbali mbali za kukusanya takwimu za utafiti huu. Katika utafiti wake wa mabadiliko ya makazi, Taimi Sitari amezifuatilia kaya alizozitembelea wakati wake wa awali, na kufuatilia shughuli za wanakaya ili kutambua mabadiliko yaliyotokea. Kwa kuangalia sehemu alizozipitia awali ameweza kung'amua mabadiliko katika hali ya makazi. Watafiti wengine wametumia mbinu ya kuhoji kwa kutumia dodoso, zilizowezesha kupatikana takwimu zinazoweza kuchambuliwa kwa kutumia kompyuta. Pia mahojiano na watu maalum wenye uelewa mkubwa wa mada husuka ulifanyika. Watu waliohojiwa ni viongozi wa kata, vijiji; wataalamu katika ngazi hizo; wawakilishi wa makundi ya kijamii; watoa huduma mbali mbali. Majadiliano kati ya watafiti na vikundi maalum vilivyohusisha wadau mbali mbali katika mada husika yalifanyika katika ngazi za kata na vijiji. Ili kuchunguza mabadiliko ya matumizi ya ardhi, picha za angani na za satelaiti zilitumika.

Matokeo ya utafiti

Matokeo ya utafiti yanazangatia maeneo makuu matano kama yanavyoelezwa kwa kirefu katika makala za watafiti zilizojumuishwa katika ripoti hii.

Taimi Sitari amechunguza juu ya mabadiliko ya makazi. Licha ya udhaifu ulijitokeza katika uzalishaji na utunzaji wa mazingira karibu na vijiji vilivyoanzishwa, ni dhahiri kuwa vijiji hivi vimedumu na kuendelea kukua. Tofauti na sehemu zingine ambako imeripotiwa kuwa wananchi wameyarudia makazi yao ya awali kabla ya kuanzishwa vijiji, katika eneo hili la magharibi mwa Bagamoyo, wananchi wamebaki katika vijiji vilivyoanzishwa. Taimi amefuatilia kaya ilizozitembelea katika utafiti wake wa awali (Sitari, 1983) ili kuchunguza mabadiliko katika fursa za kazi, huduma za jamii, uzalishaji wa kilimo, n.k. Utafiti huu unaonyesha kuwa japo hakuna mapinduzi katika uzalishaji wa kilimo, maisha ya wananchi yamekuwa bora zaidi kuliko awali. Miundo mbinu na huduma za kijamii zimeboreshwa kwa kiasi fulani. Hii ndiyo sababu inayowafanya wananchi waendelee kuishi katika vijiji hivi. Utafiti huu unatambua kukua kwa hali ya maisha ya kimji katika vijiji vikubwa vilivyoko kando kando mwa barabara kuu. Mawasiliano rahisi zaidi kati ya miji na vijiji yamefungua fursa mpya za ajira zisizo za kilimo. Ni dhahiri kuwa mwelekeo huu wa kukua kwa vijiji, kudidimia kwa kilimo na kuibuka kwa shughuli zisizokuwa za kilimo kunahitaji mwongozo wa watunga sera na wapangaji wa mipango.

Utafiti wa Emmanuel Mhache unalenga katika kuelewa uhusiano kati ya kuongezeka kwa idadi ya watu na matumizi ya raslimali ya misitu katika

eneo la utafiti. Kutokana na uchambuzi wa picha za satelaiti, misitu iliyo katika eneo la utafiti imeharibiwa na kupungua kwa kiasi kikubwa. Kutokana na kutofanikiwa kwa mapinduzi ya kilimo yaliyotarajiwa wakati wa uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa, na hasa kuzorota kwake, matumizi ya maliasili ya misitu yamekuwa njia kuu ya kukidhi mahitaji ya wananchi katika eneo hili la utafiti. Uchomaji wa mkaa kwa ajili ya kuuza umezishughulisha kaya nyingi. Miji mikubwa kama Dar es Salaam imekuwa soko kubwa la mkaa unaozalishwa katika eneo la utafiti. Uchomaji wa mkaa hupunguza gharama za maisha kwa wakazi wa mijini, lakini kwa wakati huo huo unazigharimu sana jamii za vijijini kutokana na uharibifu wa mazingira. Zaidi ya hayo, watumiaji wa bidhaa zitokanozo na misitu hawalipi gharama inayostahili ya maliasili hizo. Sera na mipango ya maendeleo izingatie utozaji wa ushuru unaostahili kulipia gharama ya maliasili hizi na matumizi bora ya kodi iliyokusanywa kwa ajili ya kuboresha maisha ya wanavijiji.

Tokea kuachwa kwa ujamaa vijijini kumekuwa na mabadiliko katika mfumo wa umiliki wa ardhi na mpango wa matumizi ya ardhi. Jussi Ylhaisi ametafiti juu ya utekelezaji wa sheria mpya zinazohusiana na matumizi ya ardhi katika eneo hili la utafiti. Mfumo wa soko huria umeweka uwazi zaidi wa umiliki na ugawanyaji wa ardhi kupitia kwenye soko. Hata, hivyo Tanzania imekuwa ni nchi pekee iliyodumisha umilikishaji wa ardhi kwa jamii kupitia mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi katika vijiji. Mtafiti huyu amefuatilia utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji. Vijiji mbali mbali viko katika hatua tofauti za utekelezaji wa mpango huu. Hata hivyo pale ambapo utekelezaji wake umefanikiwa, umetoa fursa ya vijiji kuwa na matumizi ya ardhi ulioendelevu zaidi. Kwa kupanga maeneo ya matumizi mbali mbali ya ardhi imesaidia kwa mfano kupunguza msuguano katika watumiaji wa ardhi. Imesaidia pia kuhifadhi maeneo ya maliasili yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi. Utafiti huu unashauri kuwe na kazi zaidi ya kuanzishwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa kila kijiji ili kuwe na matumizi ya ardhi yaliyo sahihi na endelevu katika vijiji.

Lengo la kuanzishwa vijiji vya ujamaa lilikuwa kuongeza tija katika kilimo na hivyo kuongeza uhakika wa upatikanaji wa chakula katika vijiji. Utafiti wa Toni Haapanen umezingatia mabadiliko katika mfumo wa chakula na uhakika wa chakula katika eneo hili la utafiti. Kutokana na kudadisi ulaji wa chakula katika kaya na uwepo wa vyakula mbali mbali katika masoko ya vijijini, imedhihirika kuwa kumekuwa na mabadiliko katika chakula kinachozalishwa na kuliwa na wakazi wa vijijini. Enzi za ujamaa wakazi wengi vijijini walikula chakula walichozalisha wenyewe. Lakini katika miaka ya hivi karibuni, wanavijiji wamezidi kutumia chakula ambacho hawakuzalisha wao wenyewe. Mara nyingi chakula kama mahindi, mchele, na nafaka

zingine huletwa kutoka mikoa jirani. Angalizo hili linaendana na matokeo yaliyodokezwa hapo mwanzo kuwa mfumo wa vijiji vya ujamaa haukufaulu kuleta mapinduzi katika kilimo. Hali hii ni tishio katika kuwa na uhakika wa kupata chakula vijijini. Pia unaonyesha kukua kwa hali tegemezi ya chakula katika kaya zilizoko vijijini.

Utafiti wa Cosmas Sokoni unachunguza hali ya muingiliano kati ya miji na vijiji. Miji na vijiji daima huingiliana. Watu, bidhaa na huduma hutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Mtafiti anachunguza ni kwa kiasi gani muingiliano huu unaweza kuwa mtaji wa kuleta maendeleo vijijini. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa muingiliano huu huwezesha miji hasa jiji la Dar es Salaam kufaidi kwa kupokea watu na bidhaa toka vijijini, lakini uwezo wa miji midogo na mikubwa kuendeleza vijiji ni duni. Ili kujenga hoja, mtafiti anatumia taarifa alizokusanya kutoka kwa ndugu walioko vijijini juu ya jamaa zao waliohamia mijini. Manufaa ya muingiliano kati ya wanandugu au jamaa walioko mijini na vijijini ni kidogo kutokana na hali duni ya wahamiaji wanaoishi mijini. Hata hivyo anatambua nguvu ya wahamiaji, japo wachache wenye raslimali na uwezo wa kuchangia maendeleo ya vijiji vyao. Pia kuna mchango ya wakaaji wa mjini wasiowenyeji wa vijiji hivi, lakini waliowekeza vijijini. Mtafiti unashauri uongozi vijijini kutumia nguvu hii ili kuchochea maendeleo vijijini.

Makala hizi tano zilizomo katika ripoti hii zinaeleza kwa kifupi na kwa lugha rahisi juu ya utafiti huu na matokeo yake. Machapisho mbali mbali juu ya matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoka katika majarida mbali mbali ya kitaaluma siku za usoni.

Machapisho

Boesen J., B. Storgård Madsen, T. Moody (1977). *Ujamaa – socialism from above*. 181 p Scandinavian Institute of African Studies. Uppsala.

Kikula, I.S. (1997). *Policy implications on environment. The case of villagisation in Tanzania*.The Nordic Africa Institute, Uppsala.

Lawi, Y. Q. (2007). Tanzania's Operation Vijiji and local ecological consciousness: The case of eastern Iraqw Land, 1974-1976, *Journal of African History, 48*, 69–93.

McCall, M.K. (1985). The significance of distance constraints in peasant farming systems with special reference to Sub-Saharan Africa, *Applied Geography 5 (4)*, 325-345

Silberfein, M. (1989). Settlement form and rural development: Scattered versus clustered settlement, *Tijdschrift voor Econ. en Soc. Geografie 80 (5)*, 258 -268

MABADILIKO YA MAKAZI VIJIJINI TANGU ENZI YA UJAMAA MAGHARIBI MWA WILAYA YA BAGAMOYO

Taimi Sitari, Idara ya Jiografia, Chuo Kikuu cha Turku, Finland

Utangulizi

Wakati wa ujenzi wa vijiji vya ujamaa, Timu ya watafiti wa Tanzania na Ufini, kupitia mradi wa 'Jipemoyo' ilifanya utafiti juu ya maendeleo katika eneo la magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo. Eneo hili lilijumuisha kata za Lugoba, Miono na Msata. Utafiti huu ulizingatia nafasi (role) ya utamaduni katika kuleta mabadiliko katika kuviunda upya vijiji vya Tanzania na uliongozwa na Profesa Marja-Liisa Swantz. Matokeo ya utafiti huu yalichapishwa katika majarida kadhaa (e.g. Sitari 1983, Hurskainen 1984, Jerman 1997, Vuorela 1987, Kiyenze 1985, Mustafa 1989). Utafiti wangu (Sitari, 1983) uliangalia mabadiliko katika mpangilio na muundo wa vijiji. Katika utafiti huu wa sasa, nimetembelea tena maeneo yale yale ya utafiti ili kujifunza mabadliko yaliyotokea toka kuundwa kwa vijiji vya ujamaa.

Kwa wakati huu, muda wa kutosha umekwishapita wa kutuwezesha kujadili juu ya aina mbali mbali za athari zilizojitokeza katika eneo hili kutokana na kuundwa kwa vijiji. Ni wazi kuwa uundaji wa vijiji haukufanikiwa kutimiza malengo yake, hasa yale ya kiuchumi. Hata hivyo, ukubwa wa operesheni na mabadiliko ya mfumo yaliyotokea, hayana budi kuwa yameleta athari kubwa katika jamii.

Mabadiliko wakati Ujamaa

Uhamiaji katika Vijiji

Operesheni vijiji ilitekelezwa kwa namna tofauti kama kutumia nguvu na ushawishi. Utekelezaji wa operesheni vijiji ulitofautiana katika sehemu mbali mbali za nchi kwa kutegemea ushujaa wa kisiasa (political zeal) na mbinu

za kiutawala za makada wa chama tawala na watumishi wa serikali katika mikoa, wilaya hadi vijiji (McHenry 1976). Katika sehemu hii ya magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo, uundaji wa vijiji vya ujamaa (hasa) ulihusisha kuwakusanya watu katika vijiji vikubwa vichache vilivyokuwa pembeni au pembezoni mwa barabara kuu. Watu walihamishwa kutoka vijiji vidogo vya pembezoni kwa mfano Gwami na maeneo ya Mkoko, kwenda katika vijiji vikubwa. Ingawa uhamiaji ulikuwa lazima, utekelezaji wake haukuwa mara zote wa kushurutisha. Kutokana na operesheni viliundwa vijiji vya ujamaa 70 katika wilaya nzima ya Bagamoyo. Idadi hii ni asilimia 43 zaidi ya vijiji 49 vilivyopangwa kuundwa kupitia mpango wa mkoa wa kutekeleza sera ya vijiji vya ujamaa ulioitwa Operesheni Pwani. Watu walioishi katika vijiji vidogo pembezoni au karibu na barabara kuu walikataa kuhama kwenda vijiji vikubwa na hatimaye waliruhusiwa kuandikisha vijiji vyao (Sitari, 1983). Vijiji hivyo ni kama Kihangaiko, Mazizi, Msoga and Saleni. Kutokana na baadhi ya wakazi kukataa kuhama kutoka vijiji vyao, aina mbali mbali za vijiji vilivyoandikishwa ilijitokeza. Baadhi ya vijiji vilikua na kuwa vikubwa vyenye makazi yaliyosongamana. Vijiji vingine vingi viliendelea kuwa na kitovu kimoja au vitovu vingi ambako wakazi walikataa kuhama. Mfano wa hali hii ni Lunga na Mboga. Hii ilizaa vijiji vyenye mlolongo wa makazi pembezoni mwa barabara kuu. Kwa upande mwingine, vijiji vya Kinzangu, Makombe na Salemi havikufikia kiwango cha chini cha kaya 250 zilizohitajika kuunda kijiji, viliunda kijiji kikubwa chenye vitovu vingi. Kijiji cha Mindu Tulieni cha wamasai-waparakuyo, kilitawanyika na kuenea kila mahali kati ya vijiji vingine. Hali hii iliwezekana kwa kuwa wakati huo mipaka ya vijiji haikuwa imewekwa kikamilifu (Sitari, 1983).

Uchambuzi wa ramani na picha za angani za miaka ya 1950 unaonyesha kuwa kusogea kwa makazi karibu na barabara kuu kulianza kabla ya uundwaji wa vijiji vya ujamaa (Sitari 1083:25 -28). Inawezekana hii ilitokana na kumalizika kwa ukoloni, kupatikana kwa uhuru na ujenzi wa taifa. Tunaweza kusema kuwa ujenzi wa vijiji vya ujamaa uliharakisha hali hii ya maendeleo ya makazi. Hii ina maana kuwa hali ya kufikika kwa makazi kwa ajili ya huduma za jamii na miundo mbinu ilifanywa kuwa rahisi zaidi.

Mpangilio wa Makazi ya vijiji

Vijiji vilivyoanzishwa viliendelezwa kwa kutumia mpangilio wa gridi za mraba /mstatili na nyumba ya kaya zilijengwa katika ploti za ekari moja zilizopangwa kwa mstari. Hii ilikuwa tofauti na mfumo wa jadi wa kujenga nyumba karibu karibu katika maeneo ya wazi na kufanya mafungu mafungu madogo ya majengo. Katika mpangilio mpya barabara /njia zinapita kati ya ploti zikifanya

pembe mramba katika mapishano, badala ya kutoka nyumba hadi nyumba ilivyokuwa awali. Badili hilo lina maana kuwa sasa nyumba zilijengwa katika plot pekee badala ya kulundikana katika mafungu yaliyoundwa makundi ya familia au koo (Sitari, 1983).

Wahamiaji katika vijiji vipya walijenga desturi ya kuhamia upande wa kijiji ambako wametokea, na karibu na wanakijiji wengine waliotoka sehemu sawa na zao (Sitari, 1983:55). Hii haikushangaza kwa kuwa wahamiaji walihamia kwa makundi yaliyotoka sehemu moja na kugawiwa viwanja kwa pamoja. Hii pia ilikuwa na manufaa kwa kuwa iliwathibitishia wahamiaji hali ya kufahamiana na usalama katika mazingira mapya.

Mjadala juu ya Zoezi la Kuanzisha Vijiji

Zoezi la kuanzisha vijiji vya ujamaa katika nchi nzima lilitangazwa mwaka 1973 na lilichangiwa na hali mbaya ya mafuta na miaka miwili mfululizo ya kuzorota kwa uzalishaji wa mazao, ambao ulidhoofisha hazina ya fedha za kigeni ya nchi.

Lengo kuu la uundaji wa vijiji vya ujamaa ilikuwa kuboresha uzalishaji wa kilimo na kwa hiyo maendeleo ya maeneo ya vijijini. Hii ilitarajiwa kufanikiwa kwa kuongeza uzalishaji katika kilimo kwa kuunda kilimo cha pamoja (ujamaa) cha mashamba makubwa zaidi na kwa hiyo kuwezesha utumiaji wa mashine za kilimo. Lengo lingine ilikuwa kuwahamishia watu katika vijiji vikubwa vilivyosongamana kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii na miundo mbinu, hasa ya elimu na afya kwa urahisi zaidi. Vijiji vilitarajiwa kujitawala, na lengo lilikuwa kuishi, kufanya kazi na kupanga shughuli za maendeleo kwa pamoja (Nyerere, 1967).

Uanzishwaji wa vijiji ulikuwa na malengo ya kijamii na kiuchumi. Wakati huo, sera ya elimu ya msingi kwa wote ilitangazwa. Lakini, mijadala juu ya mafanikio ya kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa umeangalia zaidi vipengele vya kiuchumi, na imethibitisha kuwa mabadikiliko ya kitekinolojia katika kilimo hayakutokea kama ilivyokuwa imetarajiwa (e.g. Kikula 1997, Ponte 2002, Schneider 2007, Edwards 1998). Ukilinganisha na programu nyingine za kuanzisha kilimo kwa ushirika, inaonekana kuwa mafanikio yake ni kidogo au hayapo (McHenry 1976). Katika eneo la utafiti wetu, kama ilivyo katika sehemu zingine za Tanzania, kilimo kwa njia ya ushirika hakikupata kuendelezwa (Sitari, 1983). Mashamba machache yalisafishwa kuuridhisha uongozi, lakini punde yaligawanywa kuwa mashamba ya kibanafsi. Awali kiasi fulani cha kilimo kwa kutumia mashine kilianzishwa, lakini hakikudumu kutokana na uwezo mdogo wa kukarabati mashine zilizotumika.

Kadiri ya McHenry (1976), ujamaa wa Tanzania ulikuwa tofauti na program zingine za kilimo kwa ushirika kwa vile haukuambatana na mabadiliko katika umilikishaji wa ardhi kwa kuwa umiliki binafsi wa ardhi ulikuwa kwa kiwango kidogo. Katika nchi zingine uanzishwaji wa kilimo kwa ushirika ulihusisha kutaifishwa kwa ardhi iliyokuwa chini ya umiliki binafsi. Katika Tanzania ardhi ilikuwa mali ya umma na kwa hiyo watu wote waliweza kuipata kwa urahisi.

Kuanzishwa kwa uzalishaji kwa shirika katika Tanzania ulivishirikisha vyama vya siasa, TANU (Tanganyika African National Union), na serikali, lakini nguvu kubwa ya kiutendaji ilitoka kwenye uongozi wa serikali. McHenry (1976) anaona kuwa kauli za raisi Nyerere huenda zilikuwa na msukumo zaidi katika uanzishwaji wa uzalishaji shirika katika Tanzania kuliko ule wa viongozi wengine mahali pengine popote.

Vijiji vilivyoanzishwa vilitarajiwa kujitawala, lakini McHenry (1976) anaona kuwa viongozi wadogo wa serkali hawakuwaachia madaraka wakulima. Anaona kuwa hii ni sababu kubwa iliyofanya utekelezaji wa ujamaa kutowezekana. Au kama Edwards asemevyo: Kulikuwa na mijadala ya mara kwa mara katka Chama juu ya mfumo ambao ujamaa ulitakiwa kufuata, lakini hatimaye, sehemu kuu ya wenye nguvu ya madaraka hawakutaka utawala kutoka ngazi za chini. Kulikuwa na mijadala ya mara kwa mara ndani ya chama kuhusu muundo wa ujamaa utakaofuatwa, lakini waliokuwa na nguvu hawakuruhusu utawala makini kutoka ngazi za chini (Edwards, David M. 1998:50).

Imetolewa hoja kuwa wakulima wa Afrika huru hawawezi kufikiwa na nguvu ya serikali au nguvu ya soko la kibepari, kwa hiyo mabadiliko ya kitekinolojia na mfumo wa uzalishwaji hayawezi kutokana na nguvu za nje (Hyden 1981). Ni kwa maslahi yao wakulima kudumisha uhuru wao na umiliki wa raslimali ya asili wanayoitumia katika uzalishaji ili kujikimu. Mambo mengine zaidi ya hapo yanaweza kuhatarisha uwezo na fursa zao za kujikimu.

Vipengele vingine vya zoezi la kuanzisha vijiji vya ujamaa, hasa uzuri wa kuishi katika vijiji vikubwa zaidi na uwezekano mkubwa zaidi wa kufikisha huduma za jamii, havikuzingatiwa. Kwa hakika mabadiliko haya katika mpangilio wa vijiji yaliunda vijiji vikubwa zaidi ambavyo vilikuwa ni hatua mbele kuelekea ujenzi wa maisha ya kimji (urbanization). Gould (1970) imeonyesha kuwa mji ni mlango ambao Afrika inautumia kuingia katika ulimwengu wa kisasa.

Imekubalika wakati wa uanzishwaji wa vijiji na hata baadaye kuwa utekekelezaji wa sera ya elimu ya msingi kwa wote na utoaji wa huduma ya afya ni rahisi zaidi iwapo wananchi wanaishi katika makazi yenye ukubwa

zaidi. Mafanikio mazuri yalipatikana katika Nyanja mbalimbali: vijiji zilijengwa kwa kila kijiji na uandikishwaji wa wanafunzi ulikuwa asilimia 100, na huduma za afya ziliongenezaka kwa kiasi kikubwa (e.g. Chachage 2003, Rajani 2003). Hata hivyo mafanikio haya yalizoroteshwa kutokana na kukosekana kwa raslimali ya fedha kwa kuwa malengo ya kiuchumi hayakutekelezwa au kufikiwa.

Maendeleo tangu Uanzishwaji vijiji vya Ujamaa

Katika utafiti huu ninaangalia maendeleo ya makazi katika eneo la magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo tangu kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa. Nilifanya utafiti wangu katika eneo hili kwa mara ya kwanza miaka ya 1975 – 1979, kwa hiyo sasa naangalia hali ilivyo miaka 30 baadaye. Lengo langu ni kuangalia kilichotokea katika mpangilio na muundo wa vijiji, na pia kutafiti juu ya fikra za wenyeji juu ya hali, faida na hasara za kuishi katika vijiji vikubwa zaidi.

Maoni yanayotolewa katika makala hii yanatokana na majibu ya dodoso; mahojiano; majadiliano, maongezi ya hapa na pale; na kuona wakati nilipotembelea eneo la utafiti Octoba hadi Novemba 2008 na Februari hadi Machi 2010. Nilifanya mahojiano na watu binafsi na vikundi pia. Wahojiwa walichaguliwa kutokana na watu niliowapata na kuwahusisha katika utafiti wangu wa awali katika eneo hili miaka ya 1970 na kipindi cha 1989-90. Lengo la utafiti ni kupima kwa kuangalia upeo wa mbali, athari za program ya uanzishwaji wa vijiji. Mjadala juu ya mabadiliko ya mpangilio wa makazi katika vijiji yanatokana uchambuzi wa picha za angani na picha za satelaiti na pia kutazama hali ilivyokuwa nikiwa katika eneo la utafiti.

Pia nilipata fursa ya kutembelea enao la utafiti pamoja na mtafiti mwenzangu mtanzania Dr Ali Sendaro mwaka 1989 hadi mwanzoni mwa 1990, ambapo tulidodosa juu mtazamo wa wanakijiji juu ya maendeleo tangu kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa. Hii ilikuwa ni karibu miaka 15 tokea kufanyika kwa opersheni ya kuanzisha vijiji. Matokeo ya utafiti wa wakati ule yalionyesha kuwa hakukuwa na uendelezaji katika tekinolojia ya kilimo tokea uanzishwaji vijiji vya ujamaa au hata kabla yake (Sendaro 1992). Kwa kuzingatia utafiti huu wa sasa inaonekana wazi kuwa hali haijawa bora zaidi toka wakati huo, na imekuwa kinyume chake (Jambo hili linajadiliwa zaidi na Toni Haapanen katika kitabu hiki). Hata hivyo, ni wazi kuwa hali ya watu ni nzuri zaidi kuliko ya miaka ya 30 au 20 iliyopita. Mahojiano na wakazi, waliohojiwa mwaka 1989-90 yanathibitisha kuwa jamii imepiga hatua mbele katika maendeleo. Matatizo mengi yaliyotajwa katika mahojiano ya awali yametatuliwa. Maeneo makubwa yaliyoendelezwa ni miundombinu; vijiji vingi vinapata maji ya bomba na umeme; na shule za msingi zimepanuka na

kuongezeka; na kuna shule za sekondari kadhaa katika eneo la utafiti. Hata hivyo, katika eneo la huduma za afya hakujawa na uboreshaji mkubwa, na utendaji wake umenung'unikiwa mara nyingi.

Uanzishwaji wa vijiji ulikuwa na malengo mengine zaidi ya kuendeleza uzalishaji wa kilimo kwa njia ya kufanya kazi kwa shirika na utumiaji zaidi wa mashine. Malengo hayo ni: uboreshaji wa miundombinu ya huduma za jamii na urahisishaji wa namna ya kuzifikia. Ni wazi kuwa lengo hili limefanikiwa. Pia kuundwa kwa vijiji vikubwa kumeweka idadi kubwa ya watu ambayo ni msingi wa kufanyika shughuli mbali mbali za uzalishaji. Songqing Jin and Klaus Deininger (2008) wamegundua kuwa shida zinazotokana na uduni wa miundo-mbinu ni kikwazo kwa uanzishwaji, upanuzi na tija wa sekta isiyo ya kilimo vijijijini. Ndiyo maana, uboreshaji wa miundo-mbinu umewasaidia wanavijiji kutawanya shughuli zao za kiuchumi katika sekta mbali mbali na kupunguza utegemezi wao katika kilimo.

Katika utafiti wake juu wanavijiji kuwianisha wao kwa wao kadiri ya umaskini, Bjorn F.H. Van Campenhout (2006) iligundua kuwa dhana pekee ambayo iliyoelekeza nafasi ya kaya katika uwiano na wengine ilikuwa ujuzi wa biashara /miradi. Ujuzi katika biashara / miradi ni muhimu ili kuondokana na umaskini. Minot (2007) haoni utetezi wa kutosha juu ya madai maeneo maskini na ya pembezoni yatabaki nyuma katika maenedleo ya kilimo; pia kuwa kufikika kwa miji na vitovu vya mikoa ni muhimu zaidi katika kupunguza umaskini kuliko umbali kutoka barabara kuu au Dar es Salaam. Kwa maneno mengine, kadiri ya mtazamo wa wanakijiji, mji mkuu si wa msingi katika zaidi katika maendeleo ya kiuchumi kama inavyodhaniwa. Vitovu vya makazi vikubwa zaidi vijijini vinatoa fursa zaidi za kufanyika shughuli za kiuchumi and mapato zaidi.

Zaidi ya haya, uchumi wa familia za vijijini na mijini hauna tofauti kubwa tena. Uchambuzi wa Vali Jamal (2001) unaonyesha kuwa waajiriwa wa mshahara wameamua kuzalisha chakula na kufanya biashara ndogondogo na pia wakulima vijijini wametawanya njia za kujipatia kipato katika miradi na biashara ndogo ndogo. Vishawishi vya kuhamia katika miji havina nguvu, kwa kuwa hata wafanyakazi wa mjini wanalima, na wakulima wanaendesha biashara na miradi mingine kwa mfano ufundi na biashara. Hii ina maana maisha ya vijijini yamekuwa ya ki-mji na maisha ya mjini yanaonyesha hali au tabia (characteristics) za vijijini.

Ni dhahiri kuwa katika kipindi cha miaka 30 idadi ya watu katika eneo la utafiti imeongezeka. Ongezeko la ujumla kutoka sense ya mwaka 1978 hadi ile ya 2002, ambapo ni miaka 24, ni asilimia 65.7. Katika kipindi hicho, ongezeko hilo katika wilaya ya Bagamoyo lilikuwa asilimia 68.3. Kwa hiyo katika eneo la utafiti lilikuwa kidogo kiasi. Viwango vyote hivi viko chini

ya vile vya nchi nzima, ambapo ongezeko ni karibu aslimia 110. Jedwali 1 linaonyesha viwango vya ongezeko la idadi za watu katika eneo la utafiti.

Jedwali 1. Idadi wa Watu katika vijiji kadiri ya sensa za 1978 na 2002.

Kijiji	**Idadi ya watu mwaka 1978**	**Idadi ya watu mwaka 2002**	**Ongezeko %**
Msata	2593	3477	34
Pongwe Msungura	459	879	92
Mazizi	1186	1722	45
Saleni		589	
Lunga	3622	5805	60
Mboga	1922	3232	68
Diozile	1413	2067	46
Kinzagu		652	
Makombe	1240	999*	-20
Mindu Tulieni	318	1706	436
Jumla	**12753**	**21128**	**65,7**

** Population 2006, Makombe village office*

Kati ya vijiji binafsi, vijiji vya Lunga na Mboga ni vya wastani, Lunga ni kidogo zaidi huenda kwa kuwa kutoka 1978 Saleni haikuhesabiwa kama kijiji binafsi ila kama sehemu ya Lunga. Msata inaonyesha ukuaji mdogo, hali inayoonyesha kiwango kikubwa cha uhamaji kwa kuwa hakujawa na mabadiliko ya mipaka ambayo yangekuwa chanzo cha ukuaji mdogo. Kutokukua kwa Makombe sio wa halisi; katika mwaka wa 1978 Kinzagu haikuhesabiwa kama kijiji binafsi na idadi ya watu wake iliunganishwa katika kijiji cha Makombe. Ikihesabiwa hivi, ukuaji wake ni karibu asilimia 33. Ni vigumu kuelewa takwimu za Mindu Tulieni zinaonyesha nini na haziwezi kuthibitisha kiasi cha ukuaji wa idadi ya watu katika kijiji hicho. Inawezekana kijiji cha Makombe, ambacho hakipo katika takwimu za sensa ya mwaka 2002, kimeunganishwa na Mindu Tulieni katika takwimo hizo. Idadi ilionyeshwa kwa ajili ya Makombe katika jedwali hili ni ya mwaka 2006 kama ilivyotolewa na ofisi ya kijiji. Kwa ujumla, haiwezekani kutambua wazi wazi msingi wa tofauti kati ya ukuaji wa idadi ya watu ya vijiji hivi. Hata hivyo, maelezo yanaweza kutolewa kuhusu maendeleo ya kila kijiji binafsi. Kwa mfano Pongwe Msungura, kijiji kilichoko pembezoni, awali hakikutakiwa kuwa kijiji cha ujamaa, lakini idadi ya watu wake imekua mara dufu. Sababu mojawapo inaweza kuwa ni ongezeko la fursa za ajiri katika miradi wa uchimbaji kokoto iliyoko karibu.

Idadi ya vijiji katika wilaya na katika eneo la utafiti imeongezeka. Kijiji chenye vitovu vingi cha Makombe-Kinzagu-Saleni, ambacho kilitaka usajili wakati kuanzishwa vijiji, kimegawanywa katika vijiji vitatu tofauti. Vijiji vyote

hivyo vimefaidika na shughuli za uchimbaji wa kokoto, ambazo hutoa fursa za ajira na kuvipa vijiji mapato.

Watu wote waliohojiwa wanaarifu kuwa watu wachache sana wamerudi kuishi katika vijiji vyao kabla ya kuanzisha vijiji ujamaa. Baadhi ya vijiji vya awali hatimaye vilisajiliwa na kwa hiyo ilikuwa rahisi kurudi huko. Vijiji hivyo hadi sasa vimeongezeka na kupanuka na kuenea katika maeneo ambayo ya watu waliohamishwa kwenda vijiji vipya.

Hivi sasa, kwa kuwa vijiji vimepimwa mipaka, kijiji ni eneo lililoainishwa na ni zaidi ya makazi tu. Kwa maneno mengine hakuna eneo la kuhamia, ambapo mtu hatatambuliwa kuwa mwanakijiji wa kijiji fulani. Kadiri ya mahojino kuna hali ya kutambua uhusiano kati ya wanakijiji bila kujali kama wanaishi katikati ya kijiji au mahali pengine ndani ya eneo la kijiji. Watu wanweza kuhamia nje ya kitovu cha kijiji lakini wanaendelea kuwa wanakijiji na wanashiriki katika shughuli za kijiji. Kutokana na kupima na kuweka wazi mipaka ya vijiji, takwimu za watu katika ngazi ya kijiji zimekuwa sahihi zaidi na takwimu za sensa sasa zinaweza kulinganishwa kwa usahihi zaidi kuliko zile za awali, na kwa hiyo picha halisi ya maendeleo yanayohusu idadi ya watu inaweza kupatikana.

Watu waliohama kutoka sehemu wakati wa kuanzisha vijiji, ambazo sasa ziko ndani ya vijiji vilivyopimwa na kusajiliwa wameweza kudai na kumilika mashamba yao ya zamani; lakini watu waliohama kutoka sehemu za pembezoni, ambazo sasa zinahesabika katika vijiji vingine, mara nyingi wamepoteza mashamba yao ya awali. Hali iliarifiwa na watu waliohama kutoka eneo la Mkoko na Pongwe kwenda Msata. Mashamba yao yamechukuliwa na wengine au wako mbali mno kiasi cha kutoweza kulima mashamba hayo. Hifadhi ya Misitu ya Wami-Mbiki pia imechukua baadhi ya mashamba.

Baadhi ya watu waliohama kutoka sehemu za mbali, hadi leo, baada ya miaka 30, hawana mashamba yao bali wanalima mashamba ya kukodi au kuazima. Wanadai kuwa hakuna ardhi ya kutosha katika kijiji, kulikuwa nafasi zaidi katika makazi yao ya zamani. Hata hivyo, wasingependa kurejea kwenye maeneo ya makazi ya zamani, kwa kuwa wanaona umuhimu zaidi wa huduma wanazopata kijijini. Pia kuna usalama zaidi katika kijiji kikubwa na yeyote anaweza kupata msaada anapohitaji. Wahojiwa pia walionyesha fursa walizonazo watoto kwa njia ya kusoma shule na kusema kuwa 'maisha ya watoto wetu (na wajukuu) yatakuwa tofauti'. Ni wazi kuwa huduma inayotambulika zaidi ni elimu. Kwa bahati mbaya wanavijiji wengi hawawezi kuwapa elimu ya sekondari watoto wao wote wanaofaulu mitihani na kustahili kwenda shule.

Mpangilio wa Kijiji

Watu walipohamia katika vijiji, kila kaya ilipewa eka moja kwa ajili ya ujenzi wa makazi na kulima bustani za mboga na matunda. Matumizi ya vipande hivi vya ardhi kwa ajili ya kilimo umepungua au kupotea kabisa. Badala yake zimejengwa nyumba kwa ajili ya wanafamilia na kufanya mkusanyiko wa makazi ya kifamilia ndani ya kijiji. Hii ina maana mikusanyiko ya makazi kwa msingi wa familia au ukoo umejirudia na unaonyesha nguvu na uimara wa mshikamano wa familia. Wahojiwa wanayaita maeneo waliyopewa wakati wa kuamzishwa vijiji kuwa ni sehemu za kujenga makazi ya familia sio tena mashamba.

Wakati wa kuanzishwa vijiji, mfumo wa gridi wa barabara zilizonyooka na maeneo ya mstatiri yaliyogawanywa katika ploti za eka moja ulianzishwa na kuwa muundo rasmi wa mpangilio wa makazi ya vijiji. Katika mfumo wa kiasili nyumba zilikuwa karibu karibu na kufanya mkusanyiko au kuizunguka sehemu ya katika iliyowazi. Njia za miguu zilitoka nyumba hadi nyumba. Mfumo huu wa zamani wa njia za miguu umejirudia na mfumo wa gridi za mstatili umepotea. Maendeleo ya kijiji cha Makombe ni mfano mzuri wa badiliko hili.

Kukua kwa hali ya Kimji

Kama ilivyoelezwa awali, kuanzishwa kwa vijiji kunaweza kutazamwa kuwa ni hatua kuelekea hali kimji katika maeneo ya vijijini. Katika eneo la utafiti, hali ya kimji imejitokeza zaidi katika kijiji cha Lunga ambapo katika sensa ya 2002 eneo hilo limetajwa kuwa ni la kimji. Kati ya wakazi 5805 wa Lunga, 2731 walitajwa kuwa wa kijijini na 3074 kuwa wa mjini. Hii ina maana Lunga ilikuwa ni makazi ya kimji kwa asilia 53. Kwa kuangalia na kuona, vijiji vingine vilivyoko pembezoni mwa barabara, hasa Msata na Mboga, zina mazingira ya kimji ingawa havitajwa kuwa ni miji na umuhimu wa kilimo kwa ajili ya kujikimu umepungua. Kikula (1997) anapendekeza kuwa mpangilio mpya wa makazi ya vijiji vikubwa unaweza kurahisisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Zaidi ya wafanyao biashara na mafundi wa kudumu, wakulima wengi wanafanya kazi za biashara na ufundi kama ziada juu ya kilimo. Kwa njia ya kuona, majadiliano na mahojiano wakati wa utafiti huu imethibishwa kuwa hali iko hivyo na fursa za kufanya miradi ni sababu mojawapo inayowafanya watu wasifikirie kuhamia maeneo ya pembezoni hata kama zitakuwa na fursa zaidi za kilimo.

Nilifuatilia baadhi ya watu niliowahoji mwaka 1989 katika vijiji vya Lunga, Mboga and Msata. Baadhi ya vipengele vilivyojadiliwa ilikuwa

shughuli na makazi ya waliokuwa watoto wa waliohojiwa wakati ule. Taarifa zilipatikana za watoto 126 , ambao sasa ni watu wazima. Taarifa zilionyesha kuwa asilimia 50 ya watoto walioishi Lunga, Mboga and Msata mwaka 1989 wameendelea kuishi pale. Wengi wa waliohama walienda kuishi Dar es Salaam, ingawa wachache wanaishi sehemu zingine, wengi wao Chalinze (Jedwali 2). Tukiondoa waliokufa, wanaoishi katika vijiji vyao vile vile ni zaidi ya asilimia 60.

Jedwali 2. Sehemu wanayoishi watoto wa wahojiwa katika mahojiano ya mwaka 1989.

	Lunga	**Mboga**	**Msata**	**Total**	**%**
Amekufa	4	9	6	19	15
Kijiji kile kile	25	22	19	66	52
Dar es Salaam	4	14	5	23	18
Mahali pengine	9	3	5	17	13
Haijulikani	1			1	1
Jumla	**43**	**48**	**35**	**126**	100

Watoto wa watu waliohojiwa mwaka 1989 sasa wana shughuli mbali mbali. Sehemu kubwa wanashughuli na miradi binafsi na ufundi (29 %). Asilimia 11 tu ni wakulima na karibu asilimia 10 ni madereva na wafanyakazi za ujenzi, na asilimia sita ni wanajeshi na watumishi wa serikali. Asilimia 26 walitajwa kuwa ni mama wa nyumbani (housewife). Ingawa dodoso hili hailikuwa kubwa, matokeo yako wazi kuwa vijana wa kileo hawavutiwi na kilimo kuwa shughuli ya kujikimu kimaisha.

Faida na Hasara za Kijamii

Kuishi pamoja kama jamii kumeleta manufaa kwa kuwa watu wamejifunza kufahamiana, na hii imeongeza hali ya kuaminiana. Mhojiwa mmoja alisema: “tunafahamiana vizuri zaidi, kwa hiyo tunaweza kufanya kazi pamoja”. Tunaweza kujiuliza kama uzalishaji kwa ushirika It could be asked, if the collective activities wakati wa vijiji vya ujamaa kwa kiasi Fulani ulishindikana kwa sababu ya kutoaminiana kati ya watu waliohamishwa kwa pamoja lakini hawakufahamiana vema. Katika vijiji vya kiasili ambavyo ni msingi wa muundo wa ujamaa watu walifahamiana vema.

Usalama unaonekana kuwa ni faida kubwa kutokana na watu kuishi pamoja katika kijiji kikubwa. “Iwapo mtu anapata tatizo anaweza kupata msaada” inatajwa kuwa sababu ya vijiji vikubwa kuwa mahali pazuri zaidi pa kuishi kuliko makazi madogo, na sababu ya watu kutorudi kwenye makazi ya awali kabla ya ujamaa. Ikichunguza zaidi jambo hili linahusu huduma

za afya. Pia matarajio ya watoto siku zijazo yanaonekana kuwa bora katika vijiji vikubwa. Wazazi wanaweza kusema kuwa walipata na bado wana shida kutokana na kuhamishwa, lakini walikiri kuwa "watoto wetu watakuwa na maisha tofauti". Baadhi yao wanaume kwa wanwake walionyesha kuwa wake na waume katika vijiji vikubwa wanashiriki kutekeleza majukumu kwa usawa zaidi kuliko enzi za zamani katika makazi ya awali. Hii inaweza kutokana na kukua kwa mazingira ya maisha ya kimji katika vijiji vikubwa na mabadiliko kwa ujumla kuelekea usawa kati ya wanaume na wanawake.

Fursa za kiuchumi zinazotokana na ukubwa wa vijiji ni faida ya wazi. Kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa zaidi wa miradi, watu wamepunguza utegemezi katika kilimo na hii inaongeza usalama wao. Hata hivyo, kwa upande mwingine watu wanonyesha kuwa "hakuna nafasi ya kutosha kwa ajili ya kilimo". Hasa wale waliohamishwa toka mbali na kwa hiyo wamepoteza mashamba yao ya awali hawawezi kulima kwa kiasi kikubwa kama wanavyotaka. Kukosekana kwa nafasi ya kilimo ni kikwazo kikubwa kwa wahamiaji wa wakati wa ujenzi wa vijiji vya ujamaa, hata hivyo hawako tayari kurudi katika makazi ya zamani kwa kuwa faida ya vijiji vikubwa inazidi faida za kurudi makazi ya zamani.

Kitu ambacho hakijafanikiwa ni uboreshaji wa kilimo. Ni wazi kuwa katika miaka hii 30 hakukuwa na maendeleo yoyote katika kilimo, na pengine kilimo kimezorota.

Hitimisho

Mpangilio wa makazi ulioundwa wakati wa uanzishwaji wa vijiji vya ujamaa umekuwa wa kudumu. Kumekuwa na mabadiliko kiasi, vijiji zaidi vimeandikishwa na baadhi ya wanavijiji wamerudi katika makazi ya zamani, hata hivyo hakukuwa na kutawanyika kwa makazi mapya.

Mipaka ya vijiji hivi sasa imepimwa na dhana ya kijiji inaanza kuelezea eneo zaidi ya makazi. Upimaji wa ardhi na utengenezaji wa ramani za kijiji unaimarisha zaidi dhana hii ya kijiji.

Vijiji vimekua na vingine vimeenea katika maeneo ambayo awali watu walihamishwa kuja vijijini. Lakini sehemu kubwa ya kukua kwa vijiji imefanyika ndani ya vijiji. Ploti za eka moja walizogagwiwa wahamiaji zimetumika kujenga nyumba za familia na sehemu za wazi zimeganywa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Hakuna nafasi ndani ya vijiji vikubwa kwa ajili ya kulima isipokuwa baadhi ya matunda. Mpangilio wa makazi wa kufuata gridi ya mstatili umedhoofishwa na mpangilio wa kiasili umepata nguvu zaidi.

Watu wanathamini zaidi maendeleo ya miundo mbinu ya huduma za kijamii, hasa miundombinu na zana za elimu. Miundo mbinu na zana

za afya havijaendelezwa kama elimu, na utendaji kazi wake ni hafifu. Awali huduma ya maji ilikuwa ni tatizo la kwanza lakini kutokana na mradi wa maji ya bomba uliopo, hali ya upatikanaji wa maji inaridhisha katika vijiji vyote vinavyopata huduma hii.

Watu wanatambua kuwa hali yao ni bora kuliko wakati wa kuanzishwa vijiji vya ujamaa. Kilimo hakijaendelezwa, bali kimezorota hasa uzalishaji wa mazao ya biashara. Hali bora ya maisha inatokana na uboreshaji wa huduma na miundo mbinu na kuongezeka kwa fursa za kipato kutokana na shughuli zisizokuwa za kilimo.

Machapisho

Chachage, Chachage S. L. (2003). Keynote address. Why is Tanzania still poor forty years after independence? In Yahya-Othman, Saida & Martha A. S. Qorro & Benjamin Mtinangi & Jenerali T. Ulimwengu (eds.) Why is Tanzania still poor 40 years after independence? Proceedings of the 6th UDSM Convocation Symposium 2003. pp. 1 – 29.

Edwards, David M. (1998) Matetereka: Tanzania's last ujamaa village. Occasional papers No 77, Centre of African ersity.Studies, Edinburgh University.

Gould, P. R. (1970) Tanzania 1920 – 63: The Spatial Impress of the Modernization Process. World Politics 22, no 2 (January 1970), pp 149-70. Princeton University Press.

Hyden, Göran (1982). Beyond ujamaa in Tanzania. Underdevelopment and an uncaptured peasantry. 262 p. Heinemann, Nairobi. (Reprinted, first published in 1980)

Jamal, Vali (2001) Chasing the Elusive Rural-Urban Gap in Tanzania. Journal of Contemporary African Studies, 19,1,2001,

Kikula, Idris S. (1997 Policy implications on environment. The case of villagisation in Tanzania. DUP (1996)LTD. Dar es Salaam. 237 p.

McHenry, Dean E. (1976) The Ujamaa Village in Tanzania: A Comparison with Chinese, Soviet an d Mexican Experiences in Collectivization.

Comparative Studies in Society and History, Vol 18, No. 3. pp 347-370. Cambridge University Press.

Minot, Nichlas (2006) Are Poor, Remote Areas Left behind in Agricultural Development: The Case of Tanzania. Journal of African Economies, Volume 17, Number2, pp 239-276.

Ponte, S (2002) Farmers & markets in Tanzania. How policy reforms affect rural livelihoods in Africa. Heinemann, Portsmouth.(1992)

Rajani, Rakesh (2003). Is primary education heading in the right direction? Thinking with Nyerere. In Yahya-Othman, Saida & Martha A. S. Qorro & Benjamin Mtinangi & Jenerali T. Ulimwengu (eds.) Why is Tanzania still poor 40 years after independence? Proceedings of the 6th UDSM Convocation Symposium 2003. pp. 55 – 65.

Rudengren, Jan (1981). Peasants by preference? Socio-economic and environmental aspects of rural development in Tanzania. 234 p. Scandinavian Institute of African Studies & The Economic Research Institute, Stockholm.

Sendaro, Ali (1992) Technical stagnation, aging population and agricultural production in Tanzania: The case of Lugoba, msata and Mboga villages in Bagamoyo District. In Forster, Peter G. & Sam Maghimbi (Eds) (1992) The Tanzanian Peasantry: Economy in Crisis. Avebury, Aldershot. pp.151-168.

Schneider, Leander (2007) High on Modernity? Explaining the Failings of Tanzanian Villagisation. African Studies, 66, 1 pp. 9 – 38, April 2007.

Songqing Jin & Klaus Deininger (2008) Key Constraints for Rural Non-Farm Activity in Tanzania: Combining Investment Climate and Household Surveys. Journal of African Economies, Volume 18, Number 2, pp. 319-361.

Van Campenhout, Bjorn F. H. (2006) Locally Adapted Poverty Indicators Derived from Participatory Wealth Rankings: A Case of Four Villages in Rural Tanzania. Journal of African Economies, Volume 16, Number 3, pp. 406 – 438.

ONGEZEKO LA WATU NA ATHARI ZAKE KATIKA MISITU MAGHARIBI MWA BAGAMOYO, TANZANIA

Emmanuel Mhache, Idara ya Jiografia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Utangulizi

Utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa Pwani, wilaya ya Bagamoyo. Kata mbili zilichaguliwa katika utafiti huu ambazo ni Lugoba na Msata. Katika kata hizi mbili vijiji saba vilitafitiwa kwa kina. Kata ya Lugoba, vijiji vya utafiti vilikuwa ni Lunga, Msoga, Mboga, Saleni na kijiji cha Mindu-Tulieni. Msata vijiji viwili vilitafitiwa, ambavyo ni Msata na Pongwe-Msungura.

Utafiti huu ni sehemu ya utafiti mkubwa ujulikanao kama, Maendeleo ya Makazi Vijijini, Umiliki wa Ardhi na Uhakika wa Chakula toka enzi za Ujamaa, Mashariki mwa Tanzania. Utafiti huu uliaangalia ongezeko la watu na adhari zake katika misitu ya Bagamoyo toka wakati wa Ujamaa na Operesheni Pwani hadi sasa, wakati tulionao. Ni wazi kuwa ongezeko la watu kama haliendi sambamba na ukuaji wa teknolojia na maendeleo huwa na adhari hasi katika rasilimali kama ardhi na misitu. Misitu katika eneo la utafiti imeasthiriwa sana na ongezeko la watu kwani misitu ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu hapa duniani kwa ujumla na kwa mtu binafsi (Mhache, 2005:05). Misitu imekuwa ni mhimili mkuu wa maisha ya watu mijini na vijijini.

Malengo ya utafiti

- Kutafiti matumizi ya mazao ya misitu na umuhimu wake katika maisha ya binadamu ya siku.
- Kutafiti adhari za ukuaji wa miji katika misitu.
- Kelezea na kuonyesha mabadiko ya misitu kwa kulinganisha ramani za miaka ya 1966, 1982 na 2007.
- Kutathimini mawazo ya watu katika misitu na umuhimu wake katika

maisha ya binadamu.
- Utatuzi na njia za kutatua tatizo la uharibifu wa misitu

Maswali yaliyoongoza utafiti huu

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- Zipi ni ni faida/matumizi ya mazao ya misitu na umuhimu wake katika maisha ya kila siku ya binadamu?
- Ni adhari zipi zitokanazo na ukuaji wa miji na ongezeko la watu katika misitu?
- Je ni mabadiliko gani yametokea katika misitu kwa kulinganisha ramani za miaka ya 1966, 1982 na 2007?
- Watu wana mawazo gani kuhusiana na misitu?
- Ni njia gani zinaweza kutumika kutatua tatizo la uharibifu wa misitu?

Utafiti huu ulionyesha kuwa ongezeko la watu limekuwa na adhari kubwa katika misitu ya wilaya ya Bagamoyo na nchi nzima kwa ujumla. Mchungaji Thomas Malthus (1798), mtafiti wa masuala ya idadi ya watu, aliandika kuhusiana na kanuni za ongezeko au idadi ya watu. Alikiri kuwa ongezeko la idadi ya watu inamaana matumizi ya rasilimali nayo yanaongezeka, kwa mfano chakula kitatumika kwa wingi na ardhi kubwa itahitajika ili kukidhi mahitaji ya binadamu. Mwisho ongezeko la watu litafikia kikomo, kiwango ambacho rasilimali zilizopo zitashindwa kukidhi mahitaji ya ongezeko la watu litakayokuwepo kwa wakati huo. Matokeo yake ni kutokea kwa magonjwa ya milipuko, njaa na vita, mwisho wake ni watu kufa, idadi ya binadamu kupungua na kufikia idadi ambayo rasilimali zilizopo zitaweza kukidhi mahiataji ya idadi ya watu itakayokuwepo kwa wakati huo.

Kanuni ya Mchungaji Thomas Malthus (1798) zilipingwa na watafiti waliofuata kama Boserup (1965), Tiffen na wenzake (1994) waliokiri kuwa ongezeko la watu lina faida na ni muhimu sana kwani hutoa changamoto kwa jamii kufanya ugunduzi na kugundua technologia zitakayowezesha watu kuzalisha mazao na chakula kwa wingi. Pia watu watalazimika kutumia mbolea za kisasa, kulima kwa kutumia matrekta na majembe ya kukokotwa na wanyama au maksai. Kama lengo litakuwa ni kufuga na kulima eneo dogo kwa kutumia wataalamu na utaalamu wa kisasa mavuno yatakuwa mengi na hapatakuwa na maana ya kuongeza ukubwa wa mashamba kila siku au msimu. Hili la kukuwa kwa utaalamu halijawezekana kwa kata za Lugoba na Msata, kwani watu bado wanatumia kilimo cha kizamani, kilimo cha kuhama hama na kilimo cha jembe la mkono. Kilimo cha kuhama hama kina adhari kubwa

sana katika misitu. Kwani maeneo mapya hufunguliwa kwa ajili ya kilimo, ufugaji, makazi mapya na uchimbaji mawe/kokoto. Shughuli zote hizi huhitaji kufyeka misitu na kufanya misitu kutoweka (Mhache, 2007).

Methodolojia ya utafiti huu

Taarifa zilikusanywa kwa njia ya mahojiano katika vijiji sita (Jedwali 1). Kaya ilitumika kama kigezo cha kupata taarifa katika utafiti huu na wahojiwa walikuwa ni wakuu wa kaya. Wakuu wa kaya wapatao 285 walihojiwa, wanaume wakiwa 201 and wanawake 84. Wahojiwa walipatikana kwa msaada wa viongozi wa vijiji na vitongoji. Katika mchakato mzima wa kupata taarifa husika watafiti walifanya mahojiano na viongozi wa serikali za vijiji, watendaji, mabwana shamba, maafisa misitu, na wajumbe wa kamati za mazingira kwa kila kijiji. Lengo lilikuwa ni kupata taarifa kuhusu ongezeko la watu na athari zake katika misitu, ardhi na rasilimali mbalimbali. Taarifa nyingine zilizokusanywa ni kuhusiana na kilimo, ufugaji, makazi ya watu, biashara na kadhalika. Taarifa hii inatoa muhitasari wa utafiti uhusuo ongezeko la watu na adhari zake katika misitu.

Jedwali 1. Idadi ya watu waliohojiwa na vijiji vilivyohusishwa katika utafiti huu

Vijiji vilivyotafitiwa	Idadi ya wahojiwa	Asilimia ya wahojiwa
Lunga	66	23.2
Msoga	34	11.9
Mboga	36	12.6
Saleni	37	12.9
Mindu Tulieni	28	9.8
Msata	45	15.8
Pongwe Msungura	39	13.7
Jumla	**285**	**100**

Yaliyojitokeza katika vijijini vya utafiti

Kilimo ni chanzo muhimu sana cha kujipatia riziki kwa wananchi wa kata za Lugoba na Msata (Kielelezo 1). Wananchi wengi waliohojiwa asilimia 97.2 wanategemea kilimo wakati asilimia 52.6 wanategemea ufugaji ili kujikimu kimaisha. Kilimo ndio shughuli inayotegemewa na wananchi wote katika vijiji viliyofanyiwa utafiti. Asilimia 97.2 ya wahojiwa wote walikiri kuwa kilimo ndio shughuli inayowapatia chakula na kipato. Asilimia 32.3 na 31.6 wanategemea biashara ndogondogo na mkaa kwa mfuatano kukidhi mahitaji ya maisha yao. Biashara ya mkaa inakuwa na imekuwa ikifanyika kwa muda mrefu sasa kutokana na wanachi kutokuwa na mazao ya biashara ya kudumu

kwani mazao ya pamba na simsim yaliyokuwa yanalimwa yalikosa soko la uhakika, wananchi wakaamua kuyaacha mazao hayo. Wananchi wengine bado wana marobota ya pamba ndani mwao kwa kukosa soko. Wananchi wengine asilimia 10.5 wameajiriwa wakati asilimia 7.4 wanategemea shughuli ya kuchoma tofali. Asilimia 14.4 wanategema shughuli mbalimbali kwa fundi nguo, kutengeneza baiskeli, baba na mamalishe. Lengo la shughuli hizi ni kuwapatia wananchi fedha kwa ajili ya kununua chakuka na kukidhi matumizi mbalimbali kama kulipia matibabu, kulipa ada za watoto na ujenzi.



Kielelezo 1. Njia mbalimbali za kujipatia riziki kwa wananchi 285 waliohojiwa kwa asilimia.

Faida zitokanazo na misitu

Wananchi waliohojiwa asilimia 99 walikiri kuwa misitu ina faida kubwa kwao toka zama za mababu zao (Kielelezo 2). Faida zitokanazo na misitu kama ilivyoainishwa na wahojiwa ni kipato, upatikanaji wa miti ya ujenzi, kuni, dawa asili, chakula na matunda.

Kipato: Lengo kuu la wananchi kushiriki katika suala la uvunaji wa mazao ya misitu ni kupata fedha kwa ajili ya kutatua matatizo ya kifamilia. Asilimia 1.5 ya wahojiwa 285 walikiri kuwa misitu huwapatia fedha kwa kuuza mazao ya misitu.

Upatikanaji wa miti ya ujenzi: Faida mojawapo ya misitu ni kupata miti au mijengo kwa ajili ya ujenzi kama ilivyoainishwa na asilimia 10.6 ya wahojiwa wote. Kila mtu aliyehojiwa katika utafiti huu alikiri kutumia miti katika ujenzi wa nyumba. Hata kama ni nyumba ya tofali miti ilitumika katika

milango, madirisha na wakati wa kupaua. Kila mtu aliyehojiwa alifaidika na mazao ya misitu kwa njia moja au nyingine.

Kuni na mkaa: Kuni ni nyenzo muhimu sana katika maisha ya watu wa Msata na Lugoba. Asilimia 100 ya wahojiwa walikiri kutumia kuni kama nishati kuu katika kupika. Tofauti na kuni hakuna nyenzo nyingine itumikayo kupika. Kuni hutumika kwa wingi kwani hupatikana bure kwenye misitu na katika mazingira wanayoishi wananchi. Mkaa hutengenezwa na wananchi kwa ajili ya kuuza, ni mara chache sana mkaa kutumika. Mkaa hutumiwa kwa ajili ya kunyooshea nguo na mara chache hutumika kupika hasa wakati wa mvua, kwani wakati wa mvua kuni hupatikana kwa shida sana. Asilimia 70 ya wahojiwa wote walikiri kuwa mkaa hutengenezwa kwa ajili ya kuuza na wakati mwingine hutumika kwenye mahoteli, kukaanga chips, mayai na mama lishe au baba lishe hutumia mkaa.



Kielelezo 2 Faida za misitu kulingana na wananchi waliohojiwa

Madawa asili: Vijiji vya Pongwe-Msungura na Mindu-Tulieni ni mojawapo ya vijiji vilivyo mbali na vituo vya huduma za afya. Vijiji hivi hutegemea huduma za afya kutoka vijiji vingine kama Msata na Lugoba ambavyo vipo umbali wa kilomita nne hadi tano. Umbali huu ni kikwazo kikubwa kwa familia nyingi ambazo hulazimika kutumia miti-shamba au madawa asili kujitibu wakati wapatapo ugonjwa wowote na hata wakati wa kujifungua. Asilimia 8.8 ya wahojiwa wote waliafiki kuwa misitu ni muhimu kwao kwani huwapatia madawa ya asili. Miti iliyotajwa kama dawa ni Mkundekunde, Mfuleta, Mkenge, Mkwambe, Mlama, Mpingo, Msaraka, Msisimizi, na Msosowama.

Chakula na matunda: Bila chakula hakuna maisha. Misitu ni chanzo

muhimu cha kuwapatia wananchi chakula. Asilimia 35 ya wahojiwa wote walikiri kuwa misitu huwapatia chakula na matunda (Kielelezo 2). Mfano Msingizi, Msofu, Msemberere, Mkole, Msada, Mtopetope na Mkwaju. Misitu hutoa faida mbalimbali ikiwemo chakula na matunda. Familia nyingi zilizohojiwa zilikiri kupata matunda na chakula kutoka misituni. Faida hii imepungua sana ukilinganisha na miaka ya 70 na 80. Matunda ya misituni ni mkombozi wakati wa kiangazi pia wakati ambao mavuno ya kilimo ni madogo.

Mbao: Asilimia 10.6 ya wahojiwa 285 walikiri kuwa misitu ni chanzo muhimu sana kwa mbao. Umuhimu huu umepungua kutokana na utengenezaji wa mkaa na kutokuwa na mkakati mahsusi wa upandaji miti. Miti itumikayo kwa mbao ni Mninga na Mkongo.

Faida nyinginezo za misitu: Wananchi wengine asilmia 13 waliohojiwa walitaja faida nyingine za misitu kuwa ni asali, kamba za kusuka ukindu, maji, malisho ya mifugo na maji. Faida zote hizi hupatikana bila mtu kulipa gharama yoyote.

Visababishi vikuu vya uharibifu na kutoweka kwa misitu

Utafiti huu umeonyesha kuwa kuna sababu nyingi zilizochangia uharibifu na kutoweka kwa misitu katika wilaya ya Bagamoyo. Sababu zifuatazo ziliainishwa na wananchi waliohojiwa.

Mkaa: Uchomaji mkaa ulitajwa kuwa ni njia kuu katika kutoweka kwa misitu katika kata za Lugoba na Msata. Kiasi cha asilimia 24 ya wahojiwa waliafikiana kuwa mkaa huhitaji miti mingi ili kupata mkaa wa kutasha. Katika kufanya hivyo eneo kubwa hukatwa miti kwa ajili ya kutengeneza mkaa kwa muda mfupi. Biashara ya mkaa imeanza kwa kasi katika wilaya Bagamoyo mwishoni mwa miaka ya 70 na miaka ya 80 kutokana na serikali kuacha kutoa ruzuku kwenye mbolea na mbegu. Wananchi wali wengi walishindwa kuendeleza kilimo cha kisasa na kuamua kujiingiza kwenye shuguli ya kutengeneza mkaa.

Mijengo: Asilimia 70 ya nyumba zote zilizoko katika kata za Lugoba na Msata ni za miti na udongo. Asilimia thelasini ni nyumba za tofali ambazo pia zimetumia mijengo au miti katika kupaua. Asilimia 22 ya watu waliohojiwa hukata miti ya ujenzi/mijengo kutoka maporini. Ukataji wa miti pasipo kupanda hufanya eneo kuwa jangwa.

Adhari za moto: Kaya mbalimbali zilikiri kusafisha mashamba yao kwa kutumia moto. Moto husaidia kufukuza wanyama hatari kama vile nyoka. Kusafisha mashamba kwa mtindo wa kutumia moto ulitajwa na asilimia 20 ya wahojiwa wote. Mtindo wa kutumia moto ulitafsiriwa na viongozi wa kamati

za mazingira kuwa ni hatari kwa misitu kwani huua miti na miti iliyohimili kubaki huchukua muda mrefu kuchipua na kurudi kwenye hali yake ya mwanzo.

Mbao: Ukataji miti kwa ajili ya kupata mbao ni njia mojawapo inayochangia kutoweka kwa misitu. Miti kwa ajili ya mbao ni ngumu kupatikana katika kata za Lugoba na Msata. Asilimia 19 ya wakuu wa kaya waliohojiwa walikiri kuwa ukataji wa miti kwa ajili ya mbao umechangia kwa kiasi kikubwa miti kutoweka katika eneo hili. Mbao hutumika kutengeneza vitu vya thamani kama meza, kabati, vigoda, milango, madirisha, vitanda na vitu vingine.

Malisho: Makabila ya Wamasai na Wakwere hujishughulisha na ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Ulishaji wa wanyama hawa maporini huchangia kuleta jangwa na kutoweka kwa misitu. Kwani wanyama hula vichipukizi vya miti na hatimaye miti hufa.

Asilimia 10 ya wananchi waliohojiwa walikiri kuwa kuna njia nyinginezo zisababishazo misitu kutoweka kama kukata miti kwa ajili ya kuni, kukata miti kwa ajili ya dawa, kuchimba mawe misituni na pia ujenzi wa nyumba misituni.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na mtumizi ya misitu

Idadi kubwa ya wakuu wa kaya waliohojiwa walikiri kuwa misitu haikuwapa faida sana. Kwani kutokana na misitu wamefadika kwa kupata kuni, mbao na miti ya kujengea. Wapo waliokiri kuwa wameweza kujenga nyumba za udongo na wapo waliokiri wamejenga nyumba za tofali. Wengine pia walikiri kutokana na kuuza mazao ya misitu wameweza kuwasomesha watoto wao kwa kuwalipia ada, kuwanununulia sare za shule na pia kuihudumia familia kwa matibabu na chakula pia (Mhache, 2004).

Matokeo ya utafiti

Kwa ujumla eneo la misitu lilipungua sana kutokana na matumizi ya binadamu. Hii imetokana na ongezeko la watu, uhitaji wa eneo la makazi na maeneo ya kilimo. Mwaka 1966 eneo la misitu lilikuwa ni hekta 608, wakati mwaka 1982 liikuwa ni hekta 575. Eneo la misitu lilipungua kwa hekta 33. Ramani ya mwaka 2007 inaonyesha kuwa eneo la misitu liliendelea kupungua zaidi na kufikia hekta 252.

Njia za kupunguza uharibifu wa misitu

Upandaji miti

Suala la upandaji miti katika vijiji vingi halijapewa msisitizo wa kutosha. Kwani vijijini hakuna bustani za miche ya miti. Bustani za miche ya miti zilizopo ni chache sana ambazo hazikidhi mahitaji ya wananchi. Shule ya Msingi Msoga ni moja ya shule iliyokuwa na bustani ya miti. Hata hivyo bustani hiyo ilionekana kuwa ni ndogo. Wananchi binafsi waliokuwa wakijishughulisha na bustani za miche ya miti wakati wa utafiti huu mwaka 2008-2010 ni wachache sana. Iwapo wananchi watapanda miti kwa ajili ya kuni, mkaa na mbao uharibifu wa misitu utapungua kwa kiasi kikubwa.

Mashamba darasa ya miti

Hakuna mashamba darasa au mashamba ya mifano ya miti katika vijiji vingi. Mashamba haya ni muhimu sana kwani wananchi wataweza kuigiliza yanayofanyika kwenye mashamba darasa ya miti na kupanda miti kwenye mashamba yao binafsi. Mashamba haya yakitumika vema kuwafundishia wananchi kwa vitendo, wananchi wataweza kuutumia utaalamu huo kwenye mashamba yao na kuachana na utamaduni wa kutegemea misitu asili kwa ajili ya kuni, mkaa na mbao.

Hati miliki za misitu

Kuna haja ya misitu ya vijiji kupimwa na kuwa na mawe yanayoonyesha mipaka ya misitu hiyo. Umiliki wa ardhi bado ni tatizo, kwani wananchi walio wengi wanaona misitu kama ni rasilimali huru, ambayo mtu yeyote anaweza kuitumia atakavyo. Pakiwepo na umiliki wa misitu na wananchi wakaelimishwa na kuelewa kuwa misitu ni yao na si vinginevyo, misitu itatunzwa na kurudi kwenye hali yake ya zamani.

Umiliki wa ardhi

Pawepo na utaratibu wa kumilikisha wananchi ardhi. Kila kijiji kiwe na masjala ya ardhi ili kupunguza wananchi kusafiri umbali mrefu kufuatlia hati ya ardhi. Wananchi wawe na hati ya ardhi ili iwe rahisi kuitumia kupata mikopo na kuitumia katika kuboresha njia zao za kujikimu. Mikopo itapunguza wananchi kushiriki katika shughuli zinazoharibu mazingira na misita kama kuchoma mkaa na kuanzisha shughuli nyingine kama biashara ndogondogo.

Uelewa mdogo kuhusiana na misitu

Utafiti huu ulionyesha kuwa wananchi wengi hawana uelewa kuhusiana na adhari za ukataji miti ovyo. Kwani walio wengi wanafikiria faida waipatayo sasa bila kufikiria adhari zake kwa kizazi kijacho.

Njia finyu za kujikimu

Hili ni tatizo kubwa sana. Wananchi waliohojiwa asilimia 97 wanategemea kilimo na mazao ya misitu. Kwa ujumla kilimo hakikidhi mahitaji ya wananchi walio wengi. Hili huwalazimiwananchi huchoma mkaa kwa ajili ya kupata fedha.

Sheria ndogo za vijiji

Iwapo sheria ndogo za vijiji zitatumika kama ilivyo kwenye maandishi tatizo la uharibifu wa misitu litapungua kwa kiasi kikubwa. Ikiwa aliyeharibu misitu ni ndugu wa kiongozi au mfuatilia wa sheria hizo inakuwa ni ngumu kumlipisha faini au kumpeleka mahakamani. Sheria za kijiji cha Mboga zinasema mtu yeyote atakayepatikana na kosa lihusulo misitu au vyanzo vya maji atatakiwa tulipa faini isiyozidi shilingi 50,000/=. Utekelezaji wa sheria hii ni ngumu, kwa mfano, ikiwa mtuhumiwa ni mtoto, mke au mume wa msimamizi wa sheria hizi. Je itakuwaje? Hili nalo linachangia katika uharibifu wa misitu.

Ulinzi wa misitu (Patroo)

Pawepo na ulinzi wa rasilimali za vijiji kama ulinzi wa misitu na vyanzo vya maji. Wananchi wanajua kwamba kukata miti misituni kwa ajili ya shughuli zozote bila kibali ni kosa. Kwa mfano wakati nikifanya utafiti huu wananchi waliokuwa wanakata miti misituni waliposikia mlio wa gari wengi wao walikuwa wanajificha au kukimbia wakidhani ni mafisa msitu. Ikiwa wananchi wanasikia mlio wa gari wanakimbia ina maana wanajua wanafanya kosa, pakiwepo na ulinzi wa kila siku uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji utapungua sana. Mfano mzuri ni Hifadhi ya Wami-Mbiki. Hifadhi hii imefanikiwa kulinda hifadhi kwa kutumia ulinzi shirikishi (Patrol).

Kilimo mchanganyiko

Kilimo cha kunyanganya miti na mazao ya chakula au biashara ni njia muhimu ya kunusuru misitu. Utafiti ufanyike kujua ni miti aina gani inaweza kuchanganywa na mazao ya chakua na biashara. Katika utafiti huu

imeonekana dhahiri kwamba mazao ya chakula yanaweza kuchanganywa na miti ya matunda kama miembe na michungwa.

Majiko sanifu

Wananchi wapewe elimu na utaalamu wa kutumia majiko sanifu na kuachana na matumizi ya majiko yanayotumia mafiga matatu. Kwani majiko ya aina hii hutumia kuni nyingi ukilinganisha na majiko sanifu ambayo hutumia kuni au mkaa kidogo.

Hitimisho na mapendekezo

Kutokana na utafititi huu ni ushahidi tosha kuwa misitu ni muhimu sana kwa maisha ya watu vijijini na mijini. Faida wapatazo wananchi kutokana na misitu ni nyingi, faida hizo ni nishati (kuni na mkaa), miti ya ujenzi na mbao. Faida nyingine ni asali, matunda, chakula na malisho ya mifugo. Kwa kuuza mbao na mkaa wananchi wamepata fedha, baadhi yao wameweza kuinua kipato chao kwa kiasi kikubwa. Wapo wananchi waliotumia kipato chao kujenga nyumba za tofali na kulipa ada za watoto wao, wapo waliorekebisha nyumba zao pia kulipia gharama za matibabu. Pamoja na faida hizo yapo matatizo pia. Yapo maeneo ya misitu yaliharibiwa kwa kuchomwa moto, kukatwa miti kiholela bila kupanda miti mipya. Kutokana na hilo misitu mingi iliyokuwepo zamani imetoweka na eneo kubwa kubaki vichaka. Mijengo na miti ya mbao hakuna, inapatikana kwa shida na mbali sana kutoka kwenye makazi ya watu. Hali ya ukame imeongezeka, mvua hakuna, haya yote ni matokea ya kutoweka kwa misitu ambayo ni chanzo kikubwa cha kuvuta mvua. Misitu ipo tu kwenye maeneo ya maziara.

Mapendekezo

- Kutoa mikopo kwa watu waishio vijijini ni muhimu sana ili kuwawezesha watu kujishughulisha na shughuli nyingine tafauti na uchomaji mkaa, kama kujihusisha na kilimo cha kisasa na kufanya biashara na wengine kufuga ng'ombe, mbuzi na kuku wa kisasa ili kuboresha maisha yao.
- Ili kutatua tatizo la mifugo kushambulia mashamba ya wakulima, sheria ndogondogo katika vijiji za kuwabana wafugaji ziwepo au zitungwe. Kwa vile vijiji vyenye sheria hizo ndogondogo, sheria hizo zitiliwe makazo na zifuatwe bila upendeleo.
- Wananchi waelimishwe na kushauriwa kutotumia njia za utayarishaji mashamba kama kuchoma moto na uondoaji wa visiki ambazo zinaweza kuathiri uoto thabiti wa asili.

- Wananchi waelimishwe kuhusiana na umuhimu wa kupanda miti. Mwamko wa upandaji miti katika vijiji vya utafiti huu upo chini sana. Tofauti na miti ya matunda wananchi wanapanda miti ya muarobaini na mikenge Pawepo na juhudi za kutoa miche ya miti bure ili kuamsha ari ya upandaji miti.
- Sheria ndogondogo za vijiji zitumike katika kulinda misitu na mazingira ya kila kijiji.
- Pawepo na ulinzi dhabiti wa misitu, patroo.

Machapisho

Boserup, E. 1965. The Conditions of Agricultural Growth. Allena and Unwin, London.

Malthus, T. R. 1798. An Essay on the Principle of Population.

Mhache, E. P. 2004. Tree Planting and its Impacts on the Livelihood of Communities in Unguja, Zanzibar. M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.

Mhache, E. P. 2005. Athari za upandaji miti na maisha ya jamii Unguja, Zanzibar. Muingiliano kati ya mashamba ya misitu ya serikali ya kupandwa na ya jamii na adhari zake katika bioanuwai Zanzibar, Tanzania. Pg. 17-28 Turku University, Department of Geogrpahy Publications B Nr 4.

Mhache, E. P. 2007. Deforestation an Obstacle to Sustainable Development: The role of Higher Learning Institutions in Sustainable Responses. In Huria Journal. The Open University of Dar es Salaam. Vol. VII No. 1 June 2007. Pg. 112-124.

Tiffen, M., Mortimore, M. and Gichuki, F. 1994. More People Less Erosion. Environmental Recovery in Kenya. London, John Wiley.

UHAKIKA WA UMILIKI WA ARDHI, MPANGO WA MATUMIZI ARDHI WA KIJIJI NA RASLIMALI YA MISITU MAGHARIBI MWA WILAYA YA BAGAMOYO

Jussi Ylhäisi, Taasisi ya Taaluma ya Maendeleo, Idara ya Taaluma ya Siasa na Uchumi, Chuo Kikuu cha Helsinki, Finland

Idadi ya watu katika eneo la magharibi mwa Wilaya ya Bagamoyo imeongezeka sana, lakini vile vile tija katika mashamba imepungua. Kutokana na hali hili ingetarajiwa kusiwe na hela vijijni, lakini kuna hela kuliko siku za nyuma. Viashiria vya kuwepo kwa hela vijijini ni vitu mbali mbali , vinavyoonekana vijijini ambavyo havikuwepo miaka kumi iliyopita, kama viti vya plastiki katika mabaa; pikipiki; simu za kiganjani; na hata magari binafsi. Pia siku hizi kaya hununua sehemu kubwa ya chakula badala ya kuzalisha wao wenyewe kwa ajili ya kujikimu kama inavyoelezwa na Haapanen katika makala hii. Pesa inatokana na mauzo ya raslimali ya asili inayosimamiwa na serikali, kama mbao na mkaa. Pia fedha inatokana na uuzaji wa raslimali kwa wageni wanaojihusisha na biashara ya kaboni na wenye miradi ya biofuels na ardhi. Katika eneo la utafiti, biashara ndogo nyingi ya uuzaji wa ardhi imefanyika zaidi ya eneo jirani la Kilosa ambako eneo la vijiji vyote isipokuwa makazi na mashamba vimekodishwa kwa miaka 99. Kadiri ya sera na sheria, raslimali hizi zinatakiwa kusimamiwa na vijiji, na wanakijiji wanaweza kuwa wamiliki wa ardhi. Kwa wakati huu wanakijiji wanafaidi kutokana na 'raslimali zao' lakini bila mpango wa uratibu hali ambayo imeleta hali isiyoendelevu kitamaduni, kijamii, kimazingira na kiuchumi.

Maana ya uhakika wa umiliki ardhi ni kwamba umiliki wa ardhi (binafsi, kikundi na umma) uko salama kutoka uporaji wa ardhi, ubadhirifu, mgawanyo wa upendeleo na matumizi yasiyo halali. Uhakika wa umiliki ardhi ni muhimu kwa sababu ni jambo muhimu katika maendeleo ya uchumi wa vijijini, uzalishaji katika kilimo, amani na kufuata utaratibu, na vile vile usimamizi endelevu wa maliasili. Katika kazi hii swala haki sawa katika kupata maliasili na haki za makundi ya watu waliokatika hali hatarishi linazingatiwa. Kwa ujumla mfumo wa siasa na mgawanyo wa madaraka katika nchi

unapobadilika bila sera au mipango sahihi na thabiti ya utekelezaji wa kuhamisha umiliki wa ardhi, na wakati huo huo kukiwa na msukumo kutoka jamii ya kimataifa wa kubadili mfumo wa umiliki wa ardhi, kuna hatari ya tabaka aali la wenye uwezo kuuteka mfumo. Watu wenye madaraka (Grover et al, 2007) au wenye uelewa hutumia hali hiyo kujigawia mali ya umma kwa manufaa yao binafsi (Raphael & Swai, 2009). Katika hali halisi, serikali inapochukua jukumu la usimamizi wa mali ya umma inaleta hali mali isiyo na mwenyewe ambapo taratibu na sheria za umiliki wa ardhi zinazoheshimiwa zinakosekana (Ribot, 2003). Kadiri ya utafiti huu jambo hili linafanyika kwa uwazi nchini kiasi kwamba inaonekana kuwa linakusudiwa (e.g. Nathan et al., 2007). Sasa yeyote anaweza kutumia raslimali kwa manufaa yake mwenyewe bila vikwazo vyovyote (e.g. WB 2009). Katika mada hii sheria ya vijiji ya 1999 (the Village Act of 1999), sheria ya ardhi ya 1999 (the Land Act of 1999), sheria ya misitu ya 2002 (the Forest Act of 2002) na sheria ya mpango wa matumizi ya ardhi ya 2005 (the Land use Planning Act of 2005) inatambuliwa kuwa ni sheria zinazoongoza mpango wa matumizi ya ardhi ya kitaifa na sera za misitu, maafisa katika ngazi zote na wananchi wote. Sheria (Acts) hizi zinaridhia aina mbili ya umiliki wa ardhi: umiliki wa jumuiya na umiliki wa mtu binafsi. Katika umiliki wa ardhi wa jumuiya ardhi inamilikiwa kwa pamoja na wanakijiji. Hali hii inataka mipaka ya eneo la kijiji iwe imewekwa (ikiruhusu kuanzishwa kwa msitu wa hifadhi wa kijijivillage). Kwa upande wa umiliki wa mtu binafsi (kwa mfano mashamba binafsi) mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji unatakiwa kuidhinishwa na wataalamu. Sasa hivi mipango mingi ya matumizi ya ardhi ya kijiji imekamilishwa kwa ushirikiano wa wanakijiji na wataalamu. Katika taratibu za kutengeneza mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji, mikutano inafanyika ili kuweka makubaliana kati ya wadau kulinda uhakiki wa umiliki wa ardhi ndani ya mipaka ya kijiji. Kinadharia sera ya ardhi ya Tanzania ni moja kati ya zile zilizopiga hatua kubwa na zilizo multidimensional.

Mada hii inajadili jinsi malengo ya sheria na sera zilizotajwa hapo juu zimetekelezwa na nini kimetokea 1) kwenye utaratibu wenyewe, 2) chuma riziki za watu, 3) mali asili and 4) maendeleo endelevu. Mwishowe baadhi ya mapendekezo ya Benki ya Dunia juu ya kupanga uzalishaji wa mkaa maeneo yanayozunguka Dar es Salaam na manufaa yake katika maeneo ya magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo yanajadiliwa.

Maswali muhimu juu mgawanyo sawa wa ardhi na hakika ya umiliki wa ardhi:

1. Je, jamii za vijijini ziko zinapuuzwa au zinazingatiwa katika maswala ya ardhi?
2. Je, mfumo wa umiliki wa ardhi wa Tanzania unawapa uwezo

wanajamii?
3. Je mfumo wa umiliki ardhi wa Tanzania unajumuisha umiliki wa ardhi wa jamii na watu binafsi ili kulenga umiliki wa hakika zaidi?
4. Je, kuna mgongano kati ya haki ya umiliki wa ardhi wa kijadi na wa mtu binafsi?
5. Je, utayarishaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kwa kushirikiana wanakijiji na wataalamu unasaidia uhakika wa umiliki wa ardhi?
6. Je, mpango wa matumizi ardhi wa kijiji unasaidia maendeleo ya kiuchumi kwa kutenganisha matumizi na kuweka wazi matumizi ya sehemu maalum kwa ajili shughuli ambazo hapo awali ziliingiliana?
7. Je mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji unapunguza migongano kati wa washika dau mbali mbali kwa kuhakikisha umiliki wa wanakijiji na wawekezaji (wanaogharamia mpango)?
8. Je utaratibu wa mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji unatoa hali bora zaidi ya usimamizi wa maendeleo endelevu ya mazingira katika kijiji?
9. Nani ni wasimamizi wa maliasili kama misitu na wenye umiliki na haki ya tumia miti katika katika kijiji?
10. Ni mabadiliko gani yametokea baada ya sera mpya na ni mazingira gani yatakuwepo siku zijazo?
11. Je watu wanapenda kutumia ardhi kama dhamana?
12. Muundo utaratibu wa umiliki wa ardhi wa Tanzania umeenea kwa kiasi gani katika vijiji vya wilaya ya Bagamoyo?

Karibu moja ya sita ya eneo la ardhi ya Tanzania liko chini ya uratibu wa Idara ya Misitu, lakini mapato kutokana na misitu haitoshelezi hata kuwalipa wataalamu katika sekta ya misitu. Mapato ya serikali kuu kutokana na misitu yametofautiana kutoka asilimia 1.6 ya thamani ya mbao miaka ya katika ya themanini hadi asilia 4 mwaka 2004. Sehemu inayobaki (asilimia 96.0 – 98.4%) imepotea (Milledge *et al*., 2007). Kadiri ya Draft ya Sera ya Taifa ya Misitu (2009), sababu kuu ya uharibifu wa misitu ni "kuongezeka haraka kwa idadi ya watu, umaskini, kufyeka misitu kwa ajili ya kilimo, mapori kuwaka moto, kufeli kwa sera na masoko, tegemeo sugu la kuni kwa ajili ya nishati, kukithiri kwa matumizi ya raslimali ya miti, na kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi na kutofuata mipango iliyopo". Kutokana na mapato duni kutoka misitu, na gharama kubwa ya kusimamia misitu kiserikali, kunakoambatana na uharibifu wa mazingira na upotevu wa raslimali ya asili, mwelekeo umekuwa kuvipa jumuiya majukumu ya kusimamia matumizi ya ardhi kwa kutumia njia shirikishi za kusimamia matumizi kwa pamoja (Ylhäisi 2003, Ondera, 2004). Kadiri ya Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998,

ni dhahiri kuwa haki ya umiliki wa ardhi yenye misitu na umiliki wa miti kwa jumuia za mahali ni njia pekee ya watu kujitolesheleza mahitaji yao na mahitaji ya muda mrefu ujao ya kuhifadhi na kulinda mazingira (Zahabu et al. 2009: 16). Katika ngazi ya dunia, Tanzania imekuwa ya kiongozi katika eneo hili, kwa mfano, ushiriki wa jamii kupitia miradi *(schemes)* kama *Community-Based Natural Resource Management (CBNRM), Joint Natural Resource Management (JNRM), Joint Forest Management* Namna hii ya usimamizi wa wanyama msitu kwa pamoja *(JFM), Community-Based Conservation Management (CBCM), and Community-Based Wildlife Management (CBWM),* angalia Sanduku 1. Mafanikio yake yamefungua uwezekano wa usimamizi wa pamoja kati ya serikali na jamii na vikundi vingine hifadhi za kiserikali na maeneo ya jamii. Utaratibu huu umefungua njia ya matumizi ya njia kama hizi katika maendeleo ya vijiji na uanzishaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji.

Sanduku1. Miradi ya Wamimbiki CBWM, PFM na VFM.

KatiK eneo la magharibi mwa wilay ya Bagamoyo, vijiji 13 vimo katika mfumo mkubwa wa Wamimbiki CBWM unaojumuisha pia vijiji 11 vya mkoa wa Morogoro. Chama cha wawindaji wa Denmark kwa kushirikiana na vijiji vinavyozunguka eneo hili, wanalinda msitu wenye ukubwa wa ekari za mraba 2500 sambasamba na mpaka wa magharibi wa Bagamoyo. Vijiji vinavyoshiriki, 13 vya Bagamoyo na 11 vya Mororogo vinafaidika kwa njia mbali mbali. Vijiji vyote hupokea ada ya kila mwaka ya shilling za kitanzania milioni moja. Chama cha wawindaji pia kimelipa gharama za uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji na ofisi za ardhi katika vijiji hivi. Gharama za mpango wa mpango wa matumizi ya ardhi katika mwaka wa 2005 ilikuwa shilingi milioni 120, na utaratibu huu ulichukua muda wa miezi sita. Hata za ardhi hazijapokelwa kutoka serikalini, lakini chama na vijiji vinatarajia kuzipata wakati wo wote. Wanavijiji inawabidi kunyima maeneo yao ya kuwinda, kuvua, na kukusanya maliasili. Mradi unaratibu utalii wa kupiga picha, lodging kwa wapenda hali asili na wanyama ili mradi uwe endelevu kiuchumi. Kwa hali ya mazingira mradi umekuwa wa mafanikio: eneo la kilometa za mraba 3000 za msiitu wa asili zimehifadhiwa.

Namna hii ya usimamizi wa wanyama msitu kwa pamoja (JFM) iliyoanza magharibi mwa Bagamoyo mwaka 1997 imeitooa mooyo serkali ya Tanzania na jamii za eneo hili kuwa na imani na umiliki wao wa ardhi na uwezo wao wa kusimamia. Katika mwaka wa 2008, kwa msaada wa Benki ya Dunia lilianzishwa eneo la usimamizi wa msitu kwa pamoja la hekta 19,557 katika wilaya ya Bagamoyo, pia WWF ilianzisha mfumo wa vijiji kuhifadhi ya eneo la hekta 12,000 kwenye misitu ya mwambao wa bahari katika vijiji vinne (12.12.2008, DFO)

Uhamishiaji wa umiliki wa ardhi kwa jamii na watu binafasi kwa njia mpango shirikishi wa matumizi ya ardhi Tanzania na wilaya ya Bagamoyo.

Kuipa jamii umiliki wa radhi iliyomo ndani ya mipaka ya vijiji vyao ni badiliko la msingi. Hapo awali, haki ya wakulima ya kumiliki ardhi ilikuwa ya kijadi. Lakini sasa wanapokea hati inayoonyesha haki ya kumiliki na kutumia mashamba yao. Vile vile vijiji vinapata hata ya eneo liliko ndani ya mipaka ya kijiji. Maeneo haya ya vijiji ni karibu asilia 70 ya eneo lote la Tanzania. Idadi ya vijiji vilivyoandikishwa imeongezeka yakutosha katika miaka kumi iliyopita, inapendekezwa kuwa vimefika idadi ya vijiji 13,000, ingawa taarifa ya wizara inatoas idadi ya vijiji 10, 397 (Table 1: Kironde, 2009). Jedwali 1 linaonyesha ingawa sehemu kubwa ya idadi ya vijiji vimepimwa (ikiwa ni sharti la kupata hati ya kijiji), utoaji wa hati za vijiji uko nyuma. Utoaji wa hati za vijiji zilizobakia na uanzishwaji wa misitu ya hifadhi ya vijiji unaweza kutekelezwa kirahisi na utavipa vijiji haki ya kusimamia maeneo yao.

Jedwali 1: Kuandikishwa kwa vijiji na utoaji wa hati za umiliki wa ardhi (Certificates of customary rights of occupancy (CCROs)

Vijiji vilivyoandikishwa	Vijiji vilivyopimwa	Vijiji vyenye hati ya umiliki wa ardhi	Hati za umiliki (CCROs) zilizotolewa	Vijiji vyenye regista ya ardhi
10 397	8700	753	14 017	30

Uhamishaji wa umiliki wa ardhi kama sehemu ya upangaji wa matumizi ya ardhi hufanyika katika ngazi tatu : 1) muundo wa matumizi ya ardhi wa kitaifa 2) mpango wa matumizi ya ardhi wa wilaya, na 3) mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji (Sanduku 3). Ngazi ya 1 na 2 bado hazipo, na hii ina maana kuwa kuanzishwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya katika ngazi ya kijiji imefanyika pasipo mwongozo wa ngazi ya 1 na 2.

Hiv karibuni kumekuwa na kesi katika wilaya jirani ya Kilosa ambapo halmashauri za kijiji zimelinda maliasili zao kutoka kwa watumiaji wan je (pasipokuwa na mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji ila ikiwepo mipaka ya vijiji), lakini wilaya imepeleka kesi mahakamani. Kijiji kimepoteza haki yake kwa vile sharti wilaya iidhinishe sheria ndogo ndogo za kijiji ili ziweze kutimika kisheria. Katika kesi hii wilaya haikuwa imefanya hivyo. Hadi Februari 2010, Wilaya ya Bagamoyo ina rasimu tu ya mpango wa matumizi ya ardhi wa wilaya (DLUP). Mwezi January 2010, mpango huo ulikuwa karibu kukamilika lakini kompyuta yenye huo mpango iliibiwa hotleini. Kuna vijiji 19

vyenye mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji. Mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji michache iliyokwisha kamilika na kugharimiwa na MKURABITA, imeandaliwa katika vijiji vilivyokuwa na mgongano mkubwa kati ya wafugaji na wakulima. Vijiji 13 vilivyochini ya mradi wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Wamimbiki (Sanduku 1) ndivyo ambavyo vilivyogharimiwa na mwekezaji (Sanduku 2) na anauwezekano wa kukodi ardhi baada ya mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji kukamilika.

Sanduku 2. Kuvutiwa na Ardhi ya Wanakijiji

Hapa Tanzania, kampuni zinazoshughulika na uzalishaji wa biofuel zimetenga hecta 640,000 ya ardhi. Uwekezaji huu umeathiri maelfu ya wenyeji, kwa kuwa umewanyanyang'anya haki yao kumiliki ardhi ya kimila (Sulle & Nelson, 2009). Tume ya Uwekezaji ya Tanzania (Tanzania Investment Commission-TIC) inayo mamlaka ya kutambua na kutenga ardhi kwa ajili ya wawekezaji, na imetenga hecta 2.65 milioni kwa lengo hili (NLA, 2009).
Katika wilaya ya Bagamoyo, TIC imetenga kiasi cha ploti 20 za ardhi kwa wawekezaji watarajiwa. Sehemu kubwa ya maeneo haya yako kwenye mwambao wa bahari wenye fukwe, lakini baadhi ni kwaajili ya uzalishaji wa miwa kwa ajili ya biofuel, inayohitaji eneo la ardhi lenye maji mengi. Kaskazini mwa bagamoyo, eneo la hekta 12,500 limetolewa kwa kampuni binafsi kwa lease ya kipindi cha miaka 33 hadi 99 ilikuanzisha mauzo ya kaboni chini ya Reduced Emissions from Deforestation and forest Degradation programme (REDD). Kadiri ya mwekezaji (Community Development Corporation Limited, 2009), Kukodisha ardhi kwa kampuni binafsi kunatokana na utetezi kuwa jamii iliyopo haina uwezo wa kuifikia mikopo ili kupata dola za kimarekani 40 milioni zinazohitajika kwa ajili ya mradi. Katika hifadhi ya nyaraka za ardhi ya wilaya haikuwa rahisi kupata taarifa juu ya hali ya hati za ardhi za eneo hilo. Kadiri ya sheria, wanakijiji watafidiwa na serikali iwapo ardhi ya kijiji itabadilishwa kuwa ardhi ya umma (general land). Katika hali halisi, wawekezaji wenyewe ndio wanaowalipa wanavijiji mmoja kwa mmoja. Inapotokea kuwa ardhi haijatengwa kuwa ardhi ya kijiji, kampuni zinawafidia wanavijiji kwa ajili ya thamani ya raslimanli zilizopo kwenye ardhi kama miti, malisho na vyanzo vya maji.

Eneo lilitengwa kwa ajili ya kilimo katika rasimu ya mpango wa matumizi ya ardhi wa wilaya ni kilometa za mraba 5767, mara saba ya eneo la kilimo lilipo sasa. Eneo liliko katika kilimo cha umwagiliaji kwa sasa ni kilomita za mraba saba, na kilomita za mraba 164 zimetolewa kwa wawekezaji kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji. Katika mpango huo, eneo kwa

ajili ya ufugaji ni kilomita za mraba 1700, lakini kati hizo ni asilimia 20 tu inayotumika kwa sasa. Hifadhi ya vyanzo vya maji ni kilomita za mraba 855. Kadiri ya mpango huo, eneo lililohifadhiwa kwa ajili ya misitu katika wilaya ni kilomita za mraba 347 tu. Neo lote la wilaya ya Bagamoyo ni kilomita za mraba 9847 (Halmashauri, 2008). Utekelezaji wa mpango huu utaleta mabadiliko makubwa ya mazingira katika wilaya.

Katika Tanzania ni wilaya 13 tu kati ya 127 ambazo zimekamilisha mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya. Hati binafsi za kijadi za umiliki wa ardhi zinatambuliwa kuwa ni za muda tu kwani zitaisha matumizi mpango wa ardhi wa wilaya utakapokuwa tayari. Katika sanduku 3 hatua sita katika utaratibu wa mpango shirikishi wa matumizi ardhi ya wilaya zinaonyeshwa.

Sanduku 3. Utaratibu wa kupanga matumizi ya ardhi wa Wilaya na Kijiji

Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Wilaya (DLUP)
Mpango huu hutoa kwa ajili ya wilaya na vijiji mpangilio wa ubora wamatumizi ya ardhi ili kuelekeza maamuzi.
Sheria ya matumizi ya ardhi inauona utaratibu huu kuwa wa usimamizi wa kisayansi wa ardhi na migongano ya matumizi ya ardhi kati ya washika dau katika wilaya. Mpango wa matumizi ya ardhi wa wilaya unatumika kama mwongozo wa mpango kama huo katika kijiji.

Hatua sita katika mpango shirikishi wa Matumizi ya ardhi wa Kijiji.
Hatua 1. Mafunzo ya maafisa wa wilaya (siku nne): Sheria za Ardhi, wanyama pori, mali asili; kilimo, mifugo, maendeleo ya jamii, kupanga, usimamizi wa raslimali ya maji. Wanakubaliana juu wa mtazamo wa kiwilaya juu ya mabadiliko yanayotakiwa kijijini.
Hatua 2. Kutayarisha rasimu ya Mpango shirikishi wa usimamizi wa matumizi ya ardhi unafanywa na maafisa wa wilaya pamoja na Halamashauri ya kijiji na Mkutano wa kijiji. Wanakubaliana juu ya wajibu wa halamashauri ya kijiji na mkutano wa kijiji katika mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji. Hutambua matatizo, fursa na vipaumbele.
Hatua 3. Survey inafanyika ili kutambua mapaka ya matumizi makuu ya ardhi kama kilimo, malisho, makazi, misitu na wanyama pori.
Hatua 4. Kuweka alama, kuchora ramani na kuandikisha ardhi ya umma na hifadhi, kuandika rasimu ya mpango wa matumizi ya ardhi, kuandika sheria ndogo ndogo kwa njia shirikishi na usimamizi wa wanakijiji.

Hatua 5. Utekelezaji wa mpango, ambapo katika katika maeneo ya makazi inahusisha uboreshaji wa nyumba, njia na barabara, vyoo na mifereji ya maji machafu. Katika kilimo uboreshaji wa ardhi unaambatana na bustani ya miti, kilimo cha mzunguko, agro-forestry, kuboresha umwagiliaji, n.k. Katika maeneo ya malisho ina maana ya kulinda manywesheo ya maji, mifereji ya maji, n.k. Katika maeneo ya misitu na sehemu *fragile*, upandaji wa miti, na ukataji wa kuchagua, matumizi ya majiko sanifu etc; kwenye maeneo ya wanyama pori: kupunguza muingiliano wa wanyamapori na makazi / eneo ya kilimo, ulinzi wa sehemu za maji.

Hatua 6. Kuratibu athari za mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji na uwezo wa wanakijiji na sheria na taasisi zao kuendelea kuutekeleza mradi wao wenyewe (Imeboreshwa kutoka NLA, 2009)

Mipaka ya vijiji vilivyoko magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo

Wilaya ya Bagamoyo inavyo vijiji 82 na mipaka ya vijiji 79 imepimwa hadi 2007. (Vijiji vitatu vingine viko karibu na Hifadhi ya Taifa ya Sadani (578 km^2); havijakubaliana na upimaji wa mipaka ya hifadhi). Ndani ya wilaya ya Bagamoyo, wastani wa la kijiji ni kilomita za mraba 110. Mipaka kati ya vijiji imeonyeshwa kwa wastani wa alama (boundary posts) 10. (Kwa nyongeza, asilimia 60 ya vijiji vina mito inayoongoza sehemu za mipaka. Mara nyingi mito ya kudumu imekuwa mipaka ya vijiji (Plans, 2007).) Katika hali halisi, mistari kati ya alama za mipaka imenyooka, na kwa hiyo mashamba mengi yamegawanywa na mipaka kati ya vijiji viwili. Siku za karibuni kumekuwa na matukio ambapo sehemu ya shamba inayoangukia katika kijiji kingine , imeuzwa na kijiji kingine kwa wawekezaji kwa sababu mkulima ana haki ya kumiliki ardhi katika kijiji anachoishi tu.

Utaratibu wa kufanya Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Kijiji katika wilaya ya Bagamoyo

Wakati wa kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji, timu ya wawezeshaji inatoa mapendekezo ya matumizi ya mbali mbali ya ardhi. Migongano kati ya wafugaji na wakulima ni jambo gumu zaidi kiasi kuwa maisha ya watu yamepotea. Kadiri ya Kamati ya Taifa ya mpango wa matumizi ya ardhi (National Land Use Planning Committee) wafugaji ni kundi lililohatarini linalotakiwa kuangaliwa kwa umakini katika sheria ya ardhi ya kijiji (NLA, 2009). Wafugaji wameridhika na utaratibu wa mpango

wa matumizi ya ardhi ya kijiji katika wilaya ya Bagamoyo kwa kuwa utaratibu huu unahalalisha haki yao ya kutumia ardhi, ingawa katika kila kijiji kilichokamilisha mpango maeneo ya malisho yamekuwa madogo kuliko awali. Katika vijiji vingi uwepo wa Wamasai ni chini ya miaka 20. Wakulima wanakubaliana na mpango kutokana na ushauri wa timu ya wawezeshaji wanaowaambia kuwa mpango utaleta sheria zitakazowazuia wamasai kulishia mifugo katika maeneo Fulani. Wakulima wanashauriwa kuwa hali itakuwa bora zaidi ya ilivyo sasa. Katika baadhi ya maeneo Wamasai ni wahamiaji wageni kutokana na maeneo kuonekana hayana mwenyewe (open access) nchini Tanzania. Katika sehemu nyingi za wilaya wafugaji hulisha mifugo katika maeneo ya misitu yaliyofyekwa. Hali hii inapunguza uwezekano wa misitu kuchipua upya, na sehemu kubwa za magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo tayari zimeanza kubalika kutoka hali ya misitu na kuwa maeneo ya wazi ya malisho (grazing steppes).

Uzoefu katika Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Kijiji

Mtazamo wa maafisa na wanakamati ya kijiji ya maliasili juu ya mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji ni wa kujenga. Lakini kuna hali ya kuwavunja moyo kwa sababu ucheleweshaji wa hati zinazoahidiwa. Familia zilizobadili kwenda matumizi sahihi ya ardhi kutoka matumizi mengine ili kutekeleza mpango imebidi kunyima. Kwa mfano, baada utaratibu wa mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji cha Msoga, wanakijiji wanatarajia kupokea hati za ardhi na rejesta ya nyaraka imejengwa katikati ya kijiji. Bei ya ardhi imepanda baada kuhamisha haki ya ardhi, na ziko juu zaidi ya kitovu cha kata umbali wa kilomita 10. Pia idadi ya miradi ya maendeleo katika kijiji imechangia kupanda kwa bei ya ardhi. Kadiri ya mwenyekiti wa kijiji (mkutano, Disemba 2008) upungufu pekee wa utaratibu mpango wa matumizi ya ardhi ni ongezeko la ugomvi kati ya majirani katika kijiji.(Manara (2008) alipata taarifa sawa na hizi katika wilaya jirani ya Handeni). Wafugaji bado wanaingia katika maeneo ya kilimo cha mazao yaliyopendekezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika kijiji (mahojiano, Februari 2010).

Sanduku 4. Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Kijiji cha Msoga

Kitabu cha mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji cha Msoga, wenye eneo la kilomita za mraba 29.5 na idadi ya watu 1926, kina kurasa 61 zenye taarifa juu ya matumizi ya ardhi na ramani za matumizi ya ardhi katika muundo unaoonyesha rejea za kijiographia (Jamhuri, 2007). Hii inaonyesha kuwa wawezeshaji walitumia njia sahihi katika kazi yao ya kuwashirikisha wanakijiji, wakiheshimu mawazo yao na kuwawezesha kufikiri juu ya hali ilivyo, kuwatia moyo wajadiliane na wataalamu wa timu ya mipango. Tabia hii inarahisha kuuliza maswali juu ya umiliki wa ardhi, sheria ya ardhi na haki katika usimamizi wa ardhi.

Jambo la namna ya kuwawezesha watu walio maskini zaidi halitajwi katika kitabu, lakini maamuzi yanafuata yanamanufaa sawa kwa kila mtu katika kijiji. Washiriki katika mkutano walikuwa na mtazamo kuwa eneo lilidhibitiwa na kijiji ligawanywe kwa watu, na watumiaji binafsi waliweza kukubaliana na mkutano wa kijiji juu maeneo ambayo wangegawiwa. Hatimaye washiriki walikubaliana kuwa ploti itakayogawiwa kwa wanakijiji kwa ajili ya ujenzi wa makazi iwe robo eka. Wale walio na eka moja walazimike kugawanya ardhi yao kwa watoto wao au kuuza kwa wanakijiji wengine.Baada ya majadiliano, iliamuliwa kuwa kuongeza uzalishaji kwa kila eneo badala ya kupanua ukubwa wa mashamba. Kila kitongoji kilitakiwa kuteua washiriki wawili ambao wangejifunza mbinu mpya za kilimo. Inaonekana wawezeshaji wakisaidiwa na timu ya mipango waliawaongoza wanakijiji kuelekea mwelekeo uliamuliwa tayari na wilaya (angalia sanduku 3, hatua 1).

Washiriki walikubaliana kuwa msitu wa hifadhi wa kijiji ulihitajika, na pia ulitakiwa mpango wa kuongeza misitu, kutunga sheria ndogo ndogo za kuilinda misitu, vyanzo vya maji na maeneo mengine ya matumizi maalum. Wakati huu, kila kaya hupanda miti 10 kwa mwaka. Kuna hekta 180 za msitu wa hifadhi wa kijiji, misitu 13 inayohifadhiwa kijadi, njia ya ng'ombe yenye urefu wa kilometa 1.7, kitalu cha miti, bwana la maji lenye ujazo wa mita za mraba milioni moja, mradi wa umwagiliaji wenye eneo la hecta 177 ambao uko kwenye maandalizi. Wafugaji walihama kutoka msitu wa hifadhi ulioanzishwa na wanakijiji, pia wanakijiji walitunga sheria ndogo ndogo kwa ajili ya kutekeleza mpango.

Mwezeshaji alieleza ytaratibu wa kimila wa kusajili ardhi na kufafanua mambo, kwa mfano haja ya kuamua namna mashamba kijijini yatakavyopimwa: mojas baada ya linguine, au kwa kutumia eneo kubwa njia mbayo haitumii muda mwingi. Katika mkutano uliofuata wanakijiji waliamua kutengeneza ramani ya mipaka kwa pamoja katika makundi ya watu kumi kumi ili kupunguza gharama.

Wanakijiji wanaona kuwa hawana nguvu ya kisheria ya kulinda misitu yao na kuwa msitu wa hifadhi wa kijiji huwezi kuanzishwa bila kuwa na utaratibu mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji. Imani hii kati ya wanakijiji inatokana na taarifa za maafisa wa misitu, ingawa walipoulizwa maafisa walidai kuwa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji sio wa lazima. Pia wanakijiji wana imani kuwa hifadhi za misitu za kijiji zinaanzishwa ili wanakijiji wapande miti humo.Wanavijiji wanamatazamo kuwa hifadhi ya mistu ya kijiji haiwezi kutumika. Wanapoelezwa juu ya sheria nasera ya misitu, yaani kuanzisha hifadhi ya misitu kwa ajili ya chanzo cha mali asili kwa ajili ya jamii, wanaanza kuwa na mwelekeo wa kulipenda kama ilivyokuwa miaka kumu iliyopita (Ylhäisi, 2003). Hata hivyo kuanzishwa kwa misitu ya hifadhi ya kijiji kunahitaji mipaka ya kijiji iwe imewekwa bayana (Forest policy, 1998).

Misitu na Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Kijiji

Karibu nusu ya bajeti ya taifa ya kupambana na uharibifu wa mazingira, inatengwa kwa ajili ya mpango wa matumizi ya ardhi (NLA, 2009). Hii inaonyesha kuwa serikali inatambua nguvu ya haki ya umiliki wa ardhi kuwa ni ufnguo wa hifadhi ya mazingira. Mpango wa matumizi ya mazingira unaambatana na elimu na mazingira na mipango, kwa kufuata kanuni za maendeleo endelevu. Kwa mfano, matokeo ya mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji kule Kisarawe umekuwa wa manufaa: kutokana na kuwepo kwa mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji, karibu vijiji vyote vimejenga ofisi za usajili wa ardhi. Vijiji vinaweka mipango ya matumizi ya ardhi wazi ukutani na vimeunda sheria ndogo ndogo, cha msingi zaidi ni kuwa kasi ya uharibifu wa misitu imepungua kwa asilimia 90 (NLA, 2009). Kwa upande wa sehemu ya magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo, sio rahisi kufahamu matokeo kama hayo ingawa mikutano ya mpango wa matumizi ya ardhi na shughuli zake vimekwishafanyaika katika baadhi ya vijiji. Lakini kwa vile hati bado hazipatikana maafisa wa kijiji, viongozi, na wanavijiji wanatatanishwa juu ya haki na wajibu wao.

Kuna mgongano kati ya mtazamo wa maafisa wa misitu na sera ya kitaifa. Vile vile kuna mgongano kati ya uharibifu wa mazingira unaoonekana kwa njia ya utalaam wa remote sensing kutoka kwenye picha za satelaiti na kuonekana unapotembea kwenye 'transects' na mtazamo wa jamii, maafisa wa kata na wa wilaya. Kuna mgongano kati ya bajeti ya taifa, ambayo hutenga fedha kwa ajili ya mpango wa matumizi ardhi (land devolution), na serikali kuwaruhusu vijana kufanya ajira binafsi ya kuchoma mkaa. Unakosekana udhibiti na utiaji nguvu wa utekelezaji wa sheria zinazohusu matumizi ya maliasili(Madulu, 2005), na inajulikana kuwa katika hali halisi ya utekelezaji,

kuna mwelekeo kuwa watu wako huru kutumia raslimali asili. Itakapotokea kuwa misitu imekwisha na hakuna tena ajira binafsi katika uchomaji wa mkaa, kupata ajira mbadala na njia nyepesi ya nishati kwa ajili ya miji itakuwa changamoto kubwa.

Kwa vyovyote vile, kutakuwa na upotevu mkubwa na wa kudumu wa bionuai (biodiversity). Bado kuna baadhi ya hifadhi ya misitu ya kijadi, hata katika maeneo yenye uharibu mkubwa, ambazo zimekuwa na utajiri wa aina mbali mbali za wanyama na mimea (Mwihomeke et al. 2000). Katika utaratibu wa mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji, wawezeshaji hushauri wanakijiji kuilinda pia misitu ya kijadi. Katika kila mpango wa matumizi ardhi wa kijiji unaokamilika kuna karibu misitu 20 inayolindwa kijadi, ambayo sasa unalindwa kisheria.

Charcoal production, impact on livelihood and sustainable development

Chanzo kikubwa cha pesa kwa wanakijiji ni uuzaji wa mkaa. Chanzo hiki cha fedha pia kimegawanyika karibu sawa katika kijiji. Pembezoni mwa barabara kuu kama kilometa 200 kutoka Dar es Salaam, mchango wa uzalishaji wa mkaa kwenye pato la kaya mwaka wa 1992, 2000 na 2002 ulikuwa mkubwa kutoka US$ 176, 445 hadi 645, kwa mtiririko huo, ambalo ni juu ya kima cha chini kinacholipwa kwa wafanyakazi wa serikali an sekta binafsi (Malimbwi & Zahabu 2008: 96). Katika wilaya ya Bagamoyo. Misitu iliyoko kando kando ya barabara kuu imevunwa kwa ajili ya kuchoma mkaa na kuuuza mjini Dar es Salaam. Hali kama hii imetajwa sehemu mbali mbali nchini Tanzania (e.g. Strömquist & Backéus, 2009; Drigo 2005). Mwaka 2005, uchomaji wa mkaa ulikuwa ndio matumizi makuwa ya misitu hadi umbali wa kilometa 170 kutoka Dar es Salaam. Kutoka mwaka 1991, mpaka hasa wa eneo la uchomaji mkaa ulikuwa kilometa 50 kutoka Dar es Salaam. Kwa hiyo eneo kuu la uchomaji mkaa linaenea kilometa 2 kila mwaka (Ahrendsa et al. 2010). Zaidi, Ahrendsa et al. (2010) wamegundua kuwa hakuna uhusiano kati ya kiwango cha uharibifu katika msitu na sera ya usimamizi au sheria na taratibu zinazosimamia msitu.

Kadiri ya utafiti wa Mhache, mwaka 2008, karibu asilimia 20 ya kaya zilijihusisha na uchonaji wa mkaa usio halali, ingawa idadi halisi ni kubwa zaidi ya hiyo.Katika mkutano mmoja katika kijiji cha Msata, uliowajumuisha wajumbe wa halmashauri ya kijiji na maafisa wa mali asili, mtazamo wa jumla uliona kuwa kila mwanakijiji anashiriki katika uchomaji mkaa. Hii ni biashara nzuri kwani ni karibuu na mji wa Dar es Salaam unaokua haraka. Makala zingine zimetaja kuwa hii ni namna ya kugawanya mapato kutoka mjini

kwenda vijijini. Hata hivyo hii inafanyika kwa gharama ya uharibifu wa misitu na mazingira, kadiri ya Mwampamba (2007) misitu iliyoko katika ardhi ya umma inaweza ikawa imetoweka ifikapo mwaka 2028.

Wakati huu, misitu katika wilaya ya Bagamoyo imevunwa sehemu zenye uwezekano wa kusafirisha mazao ya misitu.Upande wa kaskazini, sehemu ya uchomaji wa mkaa imeenea hadi hadi kwenye mpaka wa wilaya ya Handeni. Kwa ajili ya nani na wa sababu gani hili linatokea? Maafisa wa misitu wa Wilaya na Tarafa wanaweza kusema: "Tunahitaji kuihudumia miji. Kila mmoja aliyeko mjini anatumia mkaa. Hili ni tatizo lakini hakuna njia mbadala". Mtengeneza sera wa wizara pia anaweza kusema: Miji na watu wanahitaji nishati rahisi; hakuna kinachoweza kufanyika juu ya hili". Hakuna? "Katika sera mpya tunao mpango wa kuratibu sehemu za kuuzia mkaa ambapo umbali kuti ya sehemu za kuuzia unakuwa kilomita 10" (Mahojiano, December 2008). Wakati huo huo, ripoti ta Halmashauri (2008) kwa halmashauri ya wilaya juu ya misitu ya wilaya inasema: "Jamii zote hutegemea vyanzoi vya mapato kutoka raslimali za misitu nah ii husababisha uharibifu mkubwa wa misitu. Uchomaji wa mkaa umeenea kila mahali. Katika vijiji na taasisi, ufahamu na uelewa wa njia mbali mbali za umuliki wa misitu haupo. Pia takwimu za misitu hazitoshelezi, nah ii ni kikwazo katika usimamizi wa misitu."

Wanakijiji wanalipwa kwa u´kuchoma mkaa, lakini thamani ya miti inakwenda bure bila malipo kwa walaji wa mjini Dar es Salaam. Sehemu kubwa ya mkaa unapatikana bila malipo kwa ajili ya mali ghafi (miti) inayotumika, na leseni na kodi zinaepukwa. Sera makini ya bei ya mali ghafi inayolipwa na wachoma mkaa ingeweza kuwachochea kutumia tekinolojia bora zaidi za uzalishaji wa mkaa (WB, 2009). Hakuna kiwanda cha mbao katika wilaya. Mwaka 2008 kulikuwa na maafisa misitu (foresters) 9 katika wilaya. Mapato kutokana na leseni katika mwaka 2007 yalikuwa kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 4.

Jedwali 4: Mapato kutokana na Leseni za mazao ya misitu

	Leseni za mkaa	Leseni za mbao
Mamlaka ya Mapato Tanzania	109 000	100 000
Vijiji	50 000	100 000
Halmashauri ya Wilaya	80 000	2400 000
Serikali Kuu	200 000	60 000
Jumla	489 000	2660 000

Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. 2008.

Hitimisho

Namna hii ya mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji una mambo kadhaa yakuvutia: 1) Mashamba yanayotumiwa na wanakijiji yanakuwa mali yao kisheria; 2) Wakati huho huo eneo la kijiji linalobakia linamilikiwa kwa pamoja; 3) Sehemu ya ardhi ya umma inaendelea kuwa ya pamoja na inaweza kutumiwa endapo kutakuwa na mahitaji zaidi yap loti; 4) Maeneo ya matumizi ya ardhi yameainishwa. Haya yanafanya muundo huu wa mpango uwe kivutio: jamii kumiliki ardhi kidemokrasia, kuchanganya mfumo wa umiliki binafsi wa ardhi na mahitaji ya jamii ya kisasa na ya kiuchumi. Mfumo huu pia unaruhusu urahisi wa kubadili kwa kulingana na mahitaji ya baadaye yasiyofahamika bado na yasiyotabirika kama mabadiliko katika mbinu za kilimo (k.m matumizi týa trekta) na mabadiliko ya hali ya hewa (k.m. REDD). Maeneo makubwa ya malisho yanaweza kutokuwa ya manufaa au yanaweza kuwa njia kuu ya kuchumia riziki (k.m kutokana na kubadilika kwa uoto). Hali ya kupanda bei ulimwenguni ya mwaka 2008 inaweza kujirudia au mahitaji ya bioenergy yanaweza kuongezeka. Hata hivyo, ni muhimu kuwa kasi ya utaratibu wa kutengeneza mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji, ambao unazorota, izidishwe. Desturi ya kuwa mwekezaji ndie anayewalipia utaratibu wa mpango ina hatari ya kuchezea mpango. Hatari hii inaweza kuepukwa kwa njia ya maadali ya wawezeshaji wa utaratibu huu. Wataalamu wengi wanatoka katika ofisi za wilaya. Hili pia linaweza kuwa chanzo cha matatizo iwapo hawatakuwa mstari wa mbele kuunga mkono utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji.

Ili kuondoa hali ya hivi karibuni ya maeneo ya maliasili kutokuwa na mwenyenayo, njia ya haraka zaidi ya mpango wa matumizi ya ardhi inahitaji. Kuna uzuri kuwa mipaka ya vijiji imeainishwa karibu kila mahali wilayani Bagamoyo na katika Tanzania. Hii imekuwa sehemu ngumu nay a gharama ya utaratibu wa umilishaji wa ardhi. Msisitizo sasa unatakiwa kuwa katika kuhakikisha kuwa ardhi iliyoko ndani ya kijiji inabaki kuwa mali ya wanakijiji hicho. Hati ya ardhi ya sharti iwe na nguvu ya kisheria kuanzia wakati mpango wa ardhi wa kijiji ulipokamilika. Hati ya kijiji itumwe mara moja kwa kijiji husika na kukipa haki ya kisheria ya kulinda mazingira, mali asili na umiliki wake. Hii itasaidia jamii kuepuka wananchi wake na watu wa nje kupora ardhi. Pia itasaidia kuepuka uhamiaji wa makundi kutoka sehemu yenye msongamano wa watu au mifugo au wachoma mkaa kutoka maeneo yaliyoharibiwa, mambo ambayo huweza kupangwa na watu wenye nguvu katika dola.

Matokeo yenye kuleta matumaini katika utaratibu wa mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji ni kuwa kasi ya uharibifu wa misitu imepunguzwa

kwa asilimia 90 katika vijiji vilivyokamilisha mpango wa matumizi ya ardhi. Sheria ya matumizi ya ardhi ya 2009 (NLA of 2009) inaahidi kuwa "Mpango wa matumizi ya ardhi wa kijiji utaathiri mting´do wa maisha wa wananchi". Ongezeko ha haki ya wanavijiji inaenda pamoja na kuongezeka kwa wajibu, na matokeo yake na kuongezeka kwa moyo (commitment) katika usimamizi wa ardhi ya umma, misitu, inatoa fursa zaidi za kijamii na kiuchumi; na inatoa ulinzi na raslimali kwa walio maskini zaidi katika jamii.

Jambo kubwa katika wilaya ni uchomaji wa mkaa kwa ajili ya nishati kwa watu wa Dar es Salaam an Zanzibar. Karibu kila msitu umetumika kwa ajili ya kujipatia nishati. Kinachojitokeza sasa ni jukun´mu la vijiji la siku za baadaye: Je vina haki ya kumiliki na kusimamia maeneo yao ya misitu iliyorejeshwa? Au ni watekelezaji tu? Kadiri ya World Bank's (2010) uchambuzi unaotokana na washika dau, wachoma mkaa wapo kwa kuwa kuna kitu cha kuuza. Katika World Bank (2009) Policy Notes, kunasisitizwa umuhimu wa hifadhi ya misitu ya kijiji, lakini jambo hili linakosekana katika makal ya World Bank (2010) inayolenga zaidi katika ukusanyaji wa kodi na ushuru na kupunguza bei za mlaji. Kuna hatari kuwa maafisa wa serikali hawataachia mfumo wa zamani wa kussimamia kutoka juu ambapo wanakijiji wanakuwa watekelezaji tu. Kwa hakika hii ni kinyume cha sheria za sasa na cha programu za CBWM na PVFR zilizoonyesha matumaini makubwa.

Machapisho

Ahrendsa Antje, Neil D. Burgess, Simon A. H. Milledge, Mark T. Bulling, Brendan Fisher, James C. R. Smart, G. Philip Clarke, Boniface E. Mhoro, and Simon L. Lewis. 2010: 14556–14561. Predictable waves of sequential forest degradation and biodiversity loss spreading from an African city. PNAS 17, 2010, vol. 107, no. 33.

Community Development Corporation Limited, 2009. Feasibility study report for the establishment of Bagamoyo forest project at Mbwewe ward, Bagamoyo District, Tanzania. Dar es Salaam . 80 p.

Drigo, R. 2005. WISDOM – East Africa. Woodfuel Integrated Supply/Demand Overview Mapping (WISDOM) methodology: Spatial woodfuel production and consumption analysis of selected African countries. Rome. FAO – Forestry Department – Wood Energy. 78 pp.

Grover, R. l, M.-P. Törhönen, D. Palmer, & P. Munro-Faure. 2007. Good governance in land administration and land tenure. Land Reform, Land Settlement and Cooperatives 2007/2:pp. 7–17.Rome. FAO.

Haapanen, T. & E. Mhache. 2009. Food systems and deforestation in eastern Tanzania: How the shift from subsistence food system to market-based food system relates to loss of forest cover in Lugoba ward, Bagamoyo district.Trondheim, Norway. Presented at Nordic Africa Days, 1–3 October 2009.

University of Turku and University of Dar es Salaam. 18 pp. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. 2008. Taarifa za Kiasi cha Aridhi Wilayani Bagamoyo. Kumb BG/DC/F30/3/11. Bagamoyo. Bagamoyo District. 8 pp

Jamhuri. 2007. Mpango wa Matumizi Bora ya Arhidi ya Kijiji cha Msoga, Kata ya Lugoba. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Halmashauri ya Kijiji cha Msoga. Bagamoyo. Bagamoyo District. 61 pp.

Kironde, J.M.L. 2009. Improving land sector governance in Africa: Case, Tanzania. Presentation at: Workshop on land governance in support of the MDGs – Responding to new challenges. Washington, DC. 9–10 March 2009. Dar es Salaam, Tanzania. Ardhi University. 29 pp.

Madulu, N.F. 2005: 950-960. Environment, poverty and health linkages in the Wami River basin: A search for sustainable water resource management. Physics and Chemistry of the Earth 30.

Malimbwi Roger E. and Eliakimu M. Zahabu . 2008. Woodlands and the charcoal trade: the case of Dar es Salaam City. Working papers of the Finnish Forest Research Institute 98: 93-114.

Manara, K. 2008. The paradox of property and business formalization in Tanzania. KEPA's working papers 22. Helsinki. 24 pp.

Milledge SAH, Gelvas IK, Ahrends A. 2007. Forestry, governance and national development: Lessons learned from a logging boom in southern Tanzania (TRAFFIC East/ Southern Africa, Tanzania Development Partners Group, Tanzania Ministry of Natural Resources and Tourism, Dar es Salaam). Available at http://www.traffic.org/forestry Accessed June 2007.

Mwampamba T.H. 2007: 4221-4234. Has the woodfuel crisis returned? Urban charcoal consumption in Tanzania and its implications to present and future forest availability. Energy Policy 35.

Mwihomeke, S., & C. Mabula, ,& M. Nummelin,. 2000. Plant species richness in the traditionally protected forests of the Zigua, Handeni district, Tanzania. In: Virtanen, P. & M. Nummelin, eds: Forests, chiefs and peasants in Africa – Local management of natural resources in Tanzania, Zimbabwe and Mozambique. Silva Carelica Vol 34: 178–193.

Nathan, I., . et alJ.F. Lund, Q. Gausset, & S.K. Andersen. 2007. On the promises of devolution overcoming the constraints of natural resources management in a village in Tanzania. InThe Journal of Transdisciplinary Environmental Studies Vol 6:1. 15 pp.

NLA. 2009. National Land Use Planning Commission. (Available at:http://www.nlupc.co.tz/aboutus.php) (Sited 25.5.2009.)

Ondera, J. 2004. Lessons learnt on community forest management in Africa. Plans. 2007. Survey of villager boundaries at Bagamoyo District, Coast Region, E768, E768/3, E768/4, E768/6, Registered plans 44943, 44949, 44946, 44947, 8.1.2007. Regional Secretariet Surveyor Coast Region. Kibaha.

Raphael, T. & G. Swai., 2009. The impacts of participatory forest management and local people's perceptions on its implementation at the village level in Mufindi district, southern Tanzania highlands. In Nshubemuki, L., S.A.O. Chamshama, L. Mbwambo, & C. Balama et al.eds. Proceedings of the first Participatory Forestry Management (PFM) research workshop: Participatory forest management for improved forest quality, livelihood and governance. Morogoro. TAFORI. 133–146 pp.

Ribot, J.C. 2003. A theory of access. Rural Sociology Vol 68(2): 153–181.

Malimbwi, R.E. and E. M. Zahabu. (2008). Woodlands and the charcoal trade: the case of Dar es Salaam City. Working Papers of the Finnish Forest Research Institute 98: 93–114

Sulle, E. and Nelson, F., 2009, Biofuels, land access and rural livelihoods in Tanzania. IIED, London.

Strömquist, L. & I. Backéus. 2009. Integrated landscape analyses of change of miombo woodland in Tanzania and its implication for environment and human livelihood. Geogr. Ann. Vol 91A(1): 31–45.

World Bank, 2009. Environmental Crisis or Sustainable Development Opportunity? Transforming the charcoal sector in Tanzania. World Bank, A Policy Note . 72 p.

World Bank. 2010. Enabling reforms: A stakeholder-based analysis of the political economy of Tanzania's charcoal sector and the poverty and social impacts of proposed reforms. 50 p. The World Bank 55140.

Zahabu, E., Eid, T., Kajembe, G. C., Mbwambo, L., Mongo, C., Sangeda, A.Z., Malimbwi, R. E., Katani, J.Z., Kashaigili, J. and Luoga, E.J. 2009. Forestland tenure systems in Tanzania: an overview of policy changes in relation to forest management. INA fagrapport 14. Department of Ecology and Natural Resource Management Norwegian University of Life Sciences. 26 p.

Ylhäisi, J. 2003. Forest privatization and the role of community in forests and nature protection in Tanzania. Environmental Science & Policy Vol 6: 279–290.

Ylhäisi, J. 2006. The change of traditionally protected forests and leadership in Zigua ethnic group, Tanzania. Helsinki. Publicationes Instituti Geographici Universitas Helsingensis A139. 68 pp.

Ylhäisi J. 2010. Sustainable land privatization involving participatory land use planning in rural areas: An example from Tanzania. Land Tenure Journal 1: 91-120. FAO. Rome, Italy.

MAENDELEO YA MFUMO WA CHAKULA VIJIJINI BAADA YA ENZI YA UJAMAA

Uchunguzi kifani kutoka Lugoba, Tanzania

Toni Haapanen, Idara ya Jiografia, Chuo Kikuu cha Turku, Finland.

Utangulizi

Makala hii inatoa majumuisho ya matokeo ya utafiti juu ya mfumo wa chakula vijijini uliofanyika katika kata ya Lugoba, wilaya ya Bagamoyo, Tanzania. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza mabadiliko yaliyotokea katika mfumo wa chakula kinachotegemewa na wenyeji mara baada mwisho wa kipindi cha ujamaa katikati ya kipindi cha 1980-1990. Mfumo wa chakula ni dhana jumuishi inayohusisha uzalishaji, usambazaji, utumiaji wa chakula. Utafiti huu unachukua mtazamo mpana zaidi kuliko inavyokuwa katika tafiti juu ya tija ya kilimo, masoko ya chakula na lishe. Mabadiliko katika ueneaji na muundo wa mfumo wa chakula yanahusishwa na soko huria, mabadiliko ya kiutamaduni na kiteknolojia na kimazingira. Mada za uhakika wa kupata chakula na njia za kujikimu zinajadiliwa. Ingawa makala hii inaweza kuzingatia mambo machache tu muhimu, nina imani inatoa ugunduzi wa kitafiti na mapendekezo yanayotuwezesha kuelewa mada ya maendeleo vijijini na mipango ya baadaye ambayo ni changamani na pana.

Katika kipindi baada ya ujamaa, mtazamo wa kijamaa katika utawala wa kitaifa umeachwa na badala yake mabadiliko kiuchumi yanayozingatia soko huria yameanzishwa. Badiliko hili limeleta mfululuzo wa mabadiliko katika mfumo wa kujikimu kimaisha na mazingira ya vijijini (e.g. Bryceson 1993, Kikula 1997, Ponte 2002). Vyama vya ushirika na vyama vya msingi vilivunjwa na mfumo wa bei za ki-kanda uliondolewa na udhibiti wa serikali katika kilimo ulisimamishwa. Kadiri ya Ponte (1998: 317), kukua kwa mfumo wa kibiashara katika maisha ya vijijini na kuongezeka kwa ushiriki wa wafanyabiashara binafsi katika soko la mazao ya kilimo, yamekuwa ni mabadiliko muhimu katika maisha ya vijijini katika miaka ya themanini. Kama matokeo ya utafiti wa Lugoba yanavyoonyesha, mabadiliko haya yamejitokeza pia katika eneo la magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo.

Mabadiliko ya uchumi na utawala kitaifa yamekuwa na athari katika mfumo mzima wa chakula. Hata hivyo kuna sababu zingine zilizoathiri uzalishaji na matumizi ya chakula wakati huo kama mabadiliko katika utamaduni na mazingira ya eneo husika.

Mbinu za Utafiti

Vijiji vinne vya Lunga, Makombe, Mindu Tulieni and Msoga, vilivyoko katika kata ya Lugoba vilichaguliwa kwa ajili ya utafiti kwa vile vinatofautiana katika ukubwa, mazingira, umbali toka barabara kuu, kufikika, upatikanaji wa huduma za msingi, na mchanganyiko wa makabila. Uteuzi huu pia ulitegemea upatikanaji wa taarifa za utafiti na makala za kitaaluma juu ya vijiji hivyo. Ukusanyaji taarifa kwa ajili ya utafiti huu ulifanyika kutoka Oktoba hadi Disemba 2008 na kutoka Juni hadi Agosti 2009. Pia ulihisisha uchambuzi wa machapisho ya kiserikali, takwimu za maeneo, na taarifa za kitafiti. Taarifa za kitafiti zilikusanywa kwa kutumia dodoso 140; mahojiano 79; majadiliano kwa vikundi 11; na wanavijiji walishirkishwa katika zoezi la kutengeneza kalenda ya misimu; kutembea kufuata transekti na uchoraji ramani shirikishi. Idadi sawa ya wanaume na wanawake wawakilishi wa kaya iliyoteuliwa bila mapangilio ilishirki katika kujaza dodoso. Utafiti huu umetumia taarifa rejea za utafiti uliofanya kikundi cha utafiti kilichowashirikisha Taimi Sitari na Ali M. Sendaro mwaka 1989-90. Watu waliohojiwa ni viongozi wa kijiji; wazee; wafanyabiashara wa reja reja na wa jumla; wataalamu (maafisa ugani; mifugo; afya) na viongozi ngazi za kata na wilaya. Taarifa za kihistoria juu ya idadi ya watu, uzalishaji wa mazao; uuzaji wa mazao; lishe na hali ya hewa zilikusanywa kutoka katika ofisi za vijiji, kata, wilaya na ofisi za takwimu za kitaifa na kimataifa. Picha za angani na za satelaiti zilitumika kuainisha mabadiliko ya hali ya nchi na mazingira. Picha za anga zilizopigwa mwaka 1966 na 1982 na zile za satelaiti zilipigwa mwaka 2007 (Ikonos, 1 meter resolution).

Kupungua kwa uzalishaji chakula

Kilimo cha Mazao

Mfumo wa matumizi ya ardhi wa kijadi ulibadilika sana nchini Tanzania enzi za ujamaa. Kilimo cha mashamba ya kudumu kilizidi kuimarika na kile cha kuhamahama kilizidi kupungua. Wakati mahitaji ya ardhi karibu na kijiji yaliongezeka pasipo mabadiliko makubwa ya tekinolojia ya kilimo, ardhi iliharibika na udongo ulidhoofika, hatimaye uzalishaji wa mazao

ulipungua (Kikula 1997). Mabadiliko haya yalitokea pia sehemu ya magharibi ya wilaya ya Bagamoyo. Wengi wa wakazi wa eneo hili walifanya kilimo cha kuhamahama, isipokuwa wafugaji ambao huunda kúndi dogo tu. Katika mwaka 2008-09 asilimia 60 ya kaya zilizohojiwa katika kata ya Lugoba waliyahama mashamba yaliyokuwa na uhafifu wa rutuba. Hata hivyo sehemu kubwa ya kilimo cha kuhama hama ilifanyika katika mashamba ya familia, na kwa kawaida kulikuwa maeneo mawili au matatu ambamo kilimo cha namna hii kilifanyika. Bado kuna maeneo mapya yanayosafishwa kwa ajili ya kilimo, lakini desturi hii imepungua baada ya kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa. Asilimia 50 ya ardhi ya kilimo inayotumiwa na kaya zilizohojiwa ilikuwa ni ya kifamilia uliyopatikana kwa njia ya urithi au ndoa. Karibu aslimia 12 ya radhi inayotumiwa na wahojiwa ilipatikana kwa njia ya kununua na asilimia 14 kwa njia ya kupewa bure. Karibu 12% ya ardhi ilipatikana kwa kupewa na ofisi ya kijiji na 11% kwa njia ya kufyeka vichaka au misitu bila kibali.

Idadi ya watu katika ya Lugoba iliongezeka karibu mara dufu kutoka watu 9086 mwaka 1984 hadi watu 17924 mwaka 2006 (Vuorela 1987: app. table 1, Lugoba Ward Office 2006). Uchambuzi wa picha za angani na takwimu za satelaiti unaonyesha kuwa ongezeko la eneo la kilimo lilikuwa kwa kasi ndogo zaidi ya ile ya idadi ya watu. Hii inaonyesha kuwa wastani wa eneo linalolimwa na watu binafsi limepungua. Takwimu rasmi za kilimo zinathibitisha hali hii, japo takwimu rasmi za miaka ya nyuma zilipatikana Lunga tu. Mwaka 2008-09, wastani wa eneo la kilimo kwa kila kaya ulikuwa ekari 4.5, lakini median ilikuwa ekari 3.0 na kikilicholimwa na kaya moja. Ukiondoa kaya hiyo yenye eneo kubwa la ardhi, wastani unashuka hadi ekari 3.7 kwa vijiji vyote vinne. Kiwango kikubwa zaidi cha wastani (median) wa ukubwa wa ardhi ya kilimo kwa kila kaya kilipatikana Msoga (ekari 3.5) na kijiji cha wafugaji cha Mindu Tulieni kilikuwa na wastani mdogo zaidi (ekari 2.3). Kijiji cha Lunga kilikuwa na wastani (median) wa ekari 3.0 na Makombe ekari 2.8.

Mwaka 2008-09, karibu wahojiwa wote (96%) walilima mahindi na karibu theluthi mbili mihogo (69%) na aina mbali mbali za maharage (66%) ikijumuisha kunde, mbaazi and choroko. Asilimia 21 ya kaya zilizohojiwa walilima mboga mboga za maboga, kabichi, nyanya, bamia na mchicha. Aina za vyakula zimeendelea kuwa karibu zile zile tangu enzi ya kuanzishwa vijiji vya ujamaa isipokuwa kilimo cha mtama kimepungua. Kilimo cha mboga mboga hasa cha nyanya, matango na kabichi kimeongezeka siku za karibuni, lakini bado haya si mazao muhimu kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji kinakosekana na gharama ya pembejeo ni kubwa. Idadi kubwa zaidi (62%) ya wahojiwa wana miti ya matunda: miembe (41%), migomba (35%), michungwa (32%), mapapai (26%) minazi (9%), topetope (9%) na mafenesi (6%). Mtindo wa kilimo unaotumika zaidi ni ule wa kilimo mchanganyiko wa mahindi na

maharage au mihogo na maharage. Kwa kawaida mboga mboga hulimwa kwenye mashamba ya peke yake na miti ya matunda imepandwa kwenye maeneo ya makazi au mashamba yaliyokaribu na makazi (Sokoni, 2010). Ingawa mazao kadhaa tu ndio hutumika kwenye kilimo mchanganyiko, ni kawaida kuchanganya karibu mazao yo yote katika shamba moja.

Kwa ujumla, watu hawajishughulisha sana na kilimo cha mazao ya biashara, asilimia 30 tu hulima ufuta kwa ajili ya kuuza na kaya chache zinalima miwa, karanga, pamba au korosho. Mazao ya chakula yanazalishwa hasa kwa ajili ya matumizi katika kaya na kwa hiyo uzalishaji wa mazao ni kwa ajili ya kujikimu. Kaya zilizohojiwa ziliuza mihogo (14%), maharage (11%), mahindi (9%), mtama (7%) na maembe (7%). Wahojiwa walitakiwa kukadiria kiwango cha ongezeko ya mauzo tokea miaka ya themenini (1980s). Zaidi ya nusu ya wahojiwa (57%) walitaja kuwa mauzo yalipungua, asilimia 27 walidai kuwa mauzo yalipungua, na asilimia 16 hawakuwa na mabadiliko makubwa. Hata hivyo mauzo hutofautiana mwaka j´hadi mwaka kadiri ya mavuno. Badiliko kubwa zaidi ni kushuka kwa uzalishaji wa pamba, ambao umeendelea kujikita zaidi katika maeneo yenye tija kubwa baada ya kuvunjika kwa mfumo wa vyama vya ushirika mwishoni miaka ya themanini (1980s). Mashamba makubwa ya bega kwa bega katika vijiji vya Lunga, Msoga and Makombe yaligawanywa kwa wanakijiji na kubadilishwa kuwa mashamba ya mazao ya chakula na matumizi mengine.

Wahojiwa wengi zaidi (74%) walitaja kuwa tija kwa eka imeshuka tangu miaka ya themanini, asilimi 10 hawakuona mabadiliko na asilimia 4 walilisema kuwa tija imeongezeka, asilimia 11 hawakujibu swali. Kwa wastani wakulima walivuna 300 kg (median 200 kgs) za mahindi katika ekari moja msimu wa masika katika mwaka wa 2008. Kulikuwa na tofauti kubwa kwa kuwa 27% ya wahojiwa walivuna 100 kg au pungufu katika ekari; 30% walivuna 500 kg au zaidi katika ekari moja. Ni vigumu kutambua kwa hakika kiasi cha upungufu wa tija katika eneo hili kwa kuwa takwimu za uhakika hazipo. Takwimu kwa mwaka za kiwango cha tija katika eka zinaweza kukokotolewa kutoka takwimu za kiwilaya, lakini takwimu hizi zinaonyesha tofauti kubwa kiasi cha kutoaminika. Taarifa za kiwilaya za uzalishaji wa mazao zinatokana na makadirio yanayofanya na maafisa ugani, hata hivyo wastani wa uzalishaji katika eka ukikokotolewa katika kipindi kirefu unaweza kuonyesha mabadiliko. Uzalishaji wa mahindi katika ekari moja wilayani Bagamoyo ni 352 kg kipindi cha 1985-89 na 243 kg kipindi cha 2003-2007, na hii huonyesha mwelekea wa kupungua. Takwimu hizi ziko chini ya viwango vya kitaifa nchini Tanzania, ambavyo ni 542 kg kipindi cha 1985-89 na 449 kg kipindi cha 2003-2007 (FAOSTAT 2010). Kwa kiasi fulani hii inatokana na mvua kidogo na zisizo na uhakika, na kuchanganyika kwa mazao katika

shamba lilelile.

Kadiri ya takwimu zilizopatikana katika mji wa Bagamoyo, umbali wa 65 km mashariki mwa Lugoba, kiasi cha mvua kwa mwaka katika kipindi cha 1964 to 2007 kinaonyesha mwelekeo wa kupungua (Chati 1). Wastani wa mvua kwa mwaka ulikuwa 934 mm katika kipindi cha 1968-77, 1027 mm kipindi cha 1978-88, 1034 mm kipindi cha 1988-97 na 891 mm kipindi cha 1998-2007 (TMA 2010). Viwango vya mvua viwili vya chini kabisa katika kipindi cha miaka 43 vilirekodiwa mwaka 2001 na 2003. Tofauti kwa mwaka ni kubwa, na uwezekano wa kuzidi 800 mm au 1000 mm ni 80% na 43% tu kwa mtiririko huo. Kwa bahati mbaya kituo cha hali ya hewa cha Misioni ya Lugoba hakifanyi kazi tangu mwanzoni mwa miaka ya tisini (1990's) na hakuna taarifa za hivi karibuni na karibu zaidi ya zile za Bagamoyo.



Chati 1. Kiasi cha mvua kwa mwaka (mm) katika stesheni ya mji wa Bagamoyo kipindi cha 1964-2007 (TMA 2010).

Ilikupata kiashiria kingine cha mabadiliko katika mavuno, wahojiwa walitakiwa kutaja idadi ya miezi katika mwaka ambayo wanatumia mahindi waliyolima wenyewe. Kwa wastani, kaya zilitumia mahindi waliyozalisha wenyewe kwa kipindi cha miezi mitano mwaka uliotangulia, ikilinganishwa na miezi 11 miaka ya kati ya themanini. Wahojiwa wengi walidai kuwa hawakuwa wananunua mahindi enzi hizo, na wengine walisema unga wa mahindi haukuuzwa madukani wakati huo. Ingawa mabadiliko makubwa kiasi hichi yanaweza kuwa yametiwa chumvi, uchunguzi wa upatikanaji wa chakula katika soko la Lugoba wa mwaka 1979 kwa ajili ya mradi wa utafiti wa Jipemoyo, na uchunguzi uliofanywa na Vuorela pale Msoga (1987: 215—219)

unaunga mkono wazo kuwa ulaji wa mahindi na vyakula vingine ambavyoo vimezalishwa na wananchi wenyewe umepungua sana baada ya kipindi cha ujamaa kuisha.

Nusu ya wale waliopata upungufu wa uzalishaji wa mazao walidai kuwa ilisababishwa na mvua kidogo na zisizofuata mpangilio, jambo linalohusishwa na mabadiliko katika hali ya hewa. Sababu nyingine ni kupungua kwa rutuba katika ardhi (37%); mbinu duni za kilimo hasa zana duni ya jembe la mkono (10%). Hata hivyo, wahojiwa wachache tu walitoa sababu ya kuttotumia mbolea za kemikali / chumvi chumvi au mbolea ya samadi. Kwa upande mwingine wale waliopata ongezeko la mavuno walitaja sababu ya matumizi makubwa zaidi ya mbolea ya samadi, na matumizi zaidi ya pembejeo na nguvu kazi katika mashamba. Jedwali 1 linaonyesha kugota kwa matumizi ya pembejeo za kilimo kati ya 1989-90 na 2008-09. Matumizi ya mbegu bora yameongezeka kuttoka 36% hadi 58%, lakini matumizi ya mbolea za kemikali yameshuka kutoka 22% hadi 5% katika kipindi hicho. Matumizi ya mbolea ya samadi yamebaki chini na chini ya 30% ya wahojiwa waliitumia katika mashamba. Wakulima wengi hawatumii pembejeo za kilimo katika mashamba yao, na hili ni chanzo cha udongo kuharibika taratibu kwa upungufu wa madini. Kwa kawaida mabaki ya majani baada ya mavuno huachwa shambani, na hii hupunguza upotevu wa madini katika udongo ambao ungetokea iwapo mashamba yangesafishwa na kuachwa tupu. Kwa ujumla hakukuwa taofauti za msingi za mabadiliko ya tija kati ya vijiji vilivyofanyiwa utafiti.

Jedwali 1. Matumizi ya pembejeo za kilimo kati ya wahojiwa katika kipindi cha 1989-90 (Sendaro 1992: tables 10.5, table 10.6) na 2008-09 .

Pembejeo	% of respondents who used in 1989-1990	% of respondents who used in 2008-2009
Mbegu bora	36	58
Mbolea ya kemikali	22	5
Samadi	28	27
Madawa ya kulimia	4	7
Madawa ya kuhifadhia	49	51
Trekta	12	7
Plau (ng'ombe wa)	0	1
Jembe la mkono	100	96

Mifugo

Ufugaji unaambatana sana na makabila. Wakulima wa mazao wachache sana wana mifugo ya ng'ombe au mbuzi, wakati sehemu kubwa ya mifugo hii inamilikiwa na wafugaji wa Mindu Tulieni. Katika majadiliano na wazee wa vijiji, hali ya kubaki katika kilimo cha mazao badala ya kufuga ilisababishwa ba ukosefu wa fedha za kununulia mifugo; hofu ya wizi, na ukosefu wa nguvu kazi. Katika vijiji vyote, 22% ya wahojiwa walimiliki ngombe; mbuzi (17%), kondoo (4%) na nguruwe (2%). 69% ya wohojiwa walimiliki kuku; bata (8%), lakini idadi ya ndege katika kaya kwa kawaida ilikuwa chini ya 10. Lakini kule Mindu Tulieni, 86% ya wahojiwa walimiliki ngombe, wakati kule Lugoba, Makombe na Msoga 5% tu walikuwa na ng'ombe. Vile vile, 52% kule Mindu Tulieni walimiliki mbuzi, ambapo 8% tu walikuwa na mbuzi katika vijiji vingine. Inaonekana kwa hakuna ushirikiano mzuri kati ya makundi ya wafugaji na ya wakulima wa mazao, kiasi kuwa samadi haitumiki mashambani. Wakulima hutoa maelezo kuwa usafirishaji wa samadi ni gharama na huhitaji nguvu nyingi; upatikanaji wake ni mgumu kwa kuwa mifugo haiwekwi mahali pamoja, na kuwa si utamaduni wao. Wengine wanaamini kuwa samadi itaharibu udongo. Kwa upande mwingine, wafugaji wanadai kuwa wako tayari kuwapa bure wanaohitaji samadi. Pia kituo cha vetenari cha Lunga kimekuwa kinagawa samadi bure kwa wakulima.

Katika miongo ya karibuni, magonjwa ya mifugo hasa East Coast Fever (ECF, theileriosis), kichomi, tuberculosis na brucellosis vifo vya wanyama wengi katika eneo hili. Hali ilikuwa mbaya zaidi mwanzoni mwa miaka ya themanini ambapo serikali haikuweza tena kuhudumia majosho ya kuoshea mifugo. Uhaba na bei ghali ya dawa za acaricides na trypanicides vilisabisha dawa kupunguzwa nguvu na wafanya biashara wabovu. Hali ilikuwa mbaya zaidi kutokana na uhaba wa malisho, kiasi kuwa wafugaji hawaj´kuepuka tena maeneo yalikuwa hatari kwa mifugo kutokana na wadudu waenezao maradhi ya mifugo kama vile kupe (Giblin 1990). Karibu wafugaji wote waliohojiwa mwaka wa 2008-09 walilalamika kuwa wamepoteza idadi kubwa ya mifugo. Maafisa mifugo walikadiria kuwa maelfu ya mifugo yalipotea kutokana na ECF katika kata ya Lugoba peke yake. Kwa kuwa ECF haiathiri wanyama wengine zaidi ya ng'ombe inaeleza wazi sababu ya kuongeka kwa mbuzi na kondoo kwa kasi kubwa katika miaka 30 iliyopita (Hurskainen 1984: table 6, Lugoba Ward Office 2008).

Kadiri ya takwimu za kata, idadi ya mifugo imedumaa pale pale, mifugo 16321 mwaka 1973 na 15354 mwaka 2008 (Hurskainen 1984: table 6, Lugoba Ward Office 2008). Idadi ya wafugaji katika eneo hili imeongezeka mara tatu katika kipindi hicho hicho (Vuorela 1987: app. Table 1, Lugoba

Ward Office 2006), ikionyesha kupungua kwa wastani wa ardhi kwa kila kaya. Kule Mindu Tulieni ng'ombe walipungua kutoka wanyama 93 kwa kila kaya mwaka 1977 hadi chini kiasi cha wanyama 30 mwaka 2009 (Mustafa 1989: 111, Taarifa kutoka kwa Afisa Mifugo wa Lugoba 2009). Muundo wa umiliki wa mifugo huonyesha tofauti kubwa kati ya wafugaji kama invyoonyeshwa katika jedwali 2. Idadi ya mifugo inayomalikiwa na wafugaji wachache (wenye wanyama zaidi ya 100) imebaki juu, lakini mifugo yao pia imepungua tangu mwaka 1977. Kiasi cha mifugo katika kaya maskini zenye wanyama chini ya 50 imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Lakini, takwimu hizi hasa za mwaka 1977 zaweza kuegemea upande mmoja zaidi kwa kuwa chanzo cha takwimu kilitokana na sample ndogo (n=23).

Jedwali 2. Mgawanyo wa mifugo ya ng'ombe kati wa wafugaji wa kijiji cha Mindu Tulieni mwaka 1977 (n=23) na 2009 (n=166) (Mustafa 1986: 111, table 3, data from Lugoba Veterinary Officer 2009).

Kipengele	Kundi la matajiri > 100 ng'ombe	Kundi la kati 50-100 ng'ombe	Kundi la maskini < 50 ng'ombe
1977: kaya	26 %	22 %	52 %
1977: ng'ombe	62 %	21 %	18 %
2009:Kaya	7 %	11 %	83 %
2009: ng'ombe	44 %	25 %	31 %

Huduma za ugani

Kuna maafisa ugani watatu na afisa wa mifugo mmoja wanaofanya kazi katika kata ya Lugoba. Mmoja kati wa wahojiwa watatu walikiri kupokea huduma ya ushauri kutoka kwa maafisa hawa, na waliobaki hawapata mawasiliano yoyote na maafisa hao. Hali ilikuwa mbaya zaidi katika kijiji cha Makombe ambako wawili kati ya wahojiwa ishirini walishughulika na maafisa hao. Ushauri mkubwa uliopokelewa kutoka kwa washauri ulihusu mbegu. Ushauri kwa wakulima ulihusu udhibiti wa wadudu na madawa ya wadudu. Ushauri juu ya matumizi ya mbolea za kemikali na samadi ilitajwa na wakulima wachache tu. Wafugaji walipokea ushauri juu ya chanjo na matibabu ya magonjwa ya mifugo. Isipokuwa kwa matukio machache, wakulima hawakupokea msaada kwa njia ya kupewa madawa ya kilimo, mbegu au huduma za mifugo bila malipo. Kadiri ya Sokoni (2008), gharama za huduma za ugani ni jukumu la serikali, lakini hivi sasa ushiriki wa sekta binafsi unasisitizwa. Huduma ya ugani na usambazaji wa pembejeo ambavyo awali vilitolewa na maafisa ugani, sasa zimetengenishwa, sio jukumu tena la maafisa ugani kusambaza pembejeo sambamba na kutoa ushauri. Maafisa ugani wa kata ya Lugoba wamelalamika

juu ya ukosefu wa raslimali na vitendea kazi. Kwa mfano, wanalazimika kulipia wenyewe gharama za usafiri wakiwa kazini. Hali hii hupunguza idadi ya safari za kuwatembelea wakulima walioko sehemu za pembezoni kwa mfano kijiji cha Makombe. Pia wamekatishwa tamaa na kuchanganywa na uwezo mdogo wa wakulima wa kuboresha tija. Wakati huo huo baadhi ya wakulima wanadai kuwa wataalamu wa kilimo wanapenda kuwahudumia wakulima wakubwa wachache wenye uwezo wa kumudu pembejeo za kisasa.Kwa upande mwingine, wakulima wengi walisema kuwa wanapokea ushauri mzuri kutoka kwa maafisa kilimo ambao umewasaidia kuongeza kupata mazao bora na mengi zaidi.

Vyanzo vya chakula kiuzwacho

Aina ya vyakula vinavyouzwa katika eneo la utafiti imeongezeka sana katika kipindi cha miaka thelathini iliyopita. Kadiri ya utafiti uliofanyika mwaka 1979, aina 28 za vyakula zilikuwa zinauzwa na wafanya biashara 20 wa soko la Lunga. Aina zilizonyingi za vyakula hazikuwa zimepia katika matayarisho yo yote, kwa mfano vyakula vya kawaida: mihogo, maharage, matunda na mbogamboga. Vingine vilivyokuwepo ni unga wa mahindi na wa ngano, samaki waliokaushwa, nyama, sukari, chumvi, korosho na chai. Hata hivyo mahindi yaliuzwa na mfanya biashara mmoja tu. Vyakula hivi vilikuwa vimezalishwa kutoka katika mikoa jirani, isipokuwa baadhi ya viungo na maziwa ya unga ya watoto, ambavyo viliagizwa kutoka nje ya nchi.

Vuorela (1987: 218) anaandika kuwa mwaka 1984 mabanda ya biashara pale Msoga yaliuza samaki waliokaushwa, karanga, ndizi, mikate, nyanya, na wakati mwingine matunda ya msimu kama maembe, miwa na mapapai. Vijiji vya Makombe na Mindu Tulieni havikuwa na wafanya biashara wa vyakula wakati huo, na kwa hiyo watu wake walinunua vyakula pale Lunga. Wakati wa uhaba wa chakula katika masoko ya vijiji wananchi walisafiri hadi Chalinze, Bagamoyo au Dar es Salaam kununua vyakula. Ni wazi kuwa sehemu kubwa ya vyakula vilivyotumika katika vijiji, vilizalishwa na wanavijiji wenyewe. Biashara na kubadilishana bidhaa na kupeana chakula kati ya kaya na kaya vilikuwa jambo la kawaida.

Mwaka 2008-09, kulikuwa zaidi ya vibanda vya sokoni na mitaani 120 vilivyotumika Lunga; Msoga 7; na Makombe 11. Wafanya biashara kwa kutembeza walitembelea vitongoji mbali mbali vya Mindu Tulieni, lakini kijiji hakikuwa na maduka ya kudumu. Katika kijiji cha Lunga kiasi cha aina za vyakula 70 zilipatikana. Ukihesabia na vyakula vilivyotengenezwa viwandani, aina za vyakula huongezeka hadi kufikia zaidi ya 100. Vyakula vingi vya kawaida vilipatikana pia katika vijiji vya Msoga na Makombe. Kadiri ya

kahojiano, upungufu mkubwa wa vyakula vikuu haukuwahi kutokea miaka ya katika ya themanini. Wafanyabiashara wanapata sehemu kubwa ya vyakula wanavyouza kutoka kwa wafanya biashara wa jumla na maduka makubwa ya Chalinze na Dar es Salaam. Baadhi ya mahojiano na wafanyabiashara ya jumla na wauza maduka, bidhaa inayouzika zaidi ni unga wa mahindi, maharage mekundu, sukari, na mafuta ya kupikia. Vyakula vingine vya kawaida ni aina zingine za maharage, mchele, unga wa ngano, samaki wakavu, vitunguu, chumvi, na mboga mboga kama nyanya, mchicha, na spinachi. Sehemu kubwa ya bidhaa za chakula bado huzalishwa nchini Tanzania, maeneo ya kati na kaskazini mashariki. Hata hivyo, sehemu kubwa ya ngano inayouzwa inaletwa kutoka masoko ya dunia kwa kuwauzalishaji wa ngano katika Tanzania hukidhi sehemu ndogo tu ya mahitaji. Bidhaa za vyakula zinazoletwa kutoka nje kwa kiasi kikubwa ni zile za viwandani kama mafuta ya kupikia, hamila, tomato paste, viungo, juisi, peremende, na biskuti. Mara nyingi bidhaa hizi hutoka Afrika ya Kusini, Kenya, Uarabuni na wakati mwingine India na Ulaya. Mafuta ya nazi mara nyingi huagizwa kutoka Malaysia. Indonesia, au Argentina, na kutengenezwa na kampuni za Tanzania zilizoko Dar es Salaam.

Wauzaji wa mahindi walikadiria kuwa chini ya 20% ya mahindi wanayouza huzalishwa katika kata za Lugoba na Msata. Sehemu kubwa ya mahindi inazalishwa mkoani Dodoma na kwa msimu kutoka mikoa ya Manyara, Arusha, Iringa, Tanga, Mbeya, Ruvuma au Morogoro. Katika miongo miwili iliyopita, Tanzania imezidi kutegemea mahindi ya kuagiza kutoka soko la dunia, lakini haya huchangia chini ya 10 % ya mahindi yanayotumika nchini (Sarris & Mantzou 2005: table 2, FAOSTAT 2010). Mchele hasa hutoka mikoa ya Morogoro na Mbeya. Kunde, mbaazi, choroko na mihogo vinazalishwa katika kata ya Lugoba na vijiji vya karibu. Maharage huletwa kutoka mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Iringa na Tanga. Bidhaa zinazoharibika haraka kama matunda na mbogamboga huletwa kutoka maeneo ya karibu zaidi kuliko nafaka na maharage. Mazao haya hulimwa katika eneo la utafiti na wakati mwingine huletwa kutoka mkoa jirani wa Tanga. Nyama inayouzwa hapa inatokana na wanyama waliofugwa na wananchi wa kata ya Lugoba. Mayai na kuku vinaletwa kutoka shamba la kuzalisha kuku la Msata. Samaki wakavu huuzwa misimu yote ya mwaka. Kwa kawaida samaki wabichi hawauzwi kwa sababu wavuvi na wafanyabiashara wa samaki wa Bagamoyo, Sadani na Tanga pembezoni mwa bahari ya Hindi hawana majokofu na usafirishaji wa samaki kutoka maeneo mengine ya Mwanzana Bukoba kando ya Ziwa Victoria ni ghali.

Maendeleo ya Uhakika wa Chakula

Ugali ni chakula kikuu na kinacholiwa na wengi katika eneo hili, ambao kaya za wahojiwa wote hula mara moja au mara mbili kwa siku. Ugali huliwa na maharage, mboga za majani na wakati mwingine samaki au nyama, chapati au mkate. Ulaji huu umedumu kati ya wakulima na utafiti huu umethibitisha kuwa wafugaji pia wamebadili chakula chao cha kijadi kilichotokana na mifugo na kutumia zaidi kile cha wakulima. Asilimia 73 ya wahojiwa hula milo mitatu kwa siku; na 25% hula milo miwili kwa siku. Wengi wa wanaokula milo miwili kwa siku hukosa chakula cha asubuhi, lakini walikuwepo pia waliokosa chakula cha mchana na cha jioni. Kaya mbili kati ya zilizohojiwa, moja ya Lunga na nyingine ya Msoga hula mlo mmoja kwa siku.

Asilimia 19 ya wahojiwa walijibu kuwa wanakula zaidi mazao ya mifugo kuliko miaka ya katikati ya themanini wakati wengiwao (55%) walidai kuwa wanakula kidogo zaidi mazao yatokanayo na mifugo, kama nyama na maziwa. Kwa wastani kaya zilizohojiwa hula nyama mara nne kwa mwezi. Wengine 29% walikula nyama mara moja au mbili kwa wiki; zaidi ya mara mbili kwa mwezi (11%), mara moja au chini yake (34%) na hawana uwezo wa kula nyama (7%). Kufikia Julai 2009 bei ya nyama ilipanda zaidi kufikia shilingi 4000 kwa kilo. Bei ya nyama ya mbuzi na kondoo ilikuwa kubwa zaidi, shilingi 5000 kwa kilo. Kwa kulinganisha, naharage yanagharimu shilingi 1000 hadi 1200 kwa kilo. Inashangaza kuwa ulaji wa nyama haukutofautiana sana kati ya wafugaji na wakulima. Kwa ujumla samaki huliwa mara nyingi zaidi ya nyama, karibu zaidi ya mara moja kwa wiki kwa wastani. Nusu ya wahojiwa walisema kaya zao hula samaki angalau mara moja kwa wiki. Asilimia 62 wanakunywa maziwa angalau mara mbili kwa wiki. Ulaji wa mayai likuwa chini kutokana na bei kubwa na uzalishaji mdogo kutoka kuku wa kieneyeji. Kaya nyingi zilikula matunda na kunywa chai kati ya milo.

Theluthi mbili ya kaya za wahojiwa zimewahi kuwa na vipindi vya uhaba wa chakula na kiasi cha 63% walikosa baadhi ya milo katika miezi 12 iliyopita kwa sababu ya kukosekana kwa chakula. 27% ya wahojiwa walidai kuwa chakula wanachoweza kukipata hakitosheleza n´mahitaji ya kaya zao. Kutokana na mazoezi ya kutengeneza kalenda ya misimu na majibu ya dodoso, uhaba wa chakula ulikuwa katika miezi ya Aprili hadi Julai, kabla ya mavuno, wakati ambapo chakula kilichozalishwa na wenyeji kilikuwa kidogo. Baada ya kuvuna mazao ya masika mwezi Julai hadi Agosti, hali ya chakula inakuwa bora zaidi. Hata upungufu wa chakula hujitokeza mwezi wa Oktoba. Hii inaonyesha kuwa kipindi ambacho kaya zinatumia chakula walichozalisha wenyewe ni cha miezi michache tu katika mwaka. Wahojiwa hawakuonyesha kuwa mavuno yanatokana na kilimo cha vuli cha Januari – Februari yanaweza

kuongeza uhakika wa chakula, kwa kuwa mazao huwa kidogo sana na uzalishaji kufeli ni kawaida. Muhimu zaidi, walihusisha uhakika wa chakula na upatikanaji wa chakula walicholima wao wenyewe. Kutegemea chakula cha kununua sokoni ulitazamwa kuwa chanzo cha upungufu na ukosefu wa uhakika wa chakula.

Kati ya kaya zilizokuwa na usamala mdogo wa chakula, zilivuka kipindi cha shida ya chakula kwa njia ya kuuza nguvu kazi yao katika kazi (68%) kama ya kuchoma mkaa, kazi ya kubeba mizigo na vibarua vingine. Njia nyingine ni ile ya kukopa au kuomba msaada kutoka kwa ndugu, jamaa, marafiki au wenye maduka (55%), na kupokea mssada wa chakula toka serikalini (28%). Maafisa wa serikali kutoka eneo hili wameomba msaada wa chakula toka serikalini kwa miaka kadhaa, hata miaka ya elfu mbili (2000s). Lakini kiasi kilichotolewa na serikali wakati wa shida ya chakula kwa kawaida kilikuwa kilo kadhaa za mahindi na wa pengine maharage. Wengi wao waliopokea wamedai kuwa kiasi cha chakula kilikuwa kidogo mno kuwawezesha kujikimu kwa siku chache. Wahojiwa wengine walitumia njia ya kuuza mifugo na mali zingine (16%) na wengine walipunguza kiasi cha chakula na idadi ya milo waliyokula (10%). Wachache walitemegea kula mizizi na matunda ya porini wakati wa shida ya chakula., lakini njia hii ni haiwezekani siku hizi kwa kuwa upatikanaji wa mimea inayoliwa umepungua.

Jedwali 3 linaonyesha sehemu ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano wenye kipimo cha weight-for-age, chini ya 80% ya kiwango cha kawaida (yaani wenye uzito pungufu) kama kilichorekodiwa katika Kituo cha Afya cha Lugoba. Takwimu ya kutosha zilikuwepo Lunga, Makombe na Mindu Tulieni, lakini Msoga haikuwanazo. Kutokana na tofauti ya idadi ya watoto waliopimwa kwa mwaka, taarifa ziliunganishwa kwa makundi ya miaka ya 1997-1999 na 2007-09, ambapo wastani kiasi cha watoto wenye uzito mdogo ilikuwa 16% na 14% kwa kufuta mpangilio huo. Kijiji cha Mindu Tulieni kilikuwa na sehemu ndogo zaidi ya watoto wenye uzito mdogo, katika vipindi vyote vya 1997-1999 na 2007-2009. Hii inaonyesha kuwa hali ya chakula ilikuwa bora zaidi kati ya wafugaji. Unywaji wa maziwa ni mkubwa kwa wachungaji kuliko kwenye makundi mengine.

Jedwali 3. Sehemu ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano wenye weight-for-age index chini ya 80 % ya uzito wa kawaida kipindi cha 1997-99 na 2007-09 (Takwimu kutoka Kituo cha Afya cha Lugoba mwaka 2009 na 2010).

Kijiji	1997-1999			2007-2009		
	n	< 80 %	% uzito pungufu	n	< 80 %	% uzito pungufu
Lunga	1442	226	15.7	360	53	14.7
Makombe	161	38	23.6	104	14	13.4
Mindu Tulieni	170	22	12.9	82	8	9.8
TOTAL	1773	286	16.1	546	75	13.7

Matokeo ya uchambuzi yanaonyesha kuwa magonjwa yamayoambatana na lishe duni hayatambuliwi na kaya zilizohojiwa. Asilimia 15 tu ya wahojiwa walisema kuwa angalau mtu mmoja katika kaya iliugua magonjwa ya aina hiyo katika miaka 25 iliyopita. Magonjwa yaliyotajwa na wengi zaidi ni magonjwa kuwashwa ngozi, upungufu wa damu na kuharisha. Utafiti uliofanywa na Mwanri et al. (2000) katika shule tatu za msingi katika wilaya ya Bagamoyo, 70% ya watoto walikuwa na upungufu wa damu. Katika utafiti wangu huu, unyafuzi ulitajwa na kaya tatu tu kati ya zote zilizohojiwa na hakuna iliyokuwa na nyongea, ambapo taarifa hii inalingana na takwimu kutoka Kituo cha Afya cha Lugoba. Hapo inaonyesha kuwa upungufu mkubwa wa lishe ulikuwa umepungua, lakini kukosekana kwa virutubisho imeendelea kuwa tatizo kwa wengi. Maafisa wa afya, waganga wa jadi, maafisa kilimo na waalimu wanaona kuwa hali ya lishe ya watu wa eneo hili imeboreka baada ya mwisho wa kipindi cha ujamaa. Pia picha kadhaa za mnato zilizopigwa na Taimi Sitari mwaka 1978-79 pale Lunga na vijiji vingine zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya watoto walikuwa na matumbo makubwa, dalili tosha ya utapiamlo, kitu ambacho kilikuwa nadra mwaka 2008-09. Hitimisho kutokana na uchambuzi huu ni kuwa hali ya lishe imeboreshwa tangu miaka ya katikati ya themanini, ingawa hali bado ni mbaya katika familia nyingi, na inaweza kuwa mbaya zaidi iwapo uzalishaji wa mazao utazorota, mifugo itapotea, wanakaya watakufa, bei ya vyakula itapanda na matukio mengine.

Utumiaji wa chakula na mabadiliko ya chuma riziki

Wahojiwa wengi zaidi (83%) walionyesha kuwa kiasi cha chakula kinachonunuliwa na kaya kimeongezeka sana au kwa kiasi tangu 1985.

Walikadiria kuwa mwaka 1985 karibu robo ya chakula chota kilichotumika kilinunuliwa, ambapo sehemu hii iliongezeka kuwa zaidi ya nusu mwaka 2008-09. Robo tatu ya wahojiwa walisema kuwa walibadilishana vyakula na vijiji vingine miaka ya katika ya themanini (1980s). Nusu ya wahojiwa bado wanafanya hivyo, lakini kiasi cha chakula kinachobadilishwa kimepungua sana.

Kipato cha wastani cha kila siku ni shilingi 6070 kwa kaya na 1165 kwa kichwa. Wahojiwa wa dodoso wengi walitumia sehemu kubwa ya mapato yao katika kununua chakula. Kwa wastani walitumia 62% ya mapato katika kununua chakula au shilingi 686 kwa siku kwa kichwa. Kuongezeka kwa bei ya vyakula, kufuatia matatizo ya bei duniani ya mwaka 2007-8 ambapo bei ya mahindi katika soko la Dar es Salaam iliongezeka maradufu (USAID 2008), ilikuwa tatizo la wengi. Katika kijiji cha Makombe bei kubwa ya maji iliongeza matumizi katika kaya. Tofauti na vijiji vingine, mfumo wa maji ya bomba katika kijiji cha Makombe haufanyi kazi, na maji yanayoletwa kijijini yanagharimu shilingi 400 hadi 500 kwa ujazo wa lita 20. Wahojiwa wengi katika kijiji hiki walisema kuwa wanatumia maji yasiyo ya bomba wanapokosa fedha au uwezekano wa kuleta maji toka mabomba yaliyoko mbali. Katika vijiji vingine, upatikanaji wa maji ya bomba umeboreka baada ya kujengewa mabomba yanayoleta maji kutoka mtambo wa kusafisha maji ulioko kando kando yam to Wami kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Zaidi ya gharama za chakula, mahitaji ya fedha yanaongezeka kwa ajili ya ada ya shule, mavazi, usafiri, nyumba, pembejeo za kilimo, vifaa vya kufanyia biashara, umeme na mahitaji mengine ya lazima. Hali hii inahusika na mabadiliko ya hali ya mpangilio wa maisha, ambao umewahusisha zaidi wananchi katika mfumo wa uchumi wa fedha. Katika utafiti wa 1989-90 wahojiwa walitakiwa kueleza shughuli za wanakaya wakati wa kuanzisha vijiji vya ujamaa hasa mwaka 1975. Sendaro (1992: 156-159, table 10.3) alichanbua taarifa hizo na kuhitimisha kuwa sehemu ya watu wote iliyojishughulisha na kilimo (ukijuisha wazee na watoto) ilipungua kutoka 75% wakti wa kuunda vijiji hadi 57% mwaka 1989-90. Anaeleza kuwa badiliko hili linatokana na vijana wachache zaidi kujihusisha na shughuli ya kilimo wakiwapokea wakulima waliozeeka. Sababu nyingine ni ongezeko la uandikishwaji wa wanafunzi mashuleni.

Kadiri ya uchambuzi wa dodoso lililotolewa mwaka 2008-09, sehemu ya watu wanaoshughulika na kilimo, wakati wote au kwa vipindi, imepungua hadi 43%. Zaidi ya theluthi mbili (71%) za kaya zina wanakaya mmoja au wawili wanajipatia mapato kwa njia zisizo za kilimo, na nia kubwa zaidi ni biashara ndogo ndogo (24%), kupokea pesa toka mahali pengine (24%), uzalishaji wa mkaa (11%), ajira katika miradi ya kutengeneza kokoto (11%),

kutengeneza matofali (5%), ajira serikalini (5%) na kutengeneza pombe (4%). Tukivilinganisha vijiji, ushirika wa kaya katika shughuli zisizo za kilimo ni mdogo zaidi Mindu Tulieni na Msoga, ambako viwango na ni 52% na 62% Katika vijiji vya Lunga na Makombe kiwango ni juu zaidi, 80%. Hii inahusiana na mahali Lunga ilipo pembezoni mwa barabara kuu, hali inayotoa fursa ya biashara ndogo ndogo. Makombe pia iko karibu na mradi ya uchimbaji wa kokoto. Kama inavyoelezwa na Ylhäisi na Mhache katika ripoti hii; wananchi wanajishughulisha na kazi ya kuchoma mkaa kuliko inavyoonyeshwa na wahojiwa katika utafiti wangu, kwa kuwa shughuli hii hufanyika nje ya taratibu halali.

Hitimisho na Matazamio

Katika kipindi kilichofuata baada ya kuachana na ujamaa, soko la kilimo lilifanywa huru. Hii iliambatana na serikali kujitoa kutoka katika udhibiti was uzalishaji wa mazao; kuvunjika kwa mfumo wa ushirika, na kuachwa kwa mfumo wa bei za kikanda. Kutokana na hayo, kilimo cha mazao ya biashara, hasa pamba kilikoma katika eneo hili. Uzalishaji wa mazao ya chakula pia ulipungua kufuatia kuongeza kilimo cha kukaakaa, kuendelea kukosa matumizi ya pembejeo; ubadilikajibadilika wa mvua kwa mwaka; na kuongezeka kwa fursa za chuma riziki katika sekta zingine. Vile vile, uzalishaji wa mifugo ulidoda au kushuka sababu ya magonjwa yaliyosababisha upotevu wa ng'ombe.

Kumetokea uhamaji kutoka hali ya kutegemea chakula walichokizalisha kuelekea matumizi ya chakula kinachonunuliwa sokoni. Nafasi ya mfumo wa chakula, ambayo wananchi wa eneo la Lugoba wanaitegemea, imeendelea kuunganishwa na ngazi za mkoa, taifa na kwa kiasi kidogo ya kimataifa. Kiasi kidogo tu cha chakula sasa huzalishwa pale Lugoba na walaji wenyewe. Pia watu wanauza mazao yao kidogo kutokana na uzalishaji mdoogo na ushindani mkubwa katika soko. Sehemu kubwa ya chakula kinacholiwa katika vijiji sasa inazalishwa mahali pengine Tanzania, hasa katikati na kaskazini mashariki mwa nchi. Hata hivyo, chakula chenye asili ya nje ni cha nadra katika eneo hili, na kinajumuisha vyakula vya kiwandani, ngano na kiasi kidogo cha mazao yanayoagizwa toka nje wakati wa uhaba.

Gharama ya maisha ya kaya zilizohojiwa zimepanda tangu miaka ya katikati ya themanini, kwa sababu fedha zaidi huhitajika kwa ajili ya kununua chakula, huduma za msingi kama afya na elimu pamoja na bidhaa za vivutio zilizoanza kuingia katika masoko ya vijijini. Zaidi ya kukua kwa sekta ya huduma na biashara ndogo ndogo, uchomaji wa mkaa umepata kuwa chanzo

muhimu cha mapato. Na hivyo kuchangia kupotea kwa misitu kwa haraka na katika maeneo makubwa zaidi. Mabadiliko ya umbile la mfumo wa chakula vijijini yanahusiana na mabaliko ya demografia, uongozi wa kisiasa; desturi za kitamaduni; chuma riziki; mfumo wa matumizi ya ardhi na mazingira. Japo mabadiliko haya ni makubwa na yenye changamani, kaya zimeweka kudumisha kiwango cha msingi cha uhakika wa chakula. Inaonekana kuwa hali ya lishe taratibu imeboreka miongo michache ya karibuni.

Hata hivyo, uendelevu wa muda mrefu wa maendeleo haya unatia wasiwasi. Kwanza hali ya uhakika wa chakula katika eneo hili unaendelea kuwa dhaifu. Karibu wahojiwa wote hutumia sehemu kubwa ya mapato yao katika chakula, na theluthi mbili wanalazimika wakati fulani kukosa milo. Pili, mabadiliko katika mfumo wa chakula yana uhusiano uharibu wa mazingira ulio wa kuzunguka. Kupungua kwa tija na rutuba ulioonyeshwa na mahojiano unahusiana wakulima kutoweza kuchukua na kutumia mbinu za kilimo zilizoendelevu na kuzingatia uwiano katika kuondoa madini yaliyoko udongoni. Matumizi ya mbinu za kijadi katika mashamba ya kudumu na kutokuhamisha mashamba kwenda sehemu mpya, kuondoshwa madini na kutoyarejesha kwa njia ya kutumia mbolea hai kwa mfano samadi, bila shaka kutaleta upotevu wa rutuba týa udongo. Kadiri ya mahojiano, wakulima wengi wanaamini kuwa udongo una rutuba na hakuna manufaa ya kutumia samadi. Wanadai kuwa kutopatikana mvua ya kutosha ndio sababu pekee inayosababisha mavuno hafifu. Zaidi ya hayo, familia nyingi zimekuwa zikinakula misitu kwa njia ya kuchoma mkaa ili kupata pesa na kujipa uhakika wa chakula. Tatu, uwezekano wa kutawanya vyanzo vya mapato unakikomo kutokana na kiwango duni cha elimu; ukosefu wa raslimali kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa kilimo na kukosekana kwa mikopo kwa ajuli ya kupanua miradi midogo hasa kwa ajili ya familia maskini.

Mipango kwa ajili kuingilia kati hapo baadaye, kwa mfano kupitia programu ya Kilimo Kwanza, sharti itambue kuwa vikwazo vya maendeleo ya mfumo wa chakula vijijini sio tu unatokana na kukosekana kwa raslimali za kuboresha kilimo kwa wakulima, bali mambo muhimu yanayotokea tamaduni za kijadi zinapokutana na usasa. Urasmishaji wa ardhi ilikuwawezesha wakulima kupokea mikopo unaweza kuongeza uwekezaji katika kilimo, lakini jambo hili huendana na hatari zinazotakiwa kuzingatiwa kwa kuwa mikopo na madeni imehusishwa na kujiua kwa wakulima kule India na mahali pengine (e.g. Gill & Singh 2006, Patel 2007: 50, 64—65). Hali hii pia hupunguza kilimo cha mzunguko wa mashamba na kuzidisha uharibifu wa ardhi iwapo madini yanayotolewa ardhini hayarudishiwi. Mbadala wa pembejeo za kemikali ambazo ni gharama, msisitizo uwekwe zaidi katika matumizi ya mbolea hai kama mavi ya ng'ombe, mboji na kuweka matandazo ya majani.

Kwa upande mwingine, ukubwa wa mashamba katika eneo la utafiti unaweza mdogo mno kwa ajili ya kufanya kilimo kuwa cha kisasa kwa mkulima binafsi. Kwa kuzingatia hili, kurudisha mashamba ya pamoja na bega kwa began a matumizi kwa pamoja ya mashine kama trekta vilipendekezwa na baadhi ya wahojiwa. Vile vile, baadhi ya wafugaji walipendekeza kurudishwa kwa ushirka wa wafugaji. Inaweza kuzingatiwa zaidi mtawanyo endelevu wa chuma riziki na mipango ya muda mrefu ya maendeleo vijijini.

Machapisho

Bryceson, D.F. (1993). Liberalizing Tanzania's Food Trade: The Public and Private Faces of Urban Marketing Policy, 1939-88. 320 p. James Currey.

FAOSTAT (2010). FAOSTAT. Food and Agriculture Organization of the United Nations, Rome. Accessed 22.9.2010. <http://faostat.fao.org>

Giblin, J.L. (1990). East Coast Fever in Socio-Historical Context: A Case Study from Tanzania. The International Journal of African Historical Studies, Vol. 23, No. 3, 401—421.

Gill, A. & L. Singh (2008). Farmers' Suicides and Response of Public Policy: Evidence, Diagnosis and Alternatives from Punjab . Economic and Political Weekly June 30, 2006, 2762—2768 . Accessed 23.9.2010. <http://mpra.ub.uni-muenchen.de/146>

Hurskainen, A. (1984). Cattle and culture. The Structure of a pastoral Parakuyo society. Studia Orientalia 56. 311 p. Helsinki.

Kikula, I.S. (1997). Policy implications on environment. The case of villagisation in Tanzania. 214 p. The Nordic Africa Institute, Uppsala.

Lugoba Ward Office (2006). Takwimu za watu kata Lugoba 2006.

Lugoba Ward Office (2008). Taarifa ya utekelezaji wa kazi za kilimo/mifugo kata ya Lugoba. 21.10.2008.

Mustafa, K. (1989). Participatory research and the "pastoralist question" in Tanzania: a critique of the Jipemoyo Project experience in Bagamoyo district. Development and culture research 1989, 7. 171 p. Institute of Development Studies, University of Helsinki. Yliopistopaino, Helsinki.

Mwanri, L., A. Worsley, P. Ryan & J. Masika (2000). Supplemental Vitamin A Improves Anemia and Growth in Anemic School Children in Tanzania. The Journal of Nutrition 30, 2691—2696.

Patel, R. (2007). Stuffed and Starved. Markets, Power and the Hidden Battle for the World's Food System. 418 p. Portobello Books, London.

Ponte, S. (1998). Fast Crops, Fast Cash: Market Liberalization and Rural Livelihoods in Songea and Morogoro Districts, Tanzania. Canadian Journal of African Studies / Revue Canadienne des Études Africaines, Vol. 32, No. 2.

Ponte, S. (2002). Farmers & markets in Tanzania. How policy reforms affect rural livelihoods in Africa. 197 p. Mkuki na nyota, Dar es Salaam.

Sendaro, A.M. (1992). Technical stagnation, ageing population and agricultural production in Tanzania: The case of Lugoba, Msata and Mboga villages in Bagamoyo District. In Forster, P.G. & S. Maghimbi (eds.) The Tanzanian Peasantry: Economy in Crisis. 151—168. Avebury, Aldershot.

Sokoni, C.H. (2008). Commercialisation of smallholder production in Tanzania: implications for sustainable resources management. Geographical Journal Vol. 174, No. 2, 149—175.

TMA (2010). Bagamoyo Total Monthly Rainfall (mm) 1964-2007. Data collected from Tanzania Meteorological Agency, Dar es Salaam.

USAID (2008). Tanzania Food Security Update. May/June 2008. Famine Early Warning Systems Network. Accessed 22.9.2010. <http://www.fews.net/docs/Publications/tanzania_2008_05_final.pdf>

Vuorela, U. (1987). The Women' question and the modes of human reproduction. An analysis of a Tanzanian village. Transactions of the Finnish Anthropological Society No 20. 234 p.

UHUSIANO WA MIJI NA VIJIJI NA MCHANGO WAKE KATIKA MAENDELEO VIJIJINI

Cosmas H. Sokoni, Idara ya Jiografia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Utangulizi

Miji na vijiji vina mahusiano ya karibu sana. Hakuna miji bila vijiji. Tunaitambua miji kwa kulinganisha na vijiji. Uhusiano kati ya miji na vijiji ni mada iliyowavutia wengi kisiasa, kimaendeleo na kiutafiti. Mitazamo tofauti juu ya uhusiano wa miji na vijiji imejitokeza, na hapa inaelezwa kwa kifupi. Miji yote duniani imekua na kuongezeka kutokana na kutumia raslimali kutoka maeneo ya vijijini yanayoizunguka. Njia rahisi ya kufafanua uhusiano huu ni kwa kuangalia 'mtiririko' wa mali: bidhaa, huduma, teknolojia, fedha, mawazo, n.k. kati ya miji na vijiji (Tacoli, 1998). Tofauti ya mitazamo iko zaidi juu ya miji inachangia vipi maendeleo ya maeneo hayo ya vijijini yanayoizunguka. Mtazamo wa siku nyingi unaona kuwa miji hasa ya nchi zinazoendelea hukua kwa kuchota raslimali toka vijijini, lakini hairudishi rasmali ya kutosha ili kuendeleza vijiji. Mfumo unaojenga maendeleo ya miji ndio unaodidimiza maendeleo vijijini. Mtazamo taofauti na huu unadai kuwa miji ni kichocheo cha maendeleo vijijini. Maendeleo vijijini yanategemea bidhaa na huduma zinazopatikana mjini.

Utafiti huu unalengo la kuchangia katika mjadala huu kwa kuangalia muingiliano kati ya watu wa mjini na vijijini. Umejikita katika uchambuzi wa uhusiano kati ya wanakijiji waliohamia mjini na jamaa zao waliobaki kijiji kwao.

Nadharia juu ya uhusiano wa miji na vijiji

Popote duniani, miji inakua kwa kutumia raslimali kutoka maeneo ya vijijini. Lakini mchango wa miji katika maendeleo ya vijijini hutofautiana. Miji mingi hukua kwa 'kunyonya' vijiji – mfumo wa miji ya kikoloni – raslimali

zinakusanywa kutoka vijijini na kukuletwa mijini tayari kusafirishwa nje ya nchi. Miji ya namna hii haina uchumi imara. Uchumi wake haujajengwa katika viwanda, bali katika kutoa huduma za utawala na biashara. Uchumi wa miji hiyo hautoi msukumo wa uzalishaji katika sekta zilizoko vijijini: uzalishaji mazao, ufugaji, huduma, n.k. Katika hali hii 'mtiririko' wa bidhaa na huduma toka vijijini kwenda mjini hauambatani na mtiririko wa bidhaa na huduma kutoka mjini ambazo ni za msingi wa maendeleo vijijini. Katika hali uhamaji wa watu kutoka vijijini kwenda mjini umetazamwa kuwa unadidimiza maendeleo ya vijijini kwa kuwa unanyang'anya nguvu kazi muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kilimo. Kwa vile uchumi wa miji haujengwa katika viwanda, uhamiaji huu huleta kero katika miji ambako uwezo wa kutoa huduma za msingi unazidiwa na ukuaji kwa kasi wa idadi ya watu. Matokeo yake in ukosefu wa kazi, kukua sekta isiyo rasmi, kukua kwa makazi holela; msongamano, na maovu mbali mbali ya mjini. Kwa kufuata mtizamo huu, sera zililenga kuzuia watu toka vijijini kuhamia mjini: sera ya nguvu kazi; kukuza miji midogo; usambazaji wa maendeleo ya viwanda, n.k. zilijaribu kuzuia uhamiaji mjini, hasa katika jiji la Dar es Salaam. Sera hizi hazikufanikiwa kufikia malengo.

Mtazamo mwingine unathamini mchango wa miji katika maendeleo vijijini kutokana na bidhaa na huduma zinazotolewa. Miji ni soko la bidhaa zinazozalishwa vijijini na pia ni chanzo cha mahitaji ya bidhaa na huduma zinazohitajika vijijini. Mtizamo huu umeleta mabadiliko jinsi uhamiaji wa watu toka vijijini kwenda mjini unavyopokelewa. Mwanakijiji kuhamia mjini haitazamwi tena kama hasara kwa kaya na jamii iliyoko kijijini, bali na fursa ya kuchota bidhaa, huduma, mawazo na tekinolojia kwa ajili ya maendeleo ya vijijini. Hii inaweza kutekelezwa wakati wahamiaji mjini wanapodumisha uhusiano na makwao. Hii hufanyija kwa kudumisha mawasiliano kati ya wahamiaji na jamaa zao vijijini kwa kutembelea vijijini, kwa kutuma bidhaa, kwa kuwa na mali wanazoziendeleza vijijini na kwa kutuma fedha. Dhana hii ya kutuma fedha imeimarishwa na matokeo ya utafiti wa karibuni juu ya wahamiaji kutoka nchi zinazoendelea kwenda nchi zilizoendelea, kitaalamu wanaitwa 'diaspora' (Mercer, et al, 2008). Inasemekana fedha zinazotumwa na diaspora kwenda nchini kwao ni nyingi zaidi ya fedha ya wahisani, na kwa hiyo ina mchango mkubwa wa maendeleo. Kwa hiyo wataalamu wetu kwenda kufanya kazi nje ya nchi, si hasara kwa taifa kama ilivyofikiriwa awali, bali ni faida. Kuna hoja kuwa wahamiaji wetu wa ndani pia wanamchango ambao unachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo vijijini, na kwa hiyo uhamiaji mjini unapaswa kuthaminiwa badala ya kubezwa. Lakini hoja hii haikubaliki kwa wote. Kutokana na hali ya miji yetu wahamiaji toka vijijini hawana nafasi nzuri ya kupata kazi na mapato ya kuweza kutekeleza wajibu kama wa diaspora.

Hata hivyo kuna wahamiaji wenye uwezo. Hawa wanaweza kuwa raslimali kwa maendeleo vijijini iwapo watathaminiwa na kupewa nafasi.

Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni kuelewa mchango wa wahamiaji kutoka vijijini wanaoishi mjini katika kuendeleza maendeleo ya vijiji vyao. Ilikufikia madhumuni haya, utafiti ulilenga:

a) Kufahamu hali ya mahusiano ilivyo kati ya wahamiaji na vijiji walikotoka.
b) Kupima kwa kiasi gani mahusiano hayo yanachangia katika kuendeleza familia zao na raslimali za vijijini kwao.
c) Kuzichambua fursa za maendeleo zitokanazo na muingiliano kati ya vijiji na miji.
d) Kutambua mbinu zinazoweza kutumika ili kuufanya uhusiano kati ya miji na vijiji uchangie zaidi kuboresha hali ya maendeleo vijijini.

Ili kuyafikia malengo haya, utafiti huu ulinuia kujibu maswali yafuatayo:

a) Kwa kiasi gani wahamiaji mjini wanauhusiano na vijijini kwao?
b) Uhusiano huo unachangia vipi katika maendeleo vijijini kwao?
c) Kwa kiasi gani uhusiano huu unaweza kuwa fursa ya kujenga maendeleo vijijini?
d) Tufanye nini ili tuweza kutumia fursa hii kwa ajili ya kuendeleza vijiji vyetu?

Eneo na Mbinu za Utafiti

Utafiti ulifanyika katika Kata na vijiji kwenye mabano: Lugoba (Lunga), Msata (Msata); na Mbwewe (Mbwewe) vilivyoko pembezoni mwa barabara kuu ya Chalinze-Segera. Pia Miono (Miono) na Kiwangwa (Kiwangwa) vilivyoko mbali na barabara kuu.Vijiji vyote vinamawasiliano mazuri ya barabara na kuna usafiri wa mabasi ya kwenda mijini kila siku. Ukusanyika taarifa ulifanyika mwaka 2009.

Jumla ya kaya 251 kutoka katika vijiji vitano zilihusika katika utafiti huu. Kaya hizi zilichaguliwa kwa kuwa zina ndugu na jamaa wanaliohamia mjini. Dodoso ilitumika kuchukua taarifa katika kaya. Taarifa za nyongeza zilipatikana kwa njia ya majadiliano na uongozi na wataalamu katika ngazi ya kata na kijiji. Pia katika kila kijiji mkutano wa viongozi wa kijiji na vitongoji ulitumika kujadili mad ya utafiti. Vitu maalum kwa nafasi zao mbali mbali kijijini kama afisa afya, daktari wa kituo cha afya, mwalimu mkuu wa shule,

n.k. walihojiwa.

Kaya 232 zenye ndugu waliohamia mijini zilishiriki kujaza dodoso. Familia zilizonyingi zina ndugu alihama kijijini kwenda kuishi mji fulani. Kaya hizi zilitoa taarifa juu watu wenyeji 615 waliohamia na waliokuwa wanaishi mijini wakati wa utafiti. Kati ya wahamiaji hawa 57% walikuwa wanaume na 43% wanawake. Mijadala ilijumuisha wajumbe wa halmashauri ya kijiji, wataalamu (wa elimu, kilimo, mifugo, afya, maendeleo, n.k.); wawikilishi wa makundi (vijana, wafanya biashara, wanawake) na watafiti ilifanyika katika kila kijiji. Viongozi wa ngazi za kata na kijiji walihojiwa.

Kiwango cha uhusiano kati ya miji na vijiji

Utafiti ulilenga kutambua kiwango cha uhusiano kati ya wanavijiji na ndugu zao waliohamia mjini. Karibu kila kaya ilikuwa na ndugu waliohamia mjini. Wahojiwa walitoa taarifa za ndugu 615 waliohamijia mjini, kwa idadi mmoja hadi watatu kwa kaya. 80% ya wahamiaji walikuwa wanaishi katika mji mkubwa wa Dar es Salaam, wakati asilimia ndogo walitawanyika katika miji midogo: Bagamoyo (4.1%); Tanga (2.4%), Morogoro (2.4%), Kibaha (2.3%) na Chalinze (1.1%). Taarifa hii ni tofauti na dhana kuwa vijiji vitahusiana zaidi na miji midogo iliyokaribu kuliko miji mikubwa iliyo mbali na inaonyesha unyonge wa miji midogo katika mfumo wa mahusiano kati ya miji na vijiji. Wahamiaji wengi (57%) walikuwa wakiishi mjini kwa zaidi ya miaka 10, karibu 20% ni wahamiaji wa karibuni (Jedwali 1).

Jedwali 1: Idadi ya Miaka ambayo wahamiaji wameishi mjini.

Idadi ya miaka	1 – 5	6 -10	11-15	16 -20	21 – 25	26 – 30	>30
Idadi ya wahamiaji	120	145	57	144	27	73	51
Asilimia (%)	19.5	23.5	9.2	23.5	4.3	11.8	8.2

Wahamiaji mjini huwasiliana na ndugu zao vijijini kwa sababu hasa za kiutamaduni. Ni jadi kumzika mtu wa makamo kijijini kwao na wajibu wa ndugu waliohamia mjini kurudi kijijini kushiriki mazishi na matukio mengine ya kiutamaduni (jando na unyago; sikukuu za kidini, n.k.) kama ilivyosehemu nyinginezo za Tanzania (Lerise, et al, 2001). Pia wahamiaji hushiriki maisha ya vijijini kwao kwa kuwa na raslimali kijijini na kuziendeleza.

Kutembelea vijijini ni kwao ni njia muhimu kwa wahamiaji kuimarisha mahusiano na ndugu zao wa vijijini. Pia ni njia inayotumiwa na wahamiaji kupeleka raslimali, kupata ufahamu juu ya hali ya maendeleo na mahitaji ya

wenzao wa vijijini na kusimamia raslimali walinazo vijijini kwao. Wahamiaji wengi (56%) hutembelea vijiji vyao mara hadi mara mbili kwa mwaka, wengine hutembelea hadi mara nne (21%) kwa mwaka. Lakini asilimia sita hawakuwahi kutembelea vijijini kwao (Mchoro 1). Kulingana na ukaribu wa miji, idadi ya safari za kurudi kijijini ni chache, ikionyesha kuwa ukaribu na mjini haujatumika kwa faida. Wahojiwa wanaeleza kuwa uchache wa safari unatokana na kipato duni cha wahamiaji. Hili linashiria uwezo mdogo wa wahamiaji kuweka raslimali kwa maendeleo ya vijiji vyao. Imeelezwa kuwa safari ya kijijini inaambatana na kupokea majukumu mengi kwa mhamiaji kiasi kwamba inawazuia kwenda vijijini mara kwa mara.



Mchoro 1: Idadi ya safari za wahamiaji kwenda vijijini kwao kwa mwaka.

Kiasi cha muda ambao wahamiaji hukaa warudipo kijijini ni muhimu kwa kuwa huhusiana na uchangiaji wao katika maendeleo kijijini. Wahamiaji 38% hukaa siku moja hadi mbili wakimbelea vijijini kwao. Robo ya wahamiaji hukaa siku tatu hadi nne (Mchoro 2). Muda huu ni mfupi kuwawezesha kufanya shughuli za maendeleo kijijini. Hali duni ya maisha vijijini inadaiwa kutowavutia kukaa kwa muda zaidi na pia kuzileta familia zao. Kwa namna hii ni mashaka kuwa kizazi kijacho kitaendeleza mahusiano kama haya kati ya familia za mjini na za vijijini.

Wanavijiji pia hutembelea ndugu zao walioko mjini. Miji midogo hutegemewa kuwa vivutio mbadala vinavyoweza kupunguza watu wa vijijini kuingia kwa wingi kwenye miji mikubwa (Hannah, 2008). Tofauti na matarajio haya safari nyingi zilielekea zaidi Dar es Salaam, ikionyesha

udhaifu katika uendelezaji wa miji midogo ya Bagamoyo, Kibaha, na Chalinze katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma za kijamii. Kukosekana kwa viwanda vya kuhudumia sekta ya kilimo katika miji midogo kunadhoofisha mchango wa miji hii katika maendeleo ya vijiji.



Mchoro 2: Kiasi cha muda ambao hukaa kijijini kwa kila walitembelea vijiji vyao (N = 604)

Kubadilishana bidhaa na huduma (kwa njia ya fedha) ni kipengele muhimu katika mahusiano kati ya miji na vijiji (Tacoli, 1998). Ubadilishanaji huu katika ngazi ya kaya unaweza kuwa njia ya wahamiaji wanaoishi mjini kuchangia maendeleo ya vijiji vyao. Wahojiwa walitaja bidhaa walizoleta kijijini walipotembelea jamaa zao wa mjini (Jedwali 2). Takwimu hizi zinaonyesha udhaifu katika kutegemeana kisekta kati ya miji na vijiji. Bidhaa muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kilimo hazipatikani kupitia kubadlishana bidhaa kati ya miji na vijiji. Biashara ya mazao haifanyiki katika ngazi ya kaya, ila ya wafanyabiashara binafsi. Kaya za vijijini hazifaidiki moja kwa moja kutokana na kubadilishana bidhaa na huduma kati ya miji na vijiji. Licha ya biashara kubwa ya mananazi kule Kiwangwa, kwa mfano, umaskini umeshamiri. Wafanyabiashara wengi si wenyeji wa vijijini, na vijana wengi ni madalali wa wafanyabiashara kutoka nje. Hii ina maana kuwa faida itakanayo na biashara haibaki kuendeleza vijiji husika.

Jedwali 2: Bidhaa na huduma zilizopokelewa kutokana safari za wakuu wa kaya kwenda mjini.

Bidhaa / huduma	Haku-na	Chaku-la	Bidhaa za viwandani	Huduma ya afya	Nguo	Elimu / ujuzi	Vitendea kazi	Vifaa vya ujenzi	Pembejeo za kilimo	Dawa za asili	Hawa kujibu
Idadi ya kaya	71	46	38	37	3	4	3	1	1	1	27
Asilimia	30.6	19.8	16.4	15.9	1.3	1.7	1.3	.4	.4	.4	11.6

N = 232

Mchango wa wahamiaji katika maendeleo ya vijiji vyao

Sehemu hii inajadili juu ya uwekezaji wa wahamiaji katika vijiji vyao kwa kutumia taarifa za ndugu zao wa vijijini. Kupatikana kwa raslimali za kijijini kwa ajili ya wahamiaji ni muhimu ili kuimarisha mahusiano kati ya miji na vijiji (Howard and Wiesner, 1977). Wahamiaji wanapomiliki raslimali vijijini inaimarisha mfungamano wao na jamaa zao wa vijijini, inawavuta kufika mara nyingi na kuwekeza vijijini. Wahojiwa walitoa taarifa juu ya raslimali zilizoko kijijini zinazomilikiwa na jamaa zao walioko mijini. Inawezekana kuwa wahojiwa hawakuweza kufahamu kikamilifu jambo hili, lakini mali ya mali za wahamiaji zilizoko vijijini haziwezikufichika.

Kati ya wahamiaji 512, 58% hawakuwa na raslimali yoyote kijijini. Raslimali zilizomilikiwa ni mashamba (15%), nyumba (11%) na viwanja vya kujenga nyumba (11%), na nyingi zilipatikana kwa njia ya kurithi. Miradi nje ya kilimo haijawavutia bado wahaniaji, pengine kwa kuwa zinahitaji usimamizi wa karibu sana na kila siku. Lakini wahamiaji wasio wenyeji wa vijiji hivi wana biashara / miradi inayoshamiri vijijini. Inawezekana wajibu wa wahamiaji wenyeji wa vijiji hivi hukwazwa na wajibu kwa ndugu zao unaoweza kudhoofisha miradi yao vijijini kwao. Pia wahamiaji wengi hawana elimu na ujuzi wa kutosha kupata ajira ya kipato kizuri mjini. Mbonile (2003) anawaona hawakuwa walihamia mijini kwa bahati mbaya. Umaskini ni sababu ya msingi kwa wahamiaji kutoweza kumiliki na kuendeleza raslimali vijijini kwao. Wazee wengine wa vijijini walilalamikia watoto wao kutokuwa tayari kuomba raslimali kutoka kwa wazazi wao ili waziendeleze.

Jedwali 3: Raslimali zinazomilikiwa vijijini na wahamiaji wanaoishi mijini

Raslimali /mali	Kiwanja cha kujenga nyumba	Nyumba	Mashamba	Nyinginezo	Hakuna	Jumla
Idadi	72	58	78	7	297	512
Asilimia	14.1	11.3	15.2	1.4	58	100

Mchango wa wahamiaji katika kuhudumia jamaa zao wa vijijini katika eneo la magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo ni mdogo. Hii inaonyesha kuwa mzunguko wa fedha, bidhaa na huduma kati ya miji na vijiji ni njia ya kujikimu tu na si tegemeo la kukuza uchumi wa vijiji kama Mbonile (1995) ilivyoona katika wilaya ya Makete. Wahamiaji huwasaidia ndugu zao wa vijijini pale tu wanapokuwa na mahitaji ya kujikimu. Utoaji wa fedha kati ya wahamiaji kwenda kwa ndugu zao vijijini, ujulikanao kama remittance, ni kidogo na hauna nguvu ya kuendeleza uzalishaji vijijini. Lerise et al (2001) waliona hali sawa na hii mkoani Lindi. Kadiri ya Mushi (2003), familia ya kijijini huvutia remittance kwa kumlea kijijini mtoto wa mhamiaji. Wahojiwa walionyesha zipo familia nyingi zinazolea watoto wa wahamiaji lakini hazihudumiwi na wazazi watoto hao kwa vile hawana uwezo. Hali hii hudidimiza zaidi kiuchumi kaya za vijijini. Hata hivyo wahamiaji wachache wameonyesha mfano katika kuchangia maendeleo vijijini kwao kwa ajili ya kuendeleza nyumba/makazi yao na jamaa zao na kuwekeza katika kilimo na miradi mbali mbali.

Njia mojawapo inayoweza kutumiwa na wahamiaji kuendeleza vijiji vya kwao ni pale wanaporejea kuishi kijijini. Ongezeko la kurejea nyumbani kwa wahamiaji limeonekana kuwa ni njia ya wao kujikimu katika ugumu wa maisha (Potts, 1995). Kuongezeka kwa hali ya umaskini kutokana na mabadiliko ya kiuchumi kumedhoofisha pato na uwezo wa wahamiaji. Kurejea kijijini kwa wahamiaji imeonekana kuwa mzigo kuliko nafuu kwa jamaa zao wa vijijini kama alivyoona Mbonile (1995) katika wilaya ya Makete.

Wahamiaji wanaweza kurejea kwenye vijiji vyao vya asili au vijiji vingine. Hii inategemea uwepo na urahisi wa wahamiaji kumiliki raslimali katika vijiji. Mabadiliko ya karibuni ya kurahisisha umiliki wa ardhi (kama inavyojadiliwa na Jussi katika mkusanyo huu wa makala) umefungua nafasi kwa wahamiaji kupata raslimali katika vijiji. 58% ya kaya zilizohojiwa hazijapata wahamiaji waliorejea kijijini. Karibu theluthi (35%) zilikuwa na mhamiaji mmoja aliyerejea na 6% zilikuwa na wawili. Wahamiaji walirejea kwa sababu mbali mbali. 61% walirejea kwa sababu ya kupungua kwa uwezo wao wa kujikimu mjini; wengine (15.7%) walirudi kuchukua majukumu ya wazazi wao waliokuwa hawajiwezi tena, na wengine kutokana na mabadiliko ya kazi (23.3%). Kurejea kwao hakuambatani na hamisho la raslimali na uwezo wa kuchangia maendeleo ya vijiji vyao. Wengi hurudi kutokana na ugonjwa, hasa yanahusiana na ukimwi (Diyamett et al, 2001). Mara nyingi kurejea huku hakukuwa kumeandaliwa. Kurejea kutokana na kustaafu kunatarajiwa kuwa na manufaa zaidi kutokana na ujuzi wa siku nyingi na mali walizonazo wastaafu (Tacoli, 2002). Lakini kutokana na elimu na ujuzi mdogo wa wahamiaji wa eneo hili tokea awali, tegemeo hili halipo.

Kurejea kijijini kwa wahamiaji kulikokuwa na manufaa kuliambatana na mhamiaji kuwa na raslimali kijijini tokea awali. Hali ni nadra lakini ya muhimu kuipa msukumo zaidi. Wahojiwa walikiri kuwepo kwa wahamiaji wenye uwezo na nguvu ya kuchangia maendeleo ya vijiji lakini walilalamikia kutojali kwao. Kata ya Msata imeonekana kufanya vema zaidi pengine kutokana na kuhamasishana kati ya wahamiaji kupitia cha chao cha MWADA. Miradi ya maendeleo kadhaa, Chuo cha Ufundi, Hoteli Nyumba za kulala wageni, maduka, n.k., (imefanikiwa kutokana na nguvu ya wahamiaji. Mchango wa wahamiaji katika ujenzi wa shule kijijini Lunga, Mboga, Msoga na Saleni na kata ya Mbwewe ni mifano mizuri.

Wahamiaji wanaoishi mijini wanaweza kuchangia maendeleo ya vijiji visivyo vyao toka awali. Wahamiajiwa namna hii wanaurahisi wa kutofungwa na jadi ya wahusika na kwa hiyo wamekuwa na mafanikio katika kuendeleza miradi na biashara. Pia kwa kuwa ni wageni katika vijiji hivyo hawafungwi na wajibu mwingi kwa wanajamii, jambo ambalo lingedhoofisha shughuli zao. Kuna mifano ya miradi mingi katika eneo la utafiti inayotoa msukumo wa maendeleo lakini inasimamiwa na wahamiaji waishio mijini wasio wenyeji wa vijiji hivi, kwa mfano nyumba za kulala wageni za Lunga na Mbwewe; duka la vifaa vya ujenzi la Mbwewe; maduka ya madawa; vyombo vya usafirishaji, zahanati, baa, n.k. Wajamiaji wasiowenyeji pia kumiliki na kuendeleza mashamba kwa kilimo, k.m. shamba la mananasi la Rais wetu kule Kiwangwa hutumika kama shamba la mfano. Wakazi wengi wa Dar es Salaam wana mashamba makubwa ya mananasi kule Kiwangwa. Hili limeambatana na wenyeji kuuza sehemu kubwa ya ardhi iliyoko katika maeneo yao ya awali kabla ya kuanzishwa vijiji, angawa si vijiji vyote ninaweza kurejea mashamba hayo ya awali kama anavyoeleza Taimi katika mkusanyiko wa makala hizi. Hapa uangalizi unahitaji kwa sababu ya hatari ya kizazi kijacho kukosa maeneo ya kilimo na ushindani utakaojitokeza kati ya wakulima wadogo na wakubwa.

Wahamiaji wanoishi mjini wanatarajiwa kuchangia maendeleo ya vijiji vyao kwa kuhamasisha mashirika maendeleo kuleta huduma vijijini. Vijiji vya eneo la magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo havina mashirika mengi na yenye huduma nyingi za kuchochea maenedleo. Baadhi ya taasisi ma mashirika yanayotajwa na wahojiwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo iliyotoa msaada wa chakula; the Foundation for International Community Assistance (FINCA) hutoa mikopo kwenye vikundi; Red Cross kule Mbwewe; Camfed International inajihusiha wanawake kule Lunga, na United Nations Children's Fund (UNICEF) husaidia elimu ya wasichana pale Msata. Taasisi nyingi zinafanyakazi zinajikita katika kusaidia wananchi kujikimu kimaisha, hakuna msukumo mkubwa katika uzalishaji wa kilimo.

Uhusiano wa miji na vijiji katika Uendelezaji raslimali vijijini

Mfumo wa uhusiano na muingiliano kati ya miji na vijiji katika sehemu ya magharibi mwa wilaya ya Bagamoyo unawawezesha wahamiaji waishio mijini kuzipata na kumiliki raslimali za vijijini kama ardhi ya kilimo, misitu na mawe yenye ubora mkubwa kwa ajili ya kutengeneza kokoto. Hili linawezekana pia kutokana na kuwepo kwa barabara kuu inayoviunganisha vijiji na miji. Lakini mchango wake katika maendeleo ya vijiji bado haujafikiwa. Hali hii ya wahamiaji kuongeza matumizi ya raslimali za vijijini kusikoambatana na hali ya maendeleo vijijini, kunapingana na imani kuwa muingiliano kati ya miji na vijiji ni tegemeo la kuleta maendeleo vijijini.

Ni dhahiri kuwa kuanzishwa kwa vijiji kuliongeza na kuimarisha muingiliano kati ya miji na vijiji na kurahisisha raslimali za vijijini kusafirishwa kwenda mijini. Kukua kwa shughuli ya uzalishaji wa kokoto pembezoni mwa barabara kuu ya Chalinze- Segera ni mfano mmojawapo. Kokoto huhitajika katika shughuli kubwa za ujenzi mijini. Kata za Lugoba na Msata zina machimbo kadhaa ya kokoto. Majadiliano katika kata hizi yalionyesha wananchi kutoridhishwa na manufaa wanayopata kutokana na miradi ya kokoto licha ya kuwa sera ya madini inatoa nafasi kwa wananchi kufaidika na miradi ya uchimbaji madini. Inadaiwa kuwa hii ilitokana na kutokuwa makini katika uandaaji na kusaini makubaliano na wawekezaji, kwani vijiji vilivyofanya vema kama vile Saleni na Pongwe Msungura vimefaidika sana na miradi ya kuchimba kokoto.

Kampuni za nje na za ndani zinazochimba kokoto hutoa ajiri kwa wenyeji, lakini wenyeji wengi ujuzi unaohitajika. Hii hutoa nafasi ya wageni kuajiriwa na kuongeza ushindani katika matumizi ya raslimali katika vijiji. Lakini kwa upande mwingine wageni hutoa changamoto nyingi za maendeleo kwani hujishirikisha katika kuendeleza makazi, miradi na biashara mbali mbali kijijini. Hili limechangia kukua kwa maisha ya kimji vijijini kama inavyoelezwa humu na makala ya Taimi. Vijiji vinaweza kufaidika zaidi iwapo ushuru uanaopaswa utatozwa kwa watumiaji wa raslimali za vijiji na sehemu kubwa ya mapato yatatumika kuendeleza miundo mbinu na huduma vijijini. Vijiji hivi husafirisha mkaa kwenda mijini. Imeelezwa na Mhache katika makala hii kuwa uchomaji wa mkaa ni chanzo cha mapato ya kaya nyingi, lakini umechangia uharibifu wa mazingira, jambo linalodhoofisha hali ya maisha vijijini. Vijiji havipati faida kutokana na ushuru wa bidhaa ya mkaa kwa vile uchomaji, uuzaji na usamnazaji mara nyinngi huufuati taratibu (Peter and Sanders, 2009). Inadaiwa kuwa uchomaji, uuzaji wa jumla na usafirishaji wa mkaa unafanywa na watu wasiokuwa wenyeji wa maeneo haya, hivyo kufanya faida yake isibadi vijijini. Kwa vile mkaa ni nishati ya bei nafuu,

vijiji vinachangia kupunguza ukali wa maisha wa watu wa mijini (Peter and Sanders, 2009).

Eneo la magharibi mwa Wilaya ya Bagamoyo, pia husafirisha mbao na bidhaa za mbao ngumu. Kuna viwanda vidogo vidogo kule Miono na Lunga vinavyotengeneza bidhaa hizo kwa ajili ya mahitaji ya wajenzi wa mjini. Ukaribu na misitu ya asili katika kata ya Miono umeifanya kata hii kuwa chanzo kikubwa cha mbao ngumu kwa ajili ya ujenzi jijini Dar es Salaam ambako kunashamiri shughuli za ujenzi. Biashara isiyokuwa ya haki inajulikana kuwa ni chanzo cha wazalishaji vijijini kukosa mapato wanayostahili. Wanavijiji hupoteza mapato kutokana na mifumo ya uuzaji isiyowatendea haki. Mwanakijiji mmoja wapo wa Miono alidai: "S*oko huria linadidimiza uchumi wa kijiji."* Wageni wameshika sehemu muhimu za biashara ya mazao na mali asili kiasi kuwa mapato kutokana na biashara hizi hayatumiki kwa maendeleo ya vijiji hivi. Wanavijiji hulalamikia bei duni ya mazao wanaposhindwa kupata bei nzuri kutokana na udhaifu wa mkulima mmoja mmoja kuuza mazao kwa wafanyabiashara laghai. Wanunuzi ndio waamuzi wa bei na hufanya hivyo kwa kutumia vema udhaifu wa wakulima wasioungana. Biashara isiyo ya haki hutokea pia kwa njia ya kutumia vipimo visivyo vya viwango. Ili kuepukana na hali hii, kule Mbwewe kumeanzishwa ushirika wa wakulima na wafugaji unaonuia kupunguza nafasi ya mfanyabiashara wa kati ili kumwongezea mapato mkulima.

Tunachojifunza kutokana na Utafiti huu

Utafiti huu umeonyesha hali ya uhusiano wa miji na vijiji katika eneo hili lililo pembezoni licha ya ukaribu wake na mji mkuu wa Dar es Salaam. Miundo mbinu mizuri imerahisisha usafirishaji wa watu, bidhaa na hudma kati ya vijiji na miji. Hata kwa kuwa pembezoni mwa mfumo wa uchumi uliopo, vijiji vinaathiriwa na muingiliano na miji. Wananchi wa vijijini hupoteza raslimali kutokana na udhaifu wao na kwa njia ya tathmini, utozaji ushuru na ugawaji wa mapato ulio duni. Hili ni changamoto kwa watunga sera na wapangaji wa mipango. Mwongozo unahitaji kuhakikisha kuwa wanavijiji wanafaidika zaidi na raslimali zilizomo katika maeneo yao.

Kuongezeka kwa hali ya umaskini mijini kunaufanya mfumo wa mungiliano kati ya miji na vijiji uwe wa kujikimu zaidi kuliko kuwa kichocheo cha maandeleo vijijini. Ili muingiliano huu uwe wa manufaa zaidi vijijini kuna haja ya kujenga uwezo zaidi wa wahamiaji wanaoishi mjini wa kujipatia mapato na uwezo wa miji kusaidia shughuli za kiuchumi vijijini. Uendelezaji wa viwanda mijini uahitajika. Vijijini pia kunahaja ya kuwaendeleza wananchi

ili wanapohamia mijini wawe na elimu na ujuzi wa kuwawezesha kupata ajira na kipato kizuri zaidi. Kama Mushi (2003) anavyoona, muingiliano kati ya maeneo ya pembezoni na jiji la Dar es Salaam haujaweza kuleta mabadiliko makubwa katika kilimo vijijini. Uendelezaji wa miuondo mbinu na huduma vijijini ni muhimu ili kuwa kivutio cha wawekezaji, lakini hili liambatane na uhakikishaji kuwa wananchi wanapata haki katika uchumi wa raslimali zilizoko vijijini kwao. Kuwawezesha zaidi wanavijiji kwa kuanzisha ushirika ni muhimu. Pia mwongozo bora zaidi kwa wawekezaji juu ya umiliki wa ardhi na raslimali zingine unahitajika.

Ingawa sehemu kubwa ya wahamiaji waishio mijini wanakosa msingi mzuri wa kuendeleza vijijini kwao, kuna baadhi ya wahamiaji wachache wenye raslimali na kipato cha kutosha kuweza kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya vijijini. Kuna haja ya kushawishi na kuhamasisha matumizi ya nguzo hii ya uchumi wa vijiji. Kuweka mazingira ya kuwavutia vijijini kwa kuboresha miundo mbinu na huduma ni muhimu. Kuanzishwa kwa vyama vya hiari vinavyowaunganisha wahamiaji wanaoishi mijini kutasaidia kuwaunganisha, kuwahamasisha ili kuchangai maendeleo ya vijijini kwao kama ilivyoonekana Msata ambako MWADA imechangia vema kuendeleza shughuli za maendeleo katika kata. Uongozi wa kata na vijiji ufanye juhudi ya makusudi kuwatambua na kuwashirikisha wahamiaji wao mmoja mmoja au kwa pamoja, katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo. Woga kuwa vyama vya wahamiaji vinatajenga ukabila na ujimbo unaweza kuondoka iwapo kwa njia za utawala bora.

Utafiti huu uneonyesha kuwa miji midogo ina udhaifu katika kuchangia maendeleo ya vijijini kwa kuwa inamezwa na nguvu ya jiji la Dar es Salaam. Kuna haja ya kuendeleza zaidi uchumi wa miji midogo kwa kukuza viwanda vinavyolenga kuboresha kilimo. Utafiti huu unahitimisha kuwa, bila kuongozwa vema, muingiliano kati ya vijiji na miji, unaweza kuwa kikwazo cha maendeleo vijijini kwa kuwa unaruhusu raslimali kutoka vijijini kwenda mjini lakini kwa kutoa manufaa kidogo kwa wanavijiji. Hili ni eneo ambalo linatakiwa kuangaliwa na watunga sera na vikundi vya kijamii ili kuhakikisha kuwa maeneo ya vijijini yananufaika kutokana na raslimali zao na pia kutokana na mahusiano kati ya vijiji na miji.

Machapisho

Diyamett, Bitrina; Mathew Diyamett; Jovita James and Richard Mabala (2001),
The case of Himo and its region, northern Tanzania. Working paper series on rural-urban interactions and livelihood strategies, Working Paper No 1, IIED, London

Lerise, Fred, Anthony Kibadu, Esther Mbutolwe and Nimrod Mushi (2001), Rural-urban interactions and Livelihood strategies: The case of Lindi region, Southern Tanzania. IIED, London, 32 pages.

Mbonile, Milne J (2003), Absentee farmers and change in land use management on Mount Kilimanjaro, Tanzania. LUCID Working papers series, Paper No 24, ILRI, 22 pages

Mbonile, Milne J (1995), "Structural adjustment and rural develop- ment in Tanzania: the case of Makete District". In Simon D., van Spengen W.,

Dixon C. and Narman A. (Eds), Structurally adjusted Africa: poverty, debt and basic needs, Pluto Press, London,

Mercer, Claire; Ben Page and Martin Evans (2008), Development and the African diaspora: Place and the politics of home, Zed Books, London.

Mushi, Nimrod S., (2003), Regional development through rural-urban linkages: The Dar-es Salaam impact region. A Thesis submitted to the Faculty of Spatial Planning, University of Dortmund in fulfillment of the requirement of the award of a Dr. rer. pol. Degree.

Peter, Christian and Klas Sanders (2009), Environmental crisis or sustainable development opportunity? Tranforming the charcoal sector in

Tanzania. A Policy Note. World Bank, pages, 230 pages.

Potts, Deborah (1995), "Shall we go home? Increasing urban poverty in African cities and migration processes", The Geographical Journal Vol 161 No 3 pages 245-264.

Tacoli, C., (2002), Changing rural-urban interactions in sub-saharan Africa and their Impact on livelihoods: a summary. Working papers Series on Rural –Urban Interactions and Livelihood Startegies. Working Paper no 7, IIED.

Tacoli, Cesilia (1998), "Rural urban interactions: A guide to the literature, Environment and Urbanization Vol 10 No 1 pages 147-166.